# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

**Kikao cha Tano – Tarehe 4 Novemba, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Dkt. Joseph K. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali. Tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Meshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 68

**Serikali Kutenga Asilimia Tano kwa Kila Mradi kwa Ajili ya Vijana**

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kutenga walau asilimia tano kwa kila mradi wa kisekta ili kuwagusa vijana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua na kuthamini umuhimu wa kuwawezesha vijana katika kila sekta. Kwa sasa, Serikali inawezesha makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na: -

(i) Kutenga 30% ya zabuni itakayotekelezwa katika Halmashauri zote nchini;

(ii) Kupitia mapato ya ndani ya halmashauri zote nchini, Serikali imeendelea kutenga 10% ya mapato; asilimia nne kwa ajili ya vijana, asilimia nne kwa ajili ya wanawake, na asilimia mbili kwa ajili ya watu wenye ulemavu kwa masharti nafuu; na

(iii) Kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana inawezesha miradi ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kushirikiana na sekta mbalimbali kutathmini na kuboresha sera na miongozo yake ili kuhakikisha kuwa vijana wanaendelea kutengewa fedha kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miradi pamoja na kuwekewa sera rafiki zaidi kuwawezesha kujipatia mitaji, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Latifa, swali la nyongeza.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa nini sasa Serikali haioni haja kupitia Wizara hii ya Vijana, kuandaa na kuratibu mipango mbalimbali ya kuzisimamia Wizara za Kisekta, ikiwemo Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda, Wizara ya Madini, na Wizara ya Biashara, ambazo zinaenda kuwagusa vijana moja kwa moja ili kutenga angalau asilimia tano

ya kuweza kuwa-*push* vijana ili kuondokana au kupunguza tatizo hili la ajira? Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Latifa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari kwa maagizo yake mahususi ameshaanza kutekeleza hicho Mheshimiwa Mbunge anachokisema. Kwanza, katika Wizara zote ilikuwa ni maagizo mahususi ya Mheshimiwa Rais na maelekezo ya utekelezaji ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwamba kwenye Wizara zote za kisekta ambazo zitapewa bajeti kwa mwaka wa fedha zihakikishe zinatenga fedha kwa ajili ya kutengeneza fursa za ajira, na kuandaa mazingira ambayo yatawasaidia vijana kuweza kupata nafasi mbalimbali za kupata kazi kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo kwenye Wizara ya Kilimo, tuna programu ya *Building Better Tomorrow*, Wizara ya Viwanda na Biashara tuna mradi ambao uko upande wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambako wananchi zaidi ya 24,000,000 wamekuwa wanufaika kwa shilingi trilioni 2.8 kwa ajili ya kupewa fedha za mitaji mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye Wizara ya Madini tumeanzisha programu ya *Mining for Brighter Tomorrow* ambayo tayari tumeshaanza kuwatambua vijana kwenye uchimbaji, kuwapa vitalu vya kuchimba na kuwawezesha vifaa na kwenye Wizara nyingine ya Biashara na Viwanda nako tunaendelea kutanua ajira ikiwa ni pamoja na kurekebisha sera yetu ya uwekezaji ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ipo Wizara nyingine ya Fedha ambayo tuna fomu maalumu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Fomu Na. 15A na 15B inazotaka Wizara ya Fedha kuwasilisha kwenye miradi ya maendeleo, fedha zote zinazotolewa kwenye

mwaka wa fedha kwenda kwenye miradi mikubwa na ya kimkakati ya maendeleo, kuona ni ajira ngapi za moja kwa moja zinazozalishwa kwa ajili ya vijana, na mitaji na inawezeshwa kwa namna gani pamoja na Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, niishie hapo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunahamia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki aulize swali lake.

Na. 69

**Kuigawa Kata ya Mwangeza – Iramba**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaigawa Kata ya Mwangeza kuwa Kata za Ikulu, Mwangeza na Dominila na Vitongoji vya Midimbwi, Nyeri na Mulumba kuwa Vijiji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Katimba, Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala upo kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura ya 287 na 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014. Aidha, utaratibu umeainishwa kwa kuanza na vikao vya ngazi za vijiji, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mkoa kisha kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa tathmini ya vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa sasa Serikali imetoa kipaumbele kuboresha na kukamilisha miundombinu

msingi kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadaye kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Isack Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, napenda kutoa taarifa kwamba taratibu zote zimefuatwa kwa muda mrefu na siyo zaidi ya mara moja. Kwa majibu haya, nilikuwa naomba Serikali iniambie ni lini itapeleka hizo huduma za kipaumbele kama shule ya sekondari na kituo cha afya kwenye Kata hii ya Mwangeza ambayo kutoka mwanzo wa kata mpaka mwisho wa kata ni zaidi ya kilometa 70 na Watanzania wanapata tabu sana kwenda kufuata huduma hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imesema itaboresha huduma, naomba Serikalii iniambie leo, kituo cha afya na sekondari vitapelekwa lini katika kata hii ili kuondoa adha kubwa ya wananchi wa Mwangeza wanayoipata katika Jimbo langu la Mkalama? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya ya uwakilishi katika jimbo lake. Kama nilivyotangulia kusema kwamba kipaumbele cha Serikali kwa wakati huu ni kuimarisha Serikali za Mitaa zilizokuwepo kwa kuhakikisha inasogeza huduma karibu na wananchi na kuhakikisha kwamba inajenga miundombinu ya msingi kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nichukue nafasi kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imekuwa ikifanya hivyo kupitia miradi tofauti tofauti. Mathalan, kwenye Sekta ya Elimu, Serikali inajenga shule za sekondari kupitia Mradi wa *SEQIP*. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba

Serikali italeta fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule ya sekondari katika kata hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ombi lake la kituo cha afya, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba inaimarisha huduma za Afya Msingi, na kila mwaka Serikali inatenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha inaboresha miundombinu, na kununua vifaa na vifaatiba kwa ajili ya kutoa huduma za afya msingi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka huu wa fedha, 2023/2024 kwa kadiri alivyoainisha kipaumbele cha kituo cha afya, atapatiwa fedha kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya katika jimbo lake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tuna taarifa ya udhuru kwa Wizara ya Afya. Mheshimiwa Naibu Waziri nakuruhusu urejee kwenye kiti chako, umemaliza kujibu maswali ya TAMISEMI. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante, tunakushukuru.

Tunahamia Wizara ya Afya, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake kwa niaba ya Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 77

**Kuhuisha Taasisi ya Lishe Nchini**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja kuhuisha Taasisi ya Lishe badala ya kuifuta kabisa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mollel, Naibu Waziri, Wizara ya Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya ilipokea maelekezo ya kufutwa Taasisi ya Chakula na Lishe *(TFNC)* kupitia

tamko la Serikali lililotolewa na Msajili wa Hazina tarehe 15 Desemba, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya inatarajia kuanzisha Programu ya Taifa ya Lishe pamoja na kuanzisha Kitengo cha utafiti wa lishe katika Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR)*. Hivyo, yale majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na *TFNC* yatafanyika kwa upana wake na Programu ya Taifa ya Lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Wizara imeshaanza mchakato wa kuanzisha programu ya lishe.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mariam, karibu.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa lishe katika nchi yetu imekuwa na changamoto kubwa sana, tunashuhudia watu wakiwa na uzito wa kuzidi, lakini wengine wakiwa na upungufu kabisa wa uzito wa chini hali ambayo inasababishwa na ukosefu wa lishe bora, je, Serikali haioni haja ya kuhakikisha au kupanga mpango wa haraka ili kuhuisha taasisi hii ili iweze kufanya kazi kwa wananchi wetu waweze kupata lishe bora au elimu bora zaidi kwa kutumia taasisi hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa sababu siku zote amekuwa ni Mbunge anayefatilia masuala ya afya kwenye mkoa wake na hasa zaidi anavyofuatilia wagonjwa mbalimbali kwenye makundi mbalimbali waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza amesema tumetoka kwenye eneo ambalo tulikuwa tunapambana na ukondevu. Nchi yetu kwa sababu ya kupiga *stage* ya kimaendeleo na kazi kubwa ambayo imefanywa na Rais wetu na Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi, leo tunapambana na watu kula vyakula kwa maana ya kuongezeka uzito mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Mbunge, ndiyo maana tunakwenda kuanzisha hii programu ya lishe. Nataka kuwahakikishia kuwa elimu itaenda kutolewa kwa kasi kubwa sana na ndiyo maana wakati wote nimekuwa nikiwasisitiza Wabunge na Watanzania kwamba elimu mbalimbali zinazotolewa na wataalamu wa afya, lakini elimu anayoitoa Mheshimiwa Prof. Janabi na Madaktari wengine wote, tuhakikishe tunasikiliza na kufuatilia ili tuweze kuishi maisha ya afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante, tunakushukuru. Naomba mniruhusu turejee Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda, sasa aulize swali lake.

Na. 70

**Ujenzi wa Vituo vya Afya – Busanda**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya Kata za Lwamgasa, Nyakagomba na Magenge – Busanda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati. Hadi kufikia Septemba, 2024 Serikali ilikuwa imekamilisha ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya 898 ambavyo vinatoa huduma ngazi ya kituo cha afya ikiwa ni pamoja na huduma za upasuaji wa dharura vikiwemo Vituo vya Afya vya Bukoli na Nyakagwe kwa thamani ya shilingi milioni 400 katika Jimbo la Busanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kujenga vituo vya afya katika kata za kimkakati kote nchini, zikiwemo kata

zitakazokidhi vigezo katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tumaini Magessa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa vituo 898 hadi Septemba, 2024. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya kwenye Kata ya Nyakagomba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini Serikali itajenga vituo vya afya kwenye Kata ya Lwamgasa na Magenge?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, hakika amekuwa akifuatilia sana kuhakikisha kwamba miradi ya maendeleo inafika katika jimbo lake na inanufaisha wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba niyajibu maswali yake yote mawili kwa pamoja. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya uwekezaji mkubwa sana katika kuimarisha huduma za afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitatu, jumla ya shilingi trilioni 1.18 zimetumika katika kuhakikisha kunajengwa miundombinu mizuri kwa ajili ya kutoa huduma ya afya msingi, lakini pia kununua vifaa na vifaatiba. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika Kituo hiki cha Afya cha Nyakagomba ambacho ameomba na ninaamini ni kipaumbele kabisa katika jimbo lake, basi katika mwaka huu wa fedha zitatoka fedha kwa ajili ya kuja kuanza kujenga kituo cha afya cha kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nichukue nafasi hii kuwatangazia Wabunge wote kwamba, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutambua umuhimu na uhitaji wa kuimarisha huduma za afya msingi, basi na kwa kusikia vilio vya Waheshimiwa Wabunge vya uhitaji wa vituo vya afya katika majimbo yao, katika huu mwaka wa fedha naomba mfahamu na mpokee taarifa kwamba nyote mtapata fedha kwa ajili ya kuanza kujenga vituo vya afya vya kimkakati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali iliahidi kutujengea kituo cha afya cha kimkakati kwenye Kata ya Busolwa na Mheshimiwa Naibu Waziri amesema mwaka huu fedha zitapelekwa, je, anatuhakikishia na sisi tupo kwenye hiyo fedha itakayopelekwa kwa mwaka huu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, hakika amekuwa akifanya ufuatiliaji mkubwa sana kuhakikisha kwamba kituo cha afya cha mkakati kinajengwa katika jimbo lake. Naomba nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba katika mwaka huu wa fedha kituo cha afya kinajengwa katika kila jimbo. Pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika jimbo lake atapata fedha kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya cha mkakati.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Kata ya Ndanto ina wakazi zaidi ya 17,984, na pia Kata ya Kiwila kwa Sensa iliyopita ina wakazi 36,000, Serikali haioni sasa ni wakati wa kujenga vituo vya afya katika hatua hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia masuala mbalimbali ya maendeleo kwa watu wake. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kufanya uwekezaji katika eneo la kuimarisha afya ya msingi na katika mwaka huu wa fedha kila jimbo majimbo 214, kila jimbo litapata fedha kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya cha kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ipo kazini na itawafikia kwa ajili ya kuanza kujenga kituo hicho cha afya cha kimkakati katika eneo analoliwakilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama Naibu Waziri alivyoeleza kwamba fedha zitatoka kwenye kila jimbo, sasa nataka nijue, ni lini sasa fedha hizo zitatolewa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Utili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya ya uwakilishi katika jimbo lake. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge akae kwa mkao wa kupokea wakati wowote katika mwaka huu wa fedha, fedha zitateremshwa kwa ajili ya kuanza kujenga vituo vya afya katika majimbo 2,114. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa na kwenye jimbo lake naye atapata fedha hizi kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya cha kimkakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Geita lina vituo vya afya vinne vilivyokamilika kikiwemo

Kituo cha Ibisabageni, Bugarama, Kasota, Kakubiro na vituo vyote hivi havijapata vifaatiba. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kulitembelea jimbo langu ili aweze kujionea baadaye atuletee fedha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, hakika anafanya kazi kubwa sana ya uwakilishi katika jimbo lake. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa siyo tu kwamba niko tayari kuambatana naye kwenda kuangalia mazingira katika vituo vya afya alivyovitaja, lakini naomba nimhakikishie kwamba katika mwaka huu wa fedha zimetengwa fedha mahususi kabisa kwa ajili ya kuhakikisha vituo vya afya na zahanati zote zinaweza kupatiwa fedha kwa ajili ya kununua vifaa na vifaatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zitakuja kwa ajili ya kuhakikisha huduma za afya msingi zinaboreshwa katika jimbo lake, kwa kuhakikisha vifaa na vifaatiba vinapatikana katika vituo vya afya alivyovitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Phillipo Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Sisi kule Songwe vituo viwili wananchi wameshajitolea; Kata za Namkukwe na Kanga wameshajenga maboma yameisha. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema mwaka huu Mheshimiwa Rais ametoa fedha kwa ajili ya kuunga mkono kila kituo cha afya kwenye majimbo yetu, lakini kule Songwe tayari vituo viwili vimekamilika na bado kuletewa fedha tu. Naomba anihakikishie kwamba nasi tutapata fedha katika vituo hivyo viwili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwasemea wananchi wake, lakini niendelee kutoa msisitizo katika majibu niliyoyatoa awali kwamba katika mwaka huu wa fedha kila jimbo, majimbo 214 yatapatiwa fedha kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya cha kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge naye kwenye jimbo lake atapata fedha hizo kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya cha kimkakati pamoja na kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma ya afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imetenga fedha mahususi kwa ajili ya kununua vifaa na vifaatiba ili vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya viweze kuwa na vifaa vya kisasa na viweze kutoa huduma iliyo bora. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha katika mwaka huu wa fedha zipo na zinasambazwa nchi nzima kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya msingi vinapata vifaa na vifaatiba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Kata ya Ibumu watapatiwa kituo cha afya kwa sababu kata ya jirani ya Image pia hawana kituo cha afya, pamoja na kuwa wananchi wamekuwa wakijichangisha ili kituo cha afya kijengwe na wamekuwa wakitembea umbali mrefu sana kwenda mpaka Ilula kufuata matibabu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ya

uwakilishi, lakini naomba niendelee kusisitiza na kukumbusha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kufanya uwekezaji katika huduma ya afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zimetengwa katika mwaka huu kuhakikisha kwamba kila jimbo linapatiwa fedha kwa ajili ya kuanza kujenga kituo cha afya cha kimkakati lakini katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita zaidi ya shilingi trilioni 1.186 zimetoka kwa ajili ya kuhakikisha inajenga miundombinu ya kutolea huduma ya afya msingi na kununua vifaa na vifaatiba. Kwa hiyo, Serikali itaendelea na jitihada hizo ili kuhakikisha inaimarisha utoaji wa huduma ya afya msingi katika maeneo aliyoyataja.

**MWENYEKITI:** ahsante, Mheshimiwa Zuena Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha afya cha Gonyaza kilichopo Kata ya Suji - Same Mashariki ni kituo ambacho kinahudumia watu wengi sana na kutokana na jiografia yake ya milima, wananchi wanapata shida sana, lakini kituo hicho kinasuasua katika ujenzi wake. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ya uwakilishi anayoifanya. Naomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha inaimarisha utoaji wa huduma ya afya msingi na inafanya hivyo kwa kuhakikisha inaboresha miundombinu ikiwemo ya ujenzi wa vituo mbalimbali vya kutolea huduma ya afya msingi kama hospitali, zahanati pamoja na vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kituo cha afya alichokitaja Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie kwamba Serikali itahakikisha kituo hiki kinakamilika na kinaweza kupatiwa vifaa na vifaatiba

pamoja na watumishi wa kada ya afya ili kiweze sasa kuanza kutoa huduma za afya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Songambele Wilayani Kyerwa ni miongoni mwa kata ambazo tulizileta kama kata za kimkakati. Mheshimiwa Naibu Waziri ananihakikishiaje kwa sababu ya umuhimu wa kata hii? Yuko tayari kupelekea fedha ili kituo cha afya kianze kujengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya ya uwakilishi, lakini naomba niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuimarisha utoaji wa huduma ya afya msingi; na kwa sababu Mheshimiwa Mbunge amekuwa akipaza sauti kuomba kupatiwa kituo cha afya katika Kata ya Songambele, na kwa kuwa katika mwaka huu wa fedha zitatoka fedha kwa ajili ya kuanza kujenga vituo vya afya vya kimkakati katika majimbo 214, na kwa kuwa Kituo cha Afya cha Kata ya Songambele kitakuwa kinakidhi vigezo vinavyohitajika, nimhakikishie kwamba nacho kitapatiwa fedha katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaenda swali linalofuata. Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mbunge wa Muleba Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 71

**Ujenzi wa Barabara Kata ya Rutoro - Muleba Kaskazini**

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE** aliuliza:-

Je, lini Barabara ya Kata ya Rutoro itajengwa kwa kuwa maombi yalishawasilishwa *TARURA*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya usanifu kwa kiwango cha changarawe kwa barabara za Kata ya Rutoro zenye jumla ya kilomita 67.6 ambazo zimekisiwa kugharimu shilingi bilioni 8.078. Aidha, katika mwaka 2023/2024, Serikali imetumia shilingi milioni 445 kwa ajili ya ufunguaji na matengenezo ya barabara ya Kishuro - Mishambya katika Kata ya Ngenge, yenye urefu wa kilomita 13 kwa kiwango cha changarawe pamoja na ujenzi wa makalavati 44 ambayo yamekamilika na madaraja madogo matatu ambayo yako hatua za mwisho za ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuzipa kipaumbele barabara za Kata ya Rutoro ili zifunguliwe na kupitika kwa kipindi chote kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles John Mwijage.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru na kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Samia kwa namna ilivyotutendea haki kwenye miundombinu ya barabara chini ya *TARURA;* nimebaki na deni Rutoro na Bumbile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali mawili ya nyongeza ni kwamba mkandarasi aliyejenga kilomita 13 za Kata ya Ngenge kuelekea Rutoro anadai pesa zaidi ya shilingi milioni 500, na hiyo kilomita 13 karavati zimeachwa wazi, yaani watu hawawezi kupita kwa sababu kijana amefulia, ni mjasiliamali, alikuwa ameanza, sasa amefulia. Naomba Serikali mumpatie uwezo angalau wa kufukia karavati ili liweze kupitika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Eneo la Kata ya Rutoro ambalo nina imani Serikali itatekeleza ahadi yake, walipata matatizo makubwa ya *El-Nino,* barabara zinazopitika hizo za panya zikapata makorongo. Ombi langu, naomba Serikali mtutengenezee karavati, msipige greda, mtutengenezee karavati

kwenye yale maeneo makorofi ili tukae tukisubiri kuja kupata hiyo ahadi kubwa ya bajeti ya mwaka ujao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, hakika amekuwa akipaza sauti yake kuhakikisha kwamba maendeleo yanapelekwa katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na maswali yake yote mawili, kwanza haya ni maombi, nimeyapokea, nasi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia *TARURA* tutayafanyia kazi ili tuweze kufanya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kuhusiana na hili swali kwamba mkandarasi ana madai ya shilingi milioni 500, hili kwa upekee kabisa naomba Mheshimiwa Mbunge tukae kwa pamoja tufanye ufuatiliaji ili wakandarasi wetu waweze kuwezeshwa kufanya kazi hizi ambazo wanazifanya za kuboresha miundombinu katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na fedha hizi za kuchonga na kutengeneza makaravati katika barabara hii ya Rutoro, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nimelibeba suala hili kwa uzito mkubwa sana na kwa sababu yeye binafsi amekuwa akilizungumzia mara nyingi, tunalifanyia kazi na litapata majawabu kwa sababu Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inataka kuboresha miundombinu ya barabara kwa kutambua umuhimu wake kiuchumi na kijamii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia leo imetimia miezi 11 Kata za Kibata na Kata ya Tandawale hazina mawasiliano kabisa ya Barabara na Makao Makuu ya Tarafa ya Kipatimu. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya

ujenzi wa haraka ili kuhakikisha kwamba shughuli za kiuchumi na kijamii katika kata hizo mbili muhimu zinaendelea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwasemea wananchi wake. Naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imeongeza kwa kiwango kikubwa bajeti ya *TARURA* kutoka shilingi bilioni 275 mpaka sasa kila mwaka inatengwa shilingi bilioni 710.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa katika mwaka uliopita kumekuwa na madhara makubwa katika barabara zetu hizi hasa hizi barabara zinazosimamiwa na *TARURA* kutokana na *El-Nino,* basi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imetambua mahitaji ya kuongezeka kwa bajeti na ndiyo maana Mheshimiwa Rais ameongeza bajeti ya dharura kutoka ya shilingi bilioni 21 kwa mwaka mpaka kufikia shilingi bilioni 254.3 katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inaboresha na inarekebisha miundombinu ambayo imeharibika ili wananchi waweze kupata miundombinu iliyo bora, iweze kuwanufaisha kijamii na kiuchumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wilaya ya Makete ni moja kati ya Wilaya ambazo zimepata changamoto ya kuharibika kwa Barabara, tunaishukuru Serikali imetoa fedha kwa ajili ya kujenga Barabara ya Itundu, Barabara ya Mang'oto, Barabara ya Ibaga, Barabara ya Kinyika, lakini kumekuwepo na changamoto ya wakandarasi wamesaini mikataba, *site* hawajaja. Mheshimiwa Waziri ipi ni kauli yako kwa wakandarasi wote ambao hawajaja kujenga Barabara ya Makate wakati Serikali imewapatia fedha? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ya uwakilishi katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la Mheshimiwa Mbunge naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI kuendelea kusisitiza mameneja wote wa *TARURA* wa ngazi ya mkoa, na wilaya kuhakikisha wanafanya usimamizi wa miradi hii ya barabara. Wakandarasi wanapokuwa wamepatikana, na fedha zikiwa zimetoka, wajibu wa msingi ni kusimamia kuhakikisha kwa uharaka kabisa miradi hii inatekelezwa na wananchi wanaweza kupata barabara zilizobora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumsisitiza Meneja wa *TARURA* wa mkoa huu aweze kuhakikisha kwamba anaenda kusimamia miradi yote ya ujenzi wa barabara ambazo fedha zake zimetoka na wakandarasi wamepatikana ili waweze kujenga barabara hizi kwa wakati ikiwemo Makete. Kwa hiyo, Meneja wa *TARURA* wa Makete pia ujumbe huu unamhusu, asimamie kwa ukamilifu kuanza utekelezaji wa miradi pamoja na kuikamilisha kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nami kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Ni lini Serikali itajenga barabara kutoka Rau kuelekea Materuni ambako kuna maporomoko na watalii wengi wanafika kule, lakini wanashindwa kufika kwa wakati kutokana na barabara mbovu na hivyo Serikali kukosa mapato? Ni lini sasa Serikali itajenga barabara hii ya kimkakati? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa uwakilishi wake mzuri, lakini kuhusiana na swali lake naomba niendelee kukumbusha kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba inaimarisha barabara zetu hizi hasa zinazosimamiwa na *TARURA* ambazo ni barabara zetu za wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaona kwamba bajeti ya *TARURA* imeongezeka kutoka shilingi bilioni 275 mpaka shilingi bilioni 710 kila mwaka. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kufikia barabara nyingi zaidi na kuziweka katika hali iliyo nzuri kwa ajili ya kuhakikisha kwamba haikwamishi miradi mbalimbali na shughuli mbalimbali za kiuchumi na za kijamii. Kwa hiyo, tumelipokea ombi la Mheshimiwa Mbunge na tutalifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Wabunge.

Tunaenda Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kwa niaba yake litaulizwa na Mheshimiwa Daimu Mpakate.

Na. 72

**Miradi ya Kimkakati – Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE K.n.y. MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, ni Miradi mingapi ya kimkakati imetekelezwa katika Wilaya ya Tunduru?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati katika Wilaya ya Tunduru kama ilivyo katika wilaya nyingine na miradi hiyo ipo katika sekta zote; sekta ya elimu, Sekta ya afya, nyumba na maeneo mengine. Kwa mfano, katika Wilaya ya Tunduru, anafahamu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea na ukarabati mkubwa wa ukarabati mkubwa wa hospitali ya wilaya, ujenzi wa vituo vya afya na kadhalika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daimu Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Mji wa Tunduru unakua kwa kasi kubwa sana kwa ajili ya maendeleo ambayo nimeyazungumza pamoja na uwepo wa soko la madini, lakini kuna changamoto soko la mazao mchanganyiko, tulilokuwa nalo kwa sasa halikidhi haja ya mahitaji ya watu wa Tunduru. Je, Serikali ina mpango gani kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kujenga soko la kisasa la mazao mchanganyiko ili kuweza kuwahudumia wananchi wa Tunduru?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Jimbo la Tunduru Kusini linapakana na Msumbiji. Wananchi walio karibu na Msumbiji wanakuja Tanzania kufuata bidhaa mbalimbali za madukani. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuweka soko la kimataifa katika Kijiji cha Lukumbule ili kurahisisha biashara kati ya Msumbiji na Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, karibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge kama anavyofahamu tupo katika kipindi cha kuandaa Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa Mwaka 2025/2026. Kwa hiyo, tunayachukua haya kama mawazo yake kwamba ni muhimu yaingie katika mpango ujao, lakini nakiri kwamba yote haya ambayo ameyaeleza, uwepo wa soko la mazao ni muhimu, na pia uwepo wa soko la kimataifa kama ilivyo katika maeneo mengine kama Namanga, ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachukua katika mpango ujao wa maendeleo tuingize, naye kupitia kikao hiki ambacho kinaendelea hapa atoe mchango wake kama ushauri, nasi Serikalini tuchukue ili kutengeneza taratibu zetu na mipango, basi iingie katika mpango wa fedha ujao, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako kwa Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali Na. 73, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, swali la Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mbunge wa Chakechake litaulizwa na Mheshimiwa Abdul-Hafar Idrissa Juma.

Na. 73

**Tathmini ya Athari za Maji ya Bahari Kwenye Mashamba ya Mpunga – Chakechake**

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA K.n.y. MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN** aliuliza:-

Je, lini tathmini ya athari za kimazingira zitokanazo na maji ya bahari kwenye mashamba ya Mpunga - Bonde la Tibirinzi Chakechake itafanyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mbunge wa Chakechake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya tathmini ya mazingira katika eneo la Tibirinzi ambapo matokeo ya tathmini hiyo yalibainisha kuwa

jumla ya hekta tano zimeathirika kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepanga kukusanya taarifa za kina zitakazowezesha kubaini athari za kimazingira na kijamii katika maeneo yanayovamiwa na maji ya bahari ikiwemo eneo la Tibirinzi ili kubaini viwango vya athari na hatua za kuchukua katika kukabiliana na athari hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul-Hafar.

**MHE. ABDUL-HAFAR IDRISSA JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Je, Serikali ina mpango wa kuwashirikisha, ama itawashirikishaje wananchi wakati wa kufanya tathmini ya mazingira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Serikali ina mpango wa kuwalipa fidia au kuwapa chochote wananchi wa kaya walioathirika na athari za kimazingira, hasa zinazotokana na bahari kusogea juu katika ardhi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suleiman Ramadhan ambayo yameulizwa kwa niaba yake. Ni kweli kabisa kwamba, wakati wote wa shughuli za utafiti wa maeneo yale kuangalia zile athari mara nyingi wananchi wote wanashirikishwa. Kwa hiyo, namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi watashirikishwa ipasavyo kwa sababu ndiyo waathirika wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili linalohusu fidia, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi ni kwamba tunaendelea kufanya tafiti za kina kujua athari zenyewe na kupata thamani halisi juu ya uharibifu ule. Hivyo, baada ya kukamilisha zoezi hilo, Serikali itaangalia namna yoyote ya kuwasaidia wananchi kama ni kujenga kingo au namna yoyote ile ambayo itarahisisha kuwafidia wale wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halifa Mohammed Issa, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mtambwe katika Kisiwa cha Mtambwe Mkuu ni katika maeneo ambayo bahari imevamia sana makazi ya watu. Je, ni lini walau Waziri atakuja kufanya ziara katika jimbo hili kuja kuona athari hiyo ambayo imetokea?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Khalifa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba eneo la Mtambwe lina madhara ambayo ameyaeleza Mbunge; na kwa kuwa niko hapa kwa niaba ya Waziri anayehusika na dhamana hii nitafikisha ujumbe ili aweze kutembelea hayo maeneo na kuangalia kiasi cha athari, lakini nilikuwa nataka kutoa wito kwa Watanzania, unajua kwa sasa hivi kila siku tunaona jinsi mabadiliko ya tabianchi yanavyoleta athari kwa maeneo yetu, ardhi yetu na kwenye vyanzo vingine vya mito na kadhalika, kwa hiyo, natoa wito maeneo yote haya Waheshimiwa Wabunge tukashikamane huko nchi nzima hii hata tukigawana mti mmoja mmoja tukaupanda, maana yake kwa mara moja tutakuwa tumepanda karibu miti milioni 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kabisa tukakabili mazingira mbalimbali ambayo yanaharibiwa. Mengine yanaharibiwa kutokana na matumizi yetu, kwa mfano mti kama mkoko. Mkoko hauharibiki kwa namna nyingine yoyote bila kutengenezewa athari za kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tukapige kelele kuhusu utunzaji wa mazingira. Mnamwona Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muunago wa Tanzania anavyopambania jinsi ya ku-*protect* maeneo yetu yasiendelee kuharibika na mnamwona Makamu wa Rais, ambaye ndiye hasa amepewa dhamana ya kusimamia Mazingira, jinsi

anavyohangaika katika kulinda mazingira yasiharibiwe. Tuungane naye, tuungane na Serikali yetu chini ya Mama Samia kwa ajili ya kulinda na kuboresha mazingira yetu yasiharibiwe kwa namna yoyote kutokana na shughuli zozote ambazo sisi kama binadamu tunazifanya kwenye maeneo yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Serikali kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunahamia Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu, sasa aulize swali lake.

Na. 74

**Kukatika Umeme – Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme Wilaya ya Meatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Meatu inapata umeme kutokea Kituo cha Kupoza Umeme cha Ibadakuli kilichopo Mkoani Shinyanga umbali wa kilomita 135. Kukatika kwa umeme Wilayani Meatu kunatokana na umbali mrefu wa njia ya kusafirisha umeme pamoja na uchakavu wa miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na tatizo hilo ikiwa ni pamoja na kufungwa vidhibiti umeme katika njia ya awali, kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka Mkalama Mkoani Singida hadi Bukundi Wilayani Meatu na kuendelea na zoezi la kubadilisha nguzo zilizochakaa kwa kuweka nguzo za zege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imeanza kutekeleza ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme katika eneo la Imalilo, Wilaya ya Bariadi Mkoani Simiyu ambapo itajengwa *line* ya umeme kutokea kwenye kituo hicho hadi Meatu. Jitihada hizi zimepunguza changamoto ya kukatika umeme kwa kiasi kikubwa sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leah Komanya.

**MHE. LEAH JEREMIAH KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa jitihada za makusudi za kunusuru kukatika kwa umeme Wilayani Meatu zinazochukuliwa na Serikali ikiwemo kutoa umeme Mkalama Mkoani Singida hadi Bukundi na hatimaye Makao Makuu ya Mji wa Mwanhuzi. Nina swali moja tu Mheshimiwa Waziri. Naomba kuuliza, je, Serikali haioni haja ya kumwezesha mkandarasi anayejenga *line* ya kutoka Ibadakuli kwenda Imalilo Bariadi kwa kumlipa deni lake la shilingi bilioni saba ili kumjengea uwezo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Azma ya Serikali ni kuhakikisha tunaendelea kuboresha upatikanaji wa umeme kwa wananchi, hususan wananchi wa Meatu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutayafanyia kazi madai ya mkandarasi ili kuhakikisha anafanya kazi hii kwa haraka na kwa ufanisi mkubwa kwa manufaa ya watu wa Meatu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Robert Maboto Chacha.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, je, ni lini Serikali itakamilisha suala la usambazaji wa umeme katika mitaa ya Halmashauri ya Mji wa Bunda?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na namshukuru Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia hii mitaa kwa muda mrefu. Tayari tuna mradi pale

kupitia Wakala wa Nishati Vijijini wa Vitongoji 15 lakini kwa mitaa ambayo inabakia tutaendelea kufuatilia na kutafuta fedha kuhakikisha umeme unawekwa katika mitaa ambayo bado haijafikiwa na umeme, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Kukatika katika kwa umeme Wilayani Liwale imekuwa ni adha kubwa sana. Ukiwauliza wataalamu wanasema sababu kubwa ni umbali uliopo kutoka Mahumbika mpaka Liwale ambako kuna kituo cha kupozea umeme. Je, Serikali haioni umefika wakati sasa wa kujenga kituo cha kupozea umeme Wilayani Liwale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mbunge. Umuhimu wa kuweka kituo cha kupoza umeme Liwale upo, kwa sababu utaboresha upatikanaji wa umeme kwa wananchi wa Liwale. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa sasa tunatekeleza mradi mkubwa wa kupeleka umeme wa gridi kwenye Mikoa ya Mtwara na Lindi kutokea Ruvuma, Songea Tunduru, Masasi mpaka Mahumbika. Tukikamilisha mradi huu mkubwa, tutaona uwezekano wa kuweka vituo vya kupoza umeme, ili pamoja na umeme wa gridi ambao ni wa uhakika zaidi, basi kwenye eneo la Liwale pia kuwe kuna kituo cha kupoza umeme. Kuhakikisha kwamba tunapunguza adha ya kukatika katika kwa umeme, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tulipata wakandarasi kwenye majimbo yetu na hasa pale Tarime Vijijini na vitongoji zaidi ya 300 havina umeme. Walienda wakapima kupitia Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wakaweka *beacon*. Sasa ni lini mradi huu wa umeme utaanza kutekelezwa katika jimbo la Tarime Vijijini ili watu wangu watoke kwenye giza nene? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mbunge. Tayari tumeanza utekelezaji wa kupeleka umeme kwenye vitongoji. Tumeanza na vitongoji 15 ambavyo yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge alituonyesha kwa *list* yake na kuanzia mwezi Desemba mwaka huu tuna mradi mwingine wa vitongoji 4,000. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, katika mradi unaofuata tutaendelea kupunguza vitongoji katika jimbo lake ili kuhakikisha vitongoji hivyo ambavyo havina umeme vinapelekewa umeme na wananchi wananufaika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tuna mradi mkubwa huu wa umeme ambao Mheshimiwa Naibu Waziri ameusema hapa hivi punde wa kutoka Songea – Namtumbo - Tunduru kwenda Masasi. Mradi huu mkandarasi hayupo *site* sasa hivi. Pia, wananchi hawajalipwa fidia yao. Je, ni lini wananchi watalipwa fidia yao na kwa nini mkandarasi hayupo *site* sasa hivi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza, mradi huu unaendelea. Mkandarasi hayuko *site* kwa sababu kulikuwa kuna changamoto za malipo, lakini siyo kwamba mradi umesimama. Mradi unaendelea na tayari kazi imeanza. Tutaendelea kufuatlia kuhakikisha mkandarasi analipwa kwa sababu fedha ya *advance* ya mwanzo alishapatiwa, lakini ana madai mengine. Tutaendelea kuhakikisha kwamba analipwa ili aendelee na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Songea - Tunduru, Tunduru – Masasi na Masasi – Mahumbika inaendelea. Nif changamoto za fedha ambazo kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Fedha tutahakikisha mkandarasi analipwa ili kumwongezea uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili kuhusu fidia, hivi karibuni Mheshimiwa Rais alienda ziara Mkoa wa Ruvuma na aliwaahidi wananchi wa Tunduru kwamba watalipwa fidia yao. Nataka niwahakikishie, Seirikali ya Awamu ya Sita itahakikisha wanalipwa fidia waendelee kutupa ushirikiano wanaotupa kwa kupisha maeneo yao ili miradi iweze kuendelea. Niwahakikishie ahadi ya Mheshimiwa Rais iko pale pale, watalipwa fidia yao na tunawashukuru sana kwa kupisha hayo maeneo ili miradi iendelee, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako na majibu ya Serikali kwa Waheshimiwa Wabunge. Tunahamia Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, sasa aulize swali lake. Kwa niaba...

Na. 75

**Mpango wa Kulipa Wazabuni**

**MHE. ASIA A. HALAMGA K.n.y. MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza:-

Je, nini mpango wa kuwalipa Wazabuni wanaotoa huduma mbalimbali hususani chakula kwenye Shule za Serikali wanaodai kwa muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utaratibu wa ulipaji wa madeni mbalimbali ikiwemo madeni ya wazabuni wa chakula waliotoa huduma katika shule mbalimbali. Ulipaji huzingatia upatikanaji wa mapato na uhakiki wa madeni unaofanywa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali kufanya uhakiki ni kutekeleza azma ya usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma kulingana na sheria ya Bajeti Sura Namba 439 na Sheria ya Fedha za Umma Sura Namba 348.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha inazielekeza halmashauri zote nchini kulipia huduma mbalimbali wanazopokea kutoka kwa watoa huduma kwa wakati ili kuepuka ulimbikizaji wa madeni na kuondoa usumbufu usio wa lazima kwa watoa huduma, ahsante.

**MWENYEKITI:** Maswali ya nyongeza yataulizwa na Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. ASIA A. HALANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Priscus Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini. Nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali katika kipindi cha bajeti Mheshimiwa Waziri alitueleza kwamba zimetolewa zaidi ya shilingi bilioni 949 kwa ajili ya ulipaji wa madeni mbalimbali. Tunataka kufahamu katika ulipaji huo wa zile fedha shilingi milioni 949 watoa huduma shuleni na wao wako kwenye huo mpango?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, je, mnatumia muda gani ili wananchi hawa waweze kujua watakaa muda gani na madeni hayo kwa sababu watoa huduma shuleni wengi ni wajasiriamali wadogo wadogo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Asia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza, bila shaka wazabuni ambao wanatoa huduma shuleni ni sehemu ya fedha ile ambayo ililipwa mwaka uliopita na wanaendelea kulipwa ndani ya mwaka huu na mwaka unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kwamba ni lini, inategemea upatinaji wa mapato na kukamilika kwa uhakiki. Basi nimwomba Mheshimiwa na Wazabuni wote nchini wawe na Subira, muda ukifika, fedha zao watalipwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Miongoni mwa wanaoidai Serikali kwa muda mrefu ni pamoja na wakandarasi wanaotengeneza barabara hapa nchini, na wako wengi wana madai ya muda mrefu. Ikumbukwe watu hawa wanapochukua hizi kazi wengine wanaenda kukopa benki. Wakati wanapotakiwa kufanya marejesho, Serikali haijawalipa. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na hawa wakandarasi wanaodai, na wapo wengine wanafilisiwa na benki husika kwa sababu walienda kukopa? Nini kauli ya uhakika ya Serikali kuwapa matumaini watu hawa na ikiwezekana walipwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali ni kwamba madeni yote yanaendelea kuhakikiwa na Serikali. Uhakiki utakapokamilika na upatikanaji wa mapato, wazabuni wote pamoja na wakandarasi watalipwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu la nyongeza limeulizwa na Mheshimiwa Cecilia. Kwa hiyo, basi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri, alipojibu alisema wanafanyia uhakiki ndipo walipwe, lakini wapo watu au wakandarasi wengine wana miaka mitatu hawajalipwa. Je, huo uhakiki unachukua muda gani ili hawa watu wapate fedha zao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amechukua eneo moja tu. Nilisema kulingana na upatikanaji wa mapato na uhakiki wa madeni. Kwa hiyo, mapato ya fedha yakipatikana watalipwa. Dawa ya deni ni kulipa. Nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge fedha ikipatikana wakandarasi wote watalipwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Changamoto ya madeni ya wazabuni wa chakula shuleni inasababisha kuathiri moja kwa moja upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi na ubora wa chakula hicho hivyo kuathiri elimu kwa maana ya uwezo wa watoto kusoma. Sasa, ningependa kufahamu, Mei mwaka huu nilichangia hapa Bungeni kwenye Wizara ya Elimu kuhusu suala hili na Agosti; Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Zainab Katimba, alisema kwamba TAMISEMI imewasilisha Wizara ya Fedha madeni ya wazabuni wa chakula takribani shilingi bilioni 21.7. Sasa, je, uhakiki huo utakwisha lini? Kwa sababu nikitoa mfano kwenye Jimbo la Bukoba Mjini kuna shule sita za sekondari za Serikali ambazo zinaidai Serikali jumla ya shilingi milioni 935, na madeni hayo ni kati ya mwaka mpaka miaka sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Naibu Waziri atupe majibu ya kueleweka na ya uhakika, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba baadhi ya wazabuni malipo yao hayajakamilika na hayajawafikia, lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyoendelea kusema, kadri mapato yatakavyoendelea kupatikana ndivyo wazabuni wetu watakavyolipwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata. Swali la Mheshimiwa Salum Mohammed Shaafi, Mbunge wa Chonga, sasa aulize swali lake.

Na. 76

**Akaunti ya Fedha ya Pamoja**

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI** aliuliza: -

Je, akaunti ya fedha ya pamoja ya Muungano imeshafunguliwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mbili zinaendelea na mashauriano juu ya mapendekezo yaliyowasilishwa na Tume ya pamoja ya fedha kuhusu utaratibu wa kudumu wa kuchangia matumizi na kugawana mapato ya Muungano. Uamuzi wa pamoja utakapofikiwa na pande zote mbili za Muungano ndiyo utakaowezesha kufunguliwa kwa akaunti ya fedha ya pamoja, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shaafi.

**MHE. SALUM MOHAMMED SHAAFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kucheleweshwa huko kuundwa akaunti ya fedha ya pamoja ya Serikali, je, Serikali haioni kwamba haina nia njema ya ufunguaji wa akaunti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ufunguaji wa akaunti hii ya fedha ya pamoja ni takwa la kikatiba na siyo la kimashauriano. Nataka kufahamu, ni sababu zipi zilizosababisha mashauriano hayo kutokukamilika hadi leo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Al-imam* Shaafi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina nia njema kabisa na Mheshimiwa Mbunge mwenyewe ni shahidi kwamba ndani ya Jamhuri ya Muungano tulikuwa na changamoto 25, lakini 21 tayari zimeshapatiwa ufumbuzi, yaliyobaki ni machache na Serikali ipo katika mchakato wa kukamilisha na kupata ufumbuzi wa hizo nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la pili, kila kitu kinahitaji utaratibu, kufuata kanuni na mashauriano. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba akaunti hiyo haitecheleweshwa, awe na subira na itafunguliwa baada ya pande mbili kukamilika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya Serikali kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo la muhimu kidogo. Tumepokea taarifa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba atakuwa na majukumu nje ya Mkoa wa Dodoma na kipindi chote ambacho yeye au Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko, hawatakuwepo kwenye Bunge, nafasi hiyo na shughuli zote za Bunge upande wa Serikali zitasimamiwa na Mheshimiwa *Captain* Mstaafu George Huruma Mkuchika. *(Makofi)*

Ahsanteni, tunahamia Wizara ya Ujenzi, swali namba 78. Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, Mbunge wa Hanang, sasa aulize swali lake.

Na. 78

**Kupandishwa Hadhi Barabara ya Bashnet Hadi Zinga**

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA** aliuliza: -

Je, lini barabara ya Bashnet – Luqmanda – Bosedesh hadi Zinga itapandishwa hadhi kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, upandishwaji hadhi wa barabara unafanywa kwa kuzingatia taratibu na vigezo vilivyoainishwa katika Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 na Kanuni za Menejimenti ya Barabara za mwaka 2009. Hivyo, Mheshimiwa Mbunge anashauriwa kuwasilisha maombi ya kupandishwa hadhi barabara ya Bashnet – Luqmanda – Bosedesh hadi Zinga kupitia Bodi ya Barabara ya Mkoa. Wizara itapitia maombi hayo na endapo barabara hii itakidhi vigezo itapandishwa hadhi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Samweli Xaday Hhayuma.

**MHE. *ENG*. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza. Barabara ya Nangwa – Bisambala – Kondoa ilitengewa fedha kwa ajili ya kufanyiwa usanifu na upembuzi yakinifu. Je, kazi hiyo imefikia hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, barabara ya Haydom – Mogitu imeshafanyiwa usanifu wa kina na umekamilika. Ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Hhayuma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Nangwa – Bisambala – Kondoa, kwanza nakiri Mheshimiwa Hhayuma amekuwa akiifuatilia mara kwa mara akishirikiana na Waheshimiwa Wabunge wa Kondoa Mjini na Vijijini kwa sababu zinaunganisha wilaya hizi, nami nimeshawahi kutembelea

barabara hii. Namwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na subira, barabara hii hasa kipande cha kuunganisha Kondoa kuna mto mkubwa, lile daraja gharama yake inaweza ikazidi hata gharama ya kuijenga barabara yote. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge awe na Subira, Serikali tunafahamu, kadri fedha itakavyopatikana tutalipa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, Haydom – Mogitu; Mheshimiwa Hhayuma hili vile vile ninamhakikishia kadri tutakavyopata fedha barabara hii tunajua umuhimu wake tutaitenga kwenye bajeti ili iweze kujengwa. Hata hivyo, namhakikishia, kipindi ambacho Serikali inatafuta fedha tutajenga barabara hizi kwa kiwango cha changarawe ambacho kinapitika misimu yote ya mvua na kiangazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata. Swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 79

**Kuboresha Barabara ya Nangurukuru – Kilwa Masoko**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali kupanua na kuboresha barabara ya Nangurukuru hadi Kilwa Masoko?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANROADS*, tayari imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Nangurukuru – Kilwa Masoko yenye urefu wa kilometa 30. Kwa sasa, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ukarabati utakaohusisha upanuzi wa barabara hiyo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali yanayotupa matarajio sisi Wanakilwa. Hata hivyo, kutokana na ukweli kwamba Kilwa Masoko ndipo ambapo Serikali yetu pendwa inajenga bandari ya uvuvi na kwa maana hiyo, barabara hii ya Nangurukuru – Kilwa Masoko imekuwa ikielemewa sana na uzito wa mzigo wa magari yanayopeleka *material* bandarini, je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya haraka kupata hizi fedha ili barabara hii iweze kutengenezwa na kuboreshwa kama ambavyo tuliomba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, barabara ya Kiranjeranje – Nanjilinji hususan kipande cha Kiranjeranje – Makangaga tuliomba kujengewa kwa kiwango cha lami, lakini kwa hatua za awali angalau kujenga kwa kiwango cha changarawe ili magari yanayotoka Kiranjeranje kwenda Makangaga kufuata *material* ya *gypsum* yaweze kupita angalau kwa mazingira yaliyo mazuri. Je, Serikali imefikia hatua gani kuboresha barabara hii ya Kiranjeranje – Makangaga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya Serikali.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kassinge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara ya Kilwa Masoko kuelekea bandarini, kama alivyosema Serikali inaendelea na ujenzi wa bandari pale Kilwa Masoko na ili bandari iweze kuwa na tija. lazima barabara hii iweze kutengenezwa. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati Serikali inaenda kukamilisha bandari, sambamba na hilo Serikali imeweka kwenye kipaumbele barabara hii ili iweze kuboreshwa kwa kujengwa upya ili iweze kuendana na uwekezaji mkubwa ambao umewekwa pale. Ujenzi wa bandari utaenda sambamba na kujengwa kwa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa kadri tutakavyopata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili kuhusu Kiranjeranje – Nanjilinji, natumia nafasi hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mkoa wa Lindi ni moja ya mikoa ambayo ilipata madhara makubwa ya mvua za

El-Nino na Kimbunga Hidaya, lakini kwa kazi nzuri ambayo Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Lindi na ushirikiano ambao wamekuwa wakitupatia, na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tayari ameshatupatia shilingi bilioni 140 kwa ajili ya kwenda kurudisha miundombinu ya barabara ambayo iliharibiwa ndani ya Mkoa wa Lindi na barabara hii ikiwemo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uwezeshaji huo. Waheshimiwa Wabunge kutoka mkoa huu mnafahamu tayari nimeshakabidhi wakandarasi ndani ya Mkoa wa Lindi ili kazi iweze kuanza. Natumia nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Lindi kutembelea hii Barabara ya Kiranjeranje – Nanjilinji kuhakikisha inatengenezwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika misimu yote kama Mheshimiwa Mbunge alivyoomba, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Ni takribani mwaka mmoja sasa barabara ya Mbulu – Garbabi ya kilometa 25 imetelekezwa na mkandarasi. Je, ni lini mkandarasi atarudi katika kipande cha kilometa 25 katika Barabara ya Mbulu – Garbabi ili iweze kutekelezwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia kuhusu barabara hii ya Mbulu – Garbabi. Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia barabara hii, nampongeza kwa ufuatiliaji. Nawahakikishia wananchi wake kuwa mkandarasi huyu kuna malipo alikuwa anadai na tumeshapeleka fedha Hazina. Fedha itapatikana ili aweze kuendelea na kazi na kurudi *site*, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka *Old Shinyanga* – Bubiki ilianza kujengwa kwa

kiwango cha lami lakini imefika hapo katikati Busangwa ujenzi umesimama. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi huo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu hitaji la Mheshimiwa Mbunge na namhakikishia kadri fedha itakavyopatikana tutatekeleza ombi lake, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, lakini atakumbuka barabara ya Kibiti – Lindi – Mtwara – Masasi ilifungwa mwaka 2023, wakati wa mvua za *El-Nino*. Ni kweli Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo, lakini sasa hivi mvua zinakaribia na hakuna mkandarasi yeyote aliyeko *site* pamoja na Serikali kusaini mkataba na wakandarasi hawa. Tunataka kufahamu, kabla ya mvua hizi za *El-Nino,* lakini pia atuhakikishie wananchi wa Mtwara kwamba barabara hiyo haitafungwa mwaka huu. Ni lini, mkandarasi anayetakiwa kujenga barabara ya Kibiti – Lindi – Mtwara – Masasi atakuwepo *site*? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa ufupi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Cecil Mwambe amekuwa akifuatilia barabara hii na ningependa kujibu swali lake kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuko hatua za mwisho za kumpata mkandarasi kujenga barabara ya Mtwara – Masasi – Mingoyo, na ni mkakati wa Serikali kujenga upya barabara hii kwa sababu imeharibiwa sana na mvua. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tumejipanga na ninawatoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania, kama ambavyo tulifanya mwaka 2023, tulipata mvua kubwa za *El-Nino* na Kimbunga Hidaya lakini Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa

Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na mvua kubwa ambazo tulizipata tulihakikisha mawasiliano yanakuwepo. Hata msimu huu wa mvua ambao unakaribia kuanza tumejipanga. Kwa hiyo, nawaondoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania. Kupitia *TANROADS* ikishirikiana na *TARURA* tumejipanga ipasavyo kuhakikisha mawasiliano yanakuwepo muda wote, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe kwa kifupi.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya *Machine Tools* – Kiaria na barabara ya Kwa Sadala – Mula ni barabara za *TANROADS* lakini zimejengwa hazikuwekwa taa ilhali barabara ya Makoa Mferejini imejengwa na imewekwa taa, kwa hiyo inaleta tofauti kubwa. Je, ni lini sasa Serikali itaweka taa kwenye barabara hizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Saashisha, amekuwa akinifuata kuhusu hitaji hili. Naomba baada ya majibu haya nitakaa naye tuwasiliane na *Regional Manager* kule Kilimanjaro tuone namna ambavyo tutatekeleza jambo hili, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Neema Mgaya.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali imeshajenga kilometa 19.4 za barabara ya Njombe – Iyai yenye kilometa 74 ambayo inaunganisha Mkoa wa Njombe na Mbeya ndani ya Jimbo la Wanging'ombe kwa kiwango cha lami. Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa barabara hii kutokana na umuhimu na uzalishaji mkubwa unaofanywa na wananchi wa Jimbo la Wanging'ombe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mgaya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua umuhimu wa barabara hii na namhakikishia Mheshimiwa Neema Mgaya kwamba tutaipa kipaumbele barabara hii kadiri fedha zitakavyokuwa zinapatikana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika barabara inayokwenda Kigoma, Kata ya Vumilia kuna wananchi wa maeneo ya Mbaoni na Motomoto ambao wanaidai fidia Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi ili wabomoe nyumba zao wapishe nguzo za umeme ambazo zinapeleka umeme katika kituo kipya cha kupozea umeme kinachojengwa eneo la Uhuru. Je, ni lini Serikali italipa ili na sisi umeme ufikishwe katika kituo chetu kinachojengwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia huwa ni sehemu ya gharama ya mradi. Kwa hiyo, naependa kumhakikishia Mheshimiwa Margaret Sitta pamoja na wananchi wake kwamba waendelee kuwa na subira. Mradi husika utakapokuwa unatekelezwa, basi sehemu ya gharama hiyo ni suala la hizi fidia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la ngongeza. Barabara ya Haydom – Labay imesainiwa na Mheshimiwa Waziri alikuja. Tumesaini barabara ile na akatuahidi ujenzi utaanza. Je, ni lini pochi la Mama linafunguliwa ili fedha zianze kupelekwa kwa mkandarasi na amalize kazi ya kujenga barabara ile? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa waziri, kwa ufupi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Flatei kwa namna ambavyo anafuatilia barabara hii na tumeshakaa naye pamoja na Hazina. Mkandarasi anasubiri *advance payment*. Kwa hiyo, nakuhakikishia yeye pamoja na wananchi wake kuwa barabara hii itaanza kujengwa tutakavyopata tu *advance payment*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante kwa majibu ya Serikali kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Ushetu, sasa aulize swali lake.

Na. 80

**Upanuzi wa Uwanja wa Ndege – Kahama**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa upanuzi wa uwanja wa Ndege uliopo Wilaya ya Kahama ili uwe na hadhi ya kutua ndege kubwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kihenzile, Naibu Waziri wa Uchukuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo, Benki ya Uwekezaji ya Watu wa Ulaya imeendelea na ukarabati pamoja na upanuzi wa miundombinu yote katika Kiwanja cha Ndege Shinyanga ili kiwanja hicho kiweze kutumika wakati wa usiku na mchana. Utekelezaji umefikia 66.8%. Pia Serikali kwa kushirikiana na kampuni binafsi iliyokuwa ikichimba madini Mjini Kahama, imefanya maboresho katika Kiwanja cha Ndege cha Kahama kwa kujenga jengo jipya ya abiria na kuendelea kufanya maboresho ya miundombinu mingine ili kuendelea kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kwa kuzingatia mahitaji ya sasa, Serikali itakamilisha kwanza Mradi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga na endapo mahitaji ya mkoa yataongezeka, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Kiwanja cha Ndege cha Kahama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wilaya ya Kahama imekuwa ndiyo kitovu cha kibiashara kwa Mkoa wa Shinyanga, lakini pia na Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Nchi hizi za Maziwa Makuu. Kwa nini Serikali isitenge japo fedha kidogo ili kuukarabati uwanja huu ambao ni wa kiwango cha moramu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Manispaa ya Kahama imekuwa ikikusanya fedha nyingi zaidi ya shilingi bilioni 13 mpaka shilingi bilioni 15 kwa mwaka. Kwa nini Serikali isitoe kibali sasa kwa Manispaa hii ya Kahama angalau uwanja huu uwekwe kwa kiwango cha lami pamoja na miundombinu yetu ili kuondoa adha wanayoipata wasafirishaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Cherehani kwa ufuatiliaji wake wa karibu wa Uwanja wa Ndege wa Kahama lakini hata ule wa Shinyanga. Pili, napenda kumwarifu Mheshimiwa Cherehani pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla kwamba katika kipindi ambacho Serikali imewahi kutenga fedha nyingi kuliko wakati mwingine wowote, ni sasa. Hivi ninavyozungumza, takribani Shilingi trilioni moja zinajenga viwanja vya ndege karibu vyote kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, moja, tumepokea ushauri wake mzuri kwa ajili ya kuweka moramu ili uwanja huu uendelee kutumika zaidi na ikizingatiwa ni jengo la ubia ambalo limejengwa na wenzetu wa Madini. Pili, namwomba pia awe na subira kidogo, tutakapokamilisha Uwanja wa Ndege wa Shinyanga,

tutapima mahitaji makubwa yaliyopo kwenye Uwanja wa Ndege wa Kahama halafu tuone ni hatua ipi ambayo inahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, izingatiwe kwamba, tunapozungumza hapa hata maeneo mengine kwenye viwanja vya mikoa, kuna mahitaji makubwa ya fidia pamoja na viwanja hivyo vifanyiwe maboresho. Kwa hiyo, watupe muda kidogo, baada ya hapo tutaona cha kufanya kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, nampongeza kwa sababu amekuja na mawazo ya kimapinduzi. Anazungumza juu ya Halmashauri ya Kahama kwamba ni halmashauri kubwa ambayo inakusanya mabilioni ya pesa na anaomba kibali kwamba pengine waruhusiwe kufanya ukarabati. Kimsingi Serikali hii ya Awamu ya Sita inaunga mkono jitihada za halmashauri na Waheshimiwa Madiwani wa aina yake katika kuiunga mkono Serikali kusaidia maboresho mbalimbali ya viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu chini ya Mheshimiwa Waziri Mbarawa pamoja na Mamlaka yetu ya Viwanja vya Ndege haitakuwa kikwazo, bali itakuwa msaada katika kurahisisha azma yenu hiyo kutokana na umuhimu mkubwa ambao mmeuona endapo mtatenga fedha kwa ajili ya kufanya maboresho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara ni mkoa wenye historia katika nchi hii, kwani anatoka Muasisi wa Taifa letu Baba Julius Kambarage Nyerere. Tumeona mkiwa mnamuenzi kwa matembezi na kwa vitu mbalimbali. Sisi watu wa Mkoa wa Mara, moja ya kumuenzi Baba wa Taifa ni kuhakikisha mnakamilisha Uwanja wa Ndege wa Musoma kwa kiwango cha lami. Ni lini mtatenga fedha za kutosha kuhakikisha Uwanja wa Ndege wa Musoma unakamilika? Wabunge tumechoka kushukia Mwanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Ester Bulaya kwa swali lake ambalo

ameuliza kwa umakini mkubwa. Serikali hii ya Awamu ya Sita inatambua, inazingatia na inafahamu umuhimu wa Baba wa Taifa. Pia inatumbua umuhimu wa viwanja vya ndege nchi hii, ndiyo maana pamoja na viwanja vyote nilivyosema vinaendelea kujengwa na kukarabatiwa, Uwanja wa Ndege wa Musoma upo, umeshatengewa fedha na unajengwa. Hivi ninavyozungumza, upo 60%. Labda ninachoweza kumhakikishia, ni kuiagiza mamlaka inayosimamia iharakishe ujenzi huo ukamilike ili uweze kuanza kutumika.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 81

**Mtaala Unaofundishwa Kwenye Vyuo Maendeleo ya Jamii**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza: -

Je, Mtaala gani unaofundishwa kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Tanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Ufundi vinatumia mitaala iliyoandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na kuidhinishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(NACTVET)*. Aidha, mitaala inayotumika hivi sasa ni Mtaala wa Maendeleo ya Jamii *(Community Development)* na Uhandisi Ujenzi na Maendeleo ya Jamii *(Civil Engineering with Community Development)* kwa ngazi ya Astashahada hadi Stashahada, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Serikali ina mkakati gani kwa wanafunzi wanaohitimu Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili kuawaajiri kwenda kuleta tija kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nini tofauti kati ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilivyoanzishwa na Hayati Baba wa Taifa mwaka 1975 kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa wananchi kwa maana ya kutoa mafunzo kwa vijana na kwenda kuleta maendeleo kwa wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Taska kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na mikakati ya kufanya tathmini kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii ili kuhakikisha halmashauri zote nchini zinapata Maafisa Maendeleo wa kutosha. Kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024, jumla ya Maafisa Maendeleo ya Jamii 840 wameajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vinatoa elimu kwa ngazi ya Cheti na Diploma kwa ufaulu wa kitaalamu. Pia vinatumia Mitaala ya *NACTVET* na Vyuo vya Maendeleo ya wananchi vinatoa mafunzo ya ujuzi kwa wananchi ili kuweza kujiajiri wenyewe kama vile ususi, kilimo, useremala na ushonaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara itaendelea kusimamia vyuo hivi kuhakikisha wananchi wanapata ujuzi na kupata elimu ambayo itawasaidia kiuchumi na maendeleo katika jamii, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi…

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwa niaba ya Mheshimiwa Suma Fyandomo…

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Mbunge, naomba uketi tafadhali. Swali namba 82 la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, litaulizwa na Mheshimiwa Condester Sichalwe.

Na. 82

**Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba za Askari – Mbeya**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE K.n.y. MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga nyumba za Askari Polisi pamoja na kukarabati zilizopo mkoani Mbeya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sillo, Naibu Waziri Mambo ya Ndani.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mbeya una mahitaji ya nyumba za makazi ya kuishi Askari Polisi 1,045 na nyumba zilizopo ni 186 na ni chakavu. Tathmini kwa ajili ya kubaini uchakavu na kuzifanyia ukarabati nyumba hizo zilizopo imefanyika na kiasi cha fedha shilingi 3,523,078,000 kinahitajika. Aidha, kiasi cha fedha shilingi 51,760,000,000 zinahitajika kujengea nyumba za makazi ya Askari ili kukidhi mahitaji ya mkoa. Serikali itaanza kutenga fedha kiasi kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa majibu mazuri ya swali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, nyumba za Askari Polisi

zilizopo Mbeya Jiji pamoja na Wilaya ya Rungwe zimeonekana kuchakaa. Ni lini Serikali itaenda kukarabati nyumba hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini Jeshi la Polisi mtatujengea nyumba za Maaskari kwenye Jimbo la Momba? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Condester kama ifuatavyo. Ni kweli baadhi ya nyumba za Askari kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge katika Jiji la Mbeya, ni chakavu. Kama alivyosema, timu yetu ya wataalamu ishafanya tathmini tayari na kiasi cha fedha kama nilivyotaja kwenye jibu la msingi kimetengwa. Kwa hiyo, kwenye mwaka wa fedha 2025/2026 tutaanza ukarabati wa nyumba za Askari Polisi katika Jiji la Mbeya na maeneo hayo aliyotaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la pili, kama nilivyosema, Wizara ya Mambo ya Ndani inafanya tathmini ya upungufu wa nyumba za Askari katika wilaya zote hapa nchini ikiwepo na Jimbo la Momba. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Jimbo la Momba pia litawekwa kwenye Mpango ili kujenga nyumba za Askari Polisi kwenye Jimbo la Momba, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunahamia Wizara ya Maji, swali Na. 83, Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, sasa aulize swali lake.

Na. 83

### Ujenzi wa Miradi ya Maji Kata za Manonga

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatenga fedha za ujenzi wa miradi ya maji ya Ziwa Victoria katika Kata ya Igoweko, Uswayu na Tambalale – Manonga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kundo, Naibu Waziri Wizara ya Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Jimbo la Manonga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa maji kwa ajili ya wananchi wake, inaendelea kutekeleza miradi mikubwa miwili ya kutoa maji Ziwa Victoria ambayo ni Mradi wa Ziba-Nkinga wenye kuhudumia vijiji tisa na Mradi wa Nkinga - Simbo utakaohudumia vijiji vinane. Mipango ya Serikali ni kusambaza maji kupeleka katika Kata ya Igoweko, Tambalale na Uswayu mara baada ya kukamilika kwa miradi hiyo. Aidha, Serikali inaendelea na zoezi la uchimbaji wa visima na kujenga miundombinu rahisi ya kuchotea maji *(Point source)* kwa ajili ya Igoweko, Mpogolo na Igondela vilivyoko katika Kata ya Igoweko, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Seif Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi kuweza kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Kwanza natumia fursa hii kuishukuru Serikali kwa fedha nyingi ambazo wametupatia kwa miradi mikubwa ya maji ya Ziwa Victoria kwa maana tumeona wakandarasi. Tumepokea wakandarasi wawili ambao mmoja anafanya *extension* ya mradi ule pale Ziba-Nkinga lakini pia tumepata mkandarasi mwingine anautoa Ziba kwenda Simbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na wakandarasi hawa kuwa tayari wapo *site* wameshaingia kwa ajili ya kuanza kufanya hii kazi, na Mheshimiwa Waziri alikuja na ugeni wa Mheshimiwa Makamu wa Rais, sasa ni lini Mheshimiwa Waziri mwenyewe atapata nafasi ya kuja kuitembelea hii miradi kujionea kazi kubwa na nzuri ya kupeleka maji katika hayo maeneo ambayo inafanywa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, alipokuja alitupatia fedha kwa ajili ya kupeleka maji pale kwenye Kijiji cha Ntogo. Wakandarasi sasa hivi wameanza kuchimba mtaro kwa ajili ya kupeleka maji. Sasa, kwa sababu tulikuwa tunataka vijiji viwili; kimoja cha Ntogo pale Kaselya tumepata mkandarasi, na kwa kuwa tulikuwa tunataka tupeleke na Kijiji kile kingine cha pili cha Mwamloli, je, Mheshimiwa Waziri hawezi kutupatia shilingi milioni 300 kukamilisha hii kazi nzuri ambayo inafanywa na Chama Cha Mapinduzi ili twende vizuri kwenye mambo yetu yale mengine ya uchaguzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Mbunge. Utekelezaji wa miradi hii unatokana na kazi kubwa sana ambayo Mheshimiwa Mbunge ameifanya kwa ajili ya kuwasemea wananchi wake wa jimbo lake. Matokeo haya ni kwa sababu ya kazi kubwa sana ya ushirikiano wake mzuri sana na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali ni wajibu wetu kuhakikisha tunafuatilia utekelezaji wa miradi ili iweze kukamilika kwa wakati. Vilevile, kuhakikisha sehemu ambayo hatujafika, tunaona njia ya kuhakikisha tunafanya utafiti na tathmini ya namna gani tupeleke huduma ya maji kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alivyoomba. Sasa Mheshimiwa Mbunge kama alivyoomba shilingi milioni 300, naomba nilipokee ili tuweke katika Mpango wa Serikali wa utekelezaji katika bajeti ijayo ya mwaka wa fedha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Fatma Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Je, lini Serikali itaharakisha ujenzi wa Bwawa la Farkwa ili kuweza kukabiliana na tatizo la maji katika Jiji la Dodoma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Toufiq kama ifuatavyo. Ni kilio cha Wanadodoma, na ni kilio cha Waheshimiwa Wabunge wa Dodoma, na ni kilio cha Watanzania kwa sababu hapa ndipo Makao Makuu ya Nchi yetu. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari alipata fedha kwa ajili ya kufanya mapitio ya mradi huu wa Farkwa ambao unakamilika. Sasa tumeanza mchakato wa kumtafuta mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka Desemba itakapofika, tuna uhakika mkandarasi atakapopatikana, ataingia kazini kwa ajili ya kutekeleza mradi huu wa kuvuta maji kutoka Bwawa la Farkwa ili iwe *solution* ya kati kwa kutatua changamoto ya maji ambayo tumeendelea kukutana nayo katika Jiji lla Dodoma. Kama ambavyo nilisema, uzalishaji wetu wa maji hapa Dodoma ni lita 79,000,000 lakini mahitaji yake ni lita 149,000,000. Sasa visima pekee havitaweza kutupatia maji ya kutosha kulingana na mahitaji na ndiyo maana kunakuwa na hii changamoto ya mgao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hili Bwawa la Farkwa halitakuwa suluhisho la kudumu. Jambo ambalo liko katika Mpango wa Serikali ni kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria ili kuhakikisha kwamba sasa Jiji la Dodoma linaendelea kupendeza na wananchi wa Dodoma wapate maji ya uhakika na toshelevu kwa wakati wote, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu.

Tunahamia Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na 84

**Ujenzi wa Soko la Zao la Muhogo Kigoma**

**MHE: JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga soko la kuuzia Zao la Muhogo katika Mkoa wa Kigoma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo katika Mkoa wa Kigoma imetenga eneo la ekari 4.26 kwa ajili ya ujenzi wa soko la kuuzia zao la muhogo. Hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imepanga kujenga soko hilo katika mwaka wa fedha 2024/2025 baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kukamilika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, zao la muhogo ni zao la kibiashara katika Mkoa wa Kigoma, lakini zao hilo mwaka 2023 na mwaka 2022 lilikuwa na bei nzuri. Mwaka 2022 kilo moja ilikuwa ikiuzwa shilingi 800 mpaka shilingi 1,000 kwa kilo. Mwaka 2023 limeuzwa shilingi 600 mpaka shilingi 800 kwa kilo lakini mwaka huu limeanguka kabisa zao hilo, limepoteza soko, linauzwa kilo moja shilingi 200 mpaka shilingi 300. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia wakulima soko la uhakika ili waweze kuuza mazao yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, mpaka sasa hakuna dawa inayoweza kutibu wadudu wanaoharibu zao la muhogo. Je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta dawa ya uhakika inayoweza kutibu zao la mhogo wakati linapokuwa limewekwa kwenye *store*? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Genzabuke kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ni kweli Serikali inatambua umuhimu wa zao la mhogo, kwanza likiwa ni zao la chakula ambapo katika chakula kwa nchi yetu linachangia kwa zaidi ya 10.2%. Hivyo ni chanzo cha wanga *(starch)* na *industrial starch* na linatusaidia kuzalisha *spirit,* gundi, pamoja na vyakula vya wanyama. Serikali imeshaanza mkakati wa kuhakikisha kwamba, tunatafuta masoko ndani na nje ya nchi kupitia balozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi tumeshaanza kufanya tafiti ya zao hili kupitia taasisi yetu ya utafiti wa kilimo ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda ili kuweza kuhakikisha kwamba, zao hili la mhogo linachakatwa kwenye viwanda ili kuweza kuhakikisha kwamba wale wakulima wanaolima zao hili waweze kupata faida zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuangalia eneo hilo, ule umuhimu wake, Taasisi ya *TARI* imeshafanya utafiti wa mbegu bora pia kuhakikisha mbegu zinazokuwa na ustahimilivu ili kuweza kuwasaidia wakulima wetu walime kwa faida zaidi. Ukiangalia mwaka wa fedha 2020/2021, mavuno yalikuwa ni zaidi ya milioni 2.2 na katika mwaka uliofuata tulipanda kutoka milioni 2.2 mpaka milioni 2.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, hilo la kuhusiana na namna gani ambavyo inaweza ikahifadhiwa? Zao la Mhogo kidogo ni tofauti na mahindi ambayo yana gamba gumu nje. Zao la Mhogo linapomenywa tayari kinachobaki kule ni chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mpango wa Serikali moja ni kuanza kuhamasisha uwekezaji wa viwanda ili kuweza kuhakikisha uchakataji unafanyika. Pili, tunaenda kwenye teknolojia ya kisasa ya kuhakikisha tunakuwa na *dryers* ili ziwezi kuhifadhi zao hilo hasa *post-harvest* ili kusiwe na zile *effects* na kuweza kusababisha zao hilo likae muda mrefu. Pia, mkakati wa

kutafuta masoko ya haraka utasaidia sana kuweza kuhakikisha zao hilo haliharibiki, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daktari Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wana shida sana ya kupata vipando bora vya zao hilo la mihogo. Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia Chuo cha Tumbi Tabora, ili kiweze kutangaza na kusambaza mbegu bora ya mhogo inayozalishwa pale chuoni hasa kwenye mikoa inayolima mihogo ikiwemo Ruvuma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daktari Thea Ntara, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza, tayari Serikali ya Daktari Samia Suluhu Hassan imeshaweka umuhimu huo na imeshaanza mkakati wa kuhakikisha kwamba itajenga baadaye hiki kiwanda. Tumeshafanya usanifu na upembuzi kuweza kuhakikisha kwa mwaka wa fedha 2025/2026 tutaanza na ujenzi wa kiwanda kule Kigoma. Hatua ya pili, kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo tayari imeshaanza kufanya tafiti, kwanza, kutopata mbegu iliyo bora; pili, kuhakikisha kwamba zao hili linalozalishwa linakuwa na ustahimilivu; tatu, mbegu inayotolewa iwe bora inayoweza kukabiliana na wadudu; nne, kuhakikisha magonjwa hayawezi kuathiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hicho anachokisema Mheshimiwa Daktari Thea Ntara, tayari Serikali makini hii imeshaliona na inaendelea kutenga fedha katika mwaka wa bajeti 2025/2026, itakuwa katika hatua nzuri ya kuweza kukamilisha hilo walilolitamania, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Esther Edwin Malleko Mbunge wa Viti Maakum, aulize swali lake.

Na. 85

**Kuongeza Bajeti ya *TANAPA* na *TAWA***

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuwaongezea bajeti *TANAPA* na *TAWA* kwani majukumu yao ni makubwa ikilinganishwa na bajeti inayotengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Maliasili na Utalii Dunstan Kitandula majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya janga la ugonjwa wa UVIKO - 19 mwaka 2019, ambalo liliathiri shughuli za utalii kwa kiasi kikubwa, Taasisi za uhifadhi hususan *TANAPA* pamoja na *TAWA* zilishindwa kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kujiendesha hali ambayo iliifanya Serikali kuchukua hatua za makusudi za kunusuru taasisi hizo kwa kugharamia uendeshaji pamoja na kulipa mishahara ya watumishi. Kufuatia hatua hizo, hadi sasa Taasisi za Uhifadhi *(TANAPA, TAWA* na *NCAA)* zinapata fedha za uendeshaji kutoka Serikalini kwa utaratibu wa mgao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali iliziongezea taasisi za uhifadhi bajeti ya matumizi ya kawaida *(OC)*. Mathalan, bajeti ya *TANAPA* iliongezwa kutoka shilingi 106,958,705,429.41 mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia shilingi bilioni 118.3 ikiwa ni ongezeko la shilingi 11,348,567,370.59 sawa na ongezeko la 10.61%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile bajeti ya *TAWA* iliongezwa kutoka shilingi bilioni 45.6 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia shilingi bilioni 62.9 ikiwa na ongezeko la shilingi 17,284,226,400.00 sawa na ongezeko la 37.83%. Aidha, Serikali

itaendelea kuboresha bajeti ya taasisi hizo kutegemeana na hali ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali ili kuimarisha shughuli za ulinzi na kuboresha miundombinu ya utalii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naipongeza Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa sasa, sekta ya utalii imekua sana hasa baada ya Mheshimiwa Rais Kutangaza utalii wetu na kutengeneza Filamu ya *Royal Tour*, je, Serikali haioni umuhimu wa kurejesha utaratibu wa zamani ili fedha hizo ziende kusaidia kwenye miundombinu pamoja na huduma nyingine zinazotolewa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kazi kubwa imefanyika ya kutangaza sekta ya utalii. Hapa nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo amechukua jukumu hili yeye mwenyewe na kushiriki kwenye filamu ile ya *Royal Tour* ambayo imekuwa na matokeo mazuri sana kwa nchi yetu. Vilevile, ameshiriki kwenye filamu ya *Amazing Tanzania* ambayo kesho tunaenda kufanya uzinduzi wake kwa upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeona ukuaji wa kasi wa sekta hii na imekuwa ikifanya tathmini ya kina kuhusu mwenendo wa ukuaji wa sekta hii na mahitaji yake. Ndiyo maana nilipojibu swali la msingi nimeonesha kwenye ule upande wa *OC* jinsi ambavyo Serikali imeongeza fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka katika bajeti ya mwaka huu tuliidhinisha hapa, asilimia sita kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Sekta ya Utalii. Vilevile asilimia tatu kwenye eneo la sekta ya wanyamapori. Hizi ni fedha ambazo mwanzoni zilikuwa hazitolewi, lakini ni fedha ambazo sasa zinatoka ili kuimarisha sekta yetu kama nilivyosema kwenye upande wa *OC* na kwenye upande wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ongezeko kubwa la karibu dola bilioni tano kwa *TANAPA* dola karibu bilioni nne kwa ajili ya *TAWA*. Kwa hiyo, tathmini hii inayofanyika ya ukuaji wa sekta, ninaamini kabisa kwamba, tutaweza kukidhi mahitaji ya sekta hii na kuweza kuhakikisha kwamba, fedha zinatoka kwa kutosheleza ili tuweze kuiboresha sekta yetu ambayo kwa kiasi kikubwa inachangia sana kwenye pato la Taifa na ajira katika nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephat Kandege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba utalii unatuongezea fedha za kigeni kwa kiasi kikubwa sana. Pia, upatikanaji wa *OC* kila mtu anajua jinsi ambavyo inapatikana kwa kusuasua. Je, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba kunakuwepo na utaratibu wa kuwepo *retention* kwa ajili ya taasisi hizi ili yale matengenezo yanayotakiwa kufanywa kwa muda, yafanywe kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kama nilivyosema kwenye majibu ya awali, *retention* imeanza ndiyo maana nimesema tuna asilimia sita inayokwenda kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Utalii; pia, tunayo asilimia tatu ambayo inaenda kwenye *World Life Protection Fund.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi ambavyo tathmini zinafanyika kuhusiana na ukuaji wa sekta hii, tathmini hiyo itatuelekeza juu ya umuhimu wa kuwa na 100% *retention* au twende hatua kwa hatua ili tusiweze ku-*suffocate* maeneo mengine ambayo fedha hizi za utalii zinaweza kuchangia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru.

Tunahamia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 86

**Maabara ya Kupima Sampuli za Magonjwa ya Mifugo**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanzisha Maabara ya kupima Sampuli za Magonjwa ya Mifugo Mkoani Kagera?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Maabara ya Kupima Sampuli za Magonjwa ya Mifugo Mkoani Kagera lipo kwenye mpango wa muda mrefu wa Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania *(TVLA)* kama ilivyo pia katika Mikoa mingine. Aidha, utambuzi wa sampuli za magonjwa ya mifugo kwa Mkoa wa Kagera kwa sasa unafanyika kupitia maabara ya Kanda iliyopo Mkoani Mwanza ambayo ni miongoni mwa maabara 11 zilizopo nchini na zinamilikiwa na Serikali, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Conchesta.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Mkoa wa Kagera umewahi kuwa na maabara kubwa na nzuri chini ya Mradi wa *KALIDEP* na baadaye *KADADET*. Miradi hii ilipokufa na maabara hiyo ikafa. Ni kwa nini Serikali haikuendeleza maabara hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mkoa wa kagera licha ya ukubwa wake lakini kuna mifugo mingi na kuna ugumu katika kupeleka sampuli kwa sababu ya umbali pia ukosefu wa wataalam, wakati mwingine wa dharura hulazimika madkatari kutoka Mwanza kuja kuchukua sampuli kutoka Mkoa wa Kagera. Je, ni lini Serikali itakuwa na mpango wa kuhakikisha kwamba hii Wizara ya Mifugo inakuwa na wataalam wa kutosha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la kwanza ambalo Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kwa nini Serikali haikuendeleza hizi maabara? Ni kweli maabara hizi zilikuwepo katika maeneo mbalimbali ndani ya nchi yetu, hususan Mkoa wa kagera kulikuwa na maabara, na hii ni kwa sababu ya wingi wa mifugo iliyoko katika Mkoa wetu wa Kagera. Tunatambua na kuwapongeza sana wananchi wa Mkoa wa Kagera kuwa wafugaji wazuri na maabara ilikuwepo na kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba, Serikali inayo mkakati wa kufufua maabara zote zilizokuwa zimekufa katika maeneo yetu mbalimbali ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, kwa sababu maabara hizo zimekufa, wananchi na wafugaji wanashauriwa kupeleka sampuli zao katika Mkoa wa Mwanza ambako ndiyo kuna maabara kubwa katika kanda ya ziwa. Maabara hiyo imekuwa ikifanya vizuri na ina wataalam wa kutosha na kwa bahati nzuri sana wataalam wetu wako tayari kusafiri kuwafuata wafugaji kokote wanakopatikana, lakini hii haiondoi mpango wa Serikali wa kufufua maabara zetu zilizokuwepo katika mikoa yetu ikiwemo pamoja na Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mpango wa kuwa na wataalam wengi ni mpango madhubuti wa Serikali chini ya Mheshimiwa Rais, na ameshatoa maelekezo tuendelee kutengeneza wataalam wa mifugo ambao watatusaidia kutoa elimu kwa wafugaji wetu katika maeneo mbalimbali ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali kupitia vyuo mbalimbali ambavyo viko ndani ya nchi yetu ikiwemo Chuo Kikuu cha Sokoine na vyuo vingine vidogo vidogo ambavyo vinatoa kwa *level* ya *certificate, diploma* na *advance diploma* tunaendelea kutengeneza wataalam wa mifugo ambao watasaidia kutoa elimu kwa wafugaji wetu ili mfugaji anapofanya shughuli za

ufugaji aweze kupata tija katika shughuli hiyo aliyoifanya, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 87

**Mikopo ya Boti za Uvuvi**

**MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza:-

Je, wavuvi wameshirikishwaje katika mpango wa Serikali wa ununuzi wa Boti za uvuvi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mradi huu, wavuvi walishirikishwa katika hatua mbalimbali ikiwemo kubainisha mahitaji, kufahamishwa kuomba mkopo wa boti pamoja na kuhamasishwa na kupewa elimu kuhusu fursa zilizopo kwenye mradi, ambapo, timu ya wataalam kutoka Wizarani walitekeleza jukumu la kuwatembelea wavuvi katika maeneo yao hapa nchini ili kupata maoni na mapendekezo yao kuhusu ukubwa wa boti na vifaa vyake pamoja na kutoa matangazo kwa njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari. Aidha, kupitia mchakato huo, jumla ya boti 160 zenye thamani ya shilingi bilioni 11.5 zimetolewa kwa wanufaika 3,163 ikijumuisha wanawake 1,008 na wanaume 2,155 katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Nyoka.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wavuvi vifaa vya kuchunguza samaki mahali

walipo badala ya kuvua kwa kubahatisha ikiwa ni pamoja na kuwapatia vifaa vya uokoaji kama *life jacket* na vifaa vingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, lini Serikali itawezesha wavuvi wa Ziwa Nyasa, boti za *fiber* za *horsepower* 9.9 na *horsepower* 15 ili ziweze kukidhi uwezo wa wavuvi wa ziwa hilo?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la kuwawezesha vifaa vya uvuvi, Wavuvi wa Ziwa Nyasa. Kwanza, tulipoanza hili zoezi ambalo Mheshimiwa Rais alituruhusu kugawa boti na vifaa vya uvuvi katika maeneo mbalimbali, tulituma wataalam katika Ziwa Nyasa na walizunguka maeneo yote kwa kukutana na wavuvi na kuainisha mahitaji ya wavuvi ni nini? Baadaye wavuvi walikubali, waliainisha kwamba wanahitaji boti na vifaa vya kuvulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshatoa boti kwenye vikundi mbalimbali katika Ziwa Nyasa. Pia boti hizi zinaambatana na vifaa vyake ikiwa ni pamoja na nyavu, *life jacket* na vifaa vingine vya kuvulia. Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua ni lini Serikali itatoa vifaa vya kuchunguza kujua samaki wako wapi badala ya kwenda kuvua kwa kutumia miujiza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie kwamba, katika boti hizo tunazozitoa zinakuwa na *fish finder* ambayo inamwelekeza mvuvi wetu kwamba, samaki wako kilometa 10; ukifika kilomita 10 kata kushoto, ukifika kilomita nane kata kulia, kilomita 100, hapo ndiyo kuna mzigo. Kwa hiyo, sasa hivi wavuvi wetu hawaendi kienyeji kama ilivyokuwa zamani. Tuna *fish finder* ambazo zimekuwa zikitolewa katika boti hizo na kwa kweli kumekuwa na matokeo chanya katika uvuvi wa samaki katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ziwa Nyasa, kama nilivyosema katika jibu la msingi, tumeshatoa boti na hizi boti tumekuwa tukizitoa kwa mahitaji yao wenyewe wale wavuvi ambao wamekuwa wakihitaji, kwa sababu boti hizi wakati

mwingine zinaonesha urefu wa boti inategemea na *horsepower* gani, ina injini ya ukubwa kiasi gani? Kwa mfano, boti ikiwa na urefu wa mita 12 huwezi kuiwekea *horsepower two,* lazima uweke *horsepower* kubwa ambayo inaweza ikasukuma ile boti. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba, bado tuna uhitaji mkubwa katika Ziwa Nyasa na tuko tayari kuendelea kutoa boti hizi kwa sababu Mheshimiwa Rais amewezesha boti nyingi sana hasa kwenye mwaka huu, tutaendelea kutoa boti nyingi katika Ziwa Nyasa kuhakikisha kwamba wavuvi wetu wanakuwa na unafuu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge nawashukuru tumemaliza kipindi chetu cha maswali na majibu. Naomba nitangaze wageni ambao tunao asubuhi hii.

Kwanza, wageni waliokaa Jukwaa la Spika, tunao wageni tisa ambao ni Wajumbe wa Tume ya Utumishi kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakiongozwa na Ndugu Rashid Makame Shamsi ambaye ni Mwenyekiti. Pia wapo Wajumbe ni Ndugu Afadhali Taib Afadhali, Ndugu Habib Ali Haji, Ndugu Khadija Ahmed Omary, Ndugu Hamida Abdalla Issa, Ndugu Mahmoud Ahmada Haji, Ndugu Ramadhan Khamis Juma, Ndugu Mboja Ali Sheha na Ndugu Salama Juma Suleiman, karibuni sana. *(Makofi)*

Pili, tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge na Naibu Spika ambao ni vijana kutoka Kikundi cha *Wako Jacko Used Spare Parts*, wanaojihusisha na uuzaji wa vipuri vya magari kutoka Ilala Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, Mbunge na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambao ni Umoja wa Wanawake Katoliki Tanzania (WAWATA) kutoka Mikoa mbalimbali nchini wakiongozwa na Ndugu Eveline Mtenga, Mwenyekiti Taifa na Rais wa Wanawake Wakatoliki Afrika, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, Mbunge na Naibu Waziri wa Afya ambao ni Chama cha

Watalamu wa Mionzi Tanzania *(TARA)* wakiongozwa na Ndugu Bakari Msongamwanja ambaye ni Rais wa Chama hicho, karibuni sana kama wapo tumewaona, ahsanteni. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wengine wanne wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Godwin Mollel ambao wanatoka Kampuni ya *QFK Motors* wakiongozwa na Ndugu Kassim Hamza Mafua ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 27 wa Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya, Mbunge ambao ni wanafunzi wenzake waliosoma wote kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne katika Shule ya Sekondari Ikizu, Mkoa wa Mara, karibuni sana sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge, ambao ni marafiki zake wa Joma Ubunifu ambao ni washonaji suti kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Jacqueline Andrea Kainja, Mbunge ambao ni Mchungaji aliyeambatana na mke wake kutoka Kaliua, Mkoa wa Tabora, karibu sana sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge ambao ni Kikundi cha Sanaa cha Isongole Sekondari kutoka Wilaya ya Rungwe, Mkoa wa Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, Mbunge ambao ni Walimu Wakuu kutoka Tarime Mjini, Mkoa wa Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, Mbunge ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jimbo la Kilolo, Mkoa wa Iringa, karibu sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Tutaanza na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, atafutiwa na Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa heshima hii ya kutoa mchango wangu. Katika mchango wangu nitazungumzia hoja nne kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Mwaka 1966 Waziri Mkuu wa Zamani wa Singapore Lee Kuan Yew alitembelea Ghana na alipokutana na mwenyeji wake alitambulishwa kwa msomi wa Shahada ya Uzamivu katika somo la fasihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lilimsikitisha sana, lakini hakusema neno mbele ya mwenyeji wake. Aliporudi Singapore alifanya Mkutano na Waandishi wa Habari akasema maneno haya, kama angepata nafasi za kuzishauri nchi za kiafrika, basi angeshauri nchi za kiafrika ziwekeze kikamilifu katika Sekta ya Kilimo, kwa sababu kilimo ndiyo sekta yenye uwezo wa kuondoa umasikini katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno hayo hayo Mwalimu Nyerere Baba wa Taifa aliyarudia tena mwaka 1985 wakati akihutubia Mkutano wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi, alisema maneno hayo hayo kama Tanzania inataka kujenga Taifa linalojitegemea, basi tuwekeze katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya kwanza kilimo kitaendelea kuwa na mchango mkubwa sana katika maendeleo ya Taifa hili kwa miaka mingi ijayo na Sekta hii ina ajiri zaidi ya 70% ya Watanzania. Kwa hiyo, kama tunataka tupunguze umaskini miongoni mwa Watanzania, basi tuwekeze katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nieleze tu namna Wizara ya Kilimo inavyotekeleza Miradi yake ya Kilimo ya Maendeleo. Wizara hii inatekeleza Miradi miwili ya kilimo, Mradi wa Jenga Kesho Iliyo Bora na Ujenzi wa Mabwawa 18 ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji. Nimezitafuta takwimu ili nione kwa jinsi gani Mradi wa Jenga Kesho Iliyo Bora unavyoweza kutusaidia katika kukuza kilimo, kwa bahati mbaya mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti taarifa hizo sikuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ujenzi wa Mabwawa 18 mpaka sasa katika kipindi cha miaka mitatu Wizara imetekeleza mabwawa matatu yamekamilika na mengine 15 yako katika hatua mbalimbali za ujenzi. Kwa kutumia busara ya kawaida, Wizara ilitakiwa ijenge mabwawa manne kila mwaka badala ya kujenga mabwawa yote kwa wakati mmoja kama wanavyofanya. Kama wangefanya hivyo, leo ninavyozungumza wangekuwa wamejenga mabwawa 12 na mabwawa sita yaliyobaki yangemalizwa mwaka kesho, kwa bahati mbaya hawakufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili licha ya Wizara hii kupatiwa wastani wa shilingi trilioni moja kila mwaka kwa ajili ya Maendeleo ya Kilimo, tija katika Uzalishaji wa mazao ya kilimo bado uko chini sana, nitatoa takwimu kuonyesha wenzetu nchi jirani wanavyofanya vizuri kwenye Sekta hii kuliko sisi. Nchi moja ya jirani ina eneo la kumwagilia maji lenye hekta 650,000 wanauza mazao ya kilimo nje ya nchi yenye thamani ya dola bilioni 3.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Tanzania tuna eneo la kumwagilia maji lenye ukubwa wa hekta 827,000, tunauza nje mazao yenye thamani ya dola bilioni 2.3, utaona kwa jinsi gani tulivyokua tuko nyuma. Nilitegemea fedha hizi za bajeti zingetumika katika kuwapa wakulima mbegu zilizobora, huduma bora za ugani, utafiti wenye matokeo sahihi kwa wakulima lakini nalo hili naona halikufanyika kwa usahihi. *(MakofI)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya tatu ni kwamba, njia muafaka ya kuongeza tija katika uzalishaji iwe katika Sekta ya Kilimo au Sekta ya Viwanda ni kuwekeza kwenye elimu bora inayosisitiza juu ya ufundi, ujuzi na ugunduzi. Kwa bahati mbaya elimu yetu bado haikidhi kiwango hicho cha ubora na mara nyingi tunafundisha masomo ya jumla jumla badala ya masomo yanayosisitiza ujuzi, weledi na umahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatumia wastani wa shilingi bilioni 500 kila mwaka kwa ajili ya Mikopo ya Elimu ya Juu, lakini kama nilivyosema, fedha hizo mchango wake ni mdogo sana katika kukuza uchumi na sababu yake ni hiyo niliyoeleza hapo juu. Tatizo letu ni nini? Tatizo letu tunafundisha masomo ya jumla jumla ambayo hayana uhusiano wa moja kwa moja katika kupunguza umasikini. Ningetarajia tungefundisha masomo kama usimamizi wa mipango, usimamizi wa maendeleo, usimamizi wa rasilimali watu, usimamizi wa viwanda, usimamizi wa sekta ya afya, na mambo ambayo yana uhusiano moja kwa moja na kupunguza umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningetarajia tungefundisha masomo ya ukalimani, ufundishaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni ili tusafirishe watalamu nchi za ughaibuni. Kwa upande wa teknolojia ningetarajia tungewafundisha vijana masuala ya sayansi ya data *(data analytic)* akili bandia *(artificial intelligence), cyber* na *blockchain. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya nne ni kwamba, baadhi ya matumizi ya Serikali kwa maoni yangu, badala ya kusaidia kuongeza tija, yanaibebesha Serikali mzigo mkubwa sana. Nitatoa mfano. Mfano wa kwanza, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Maliasili, na Wizara ya Maji wananunua

mitambo inayofanana na wote wanafanya kazi ya kuchimba mabwawa pamoja na kutengeneza barabara. Baada ya muda mfupi tu vifaa vinaanza kutelekezwa porini kwa sababu gharama za mafuta zimeongezeka sana na gharama za matengenezo zimekua kubwa sana. Badala vifaa hivyo kuwekwa katika sehemu moja na kila anayehitaji akakodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya tano, Chuo Kikuu cha Dodoma kina shule nzima ya teknolojia ya habari. Wakati huo huo Wizara ya Habari na Teknolojia ya Habari inajenga Chuo cha Umahiri wa TEHAMA. Kwangu mimi haya ni matumizi mabaya sana ya fedha. Tatizo letu kama Taifa siyo majengo, tatizo letu ni walimu walio bora, vifaa vilivyo bora, na mazingira bora. Sasa fedha ambazo zinatumika kujenga Chuo kipya zingepelekwa Dodoma ili kutengeneza Chuo cha Umahiri katika hii Jumuiya ya Afrika Mashariki ili vijana wetu wapate mafunzo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya sita, mfumo wetu wa Vyuo Vikuu ni utaratibu wa kwamba Chuo Kikuu kimoja kinafundisha kila somo na kwa maana hiyo hatusisitizi umahiri na weledi. Kwa maoni yangu, haya ni matumizi mabaya sana ya rasilimali katika Taifa. Ingekuwa vizuri kama Taifa tugawe Vyuo Vikuu kulingana na uchaguzi wa weledi na ubobezi wa masomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nashauri Chuo Kikuu cha Dodoma kingefundisha masuala ya sayansi, teknolojia na uvumbuzi; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kikafundisha masomo ya sayansi ya jamii, Muhimbili kikaendelea kama kilivyo na *SUA* kikaendelea kama kilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine ni kwamba, Wizara ya Elimu ina dhamira ya kufundisha masomo ya ufundi na amali katika shule zote za sekondari sambamba na kuwa na Vyuo vya *Technical* Tanzania nzima, nia ni nzuri, dhamira ni nzuri lakini uwezo haupo wa kutekeleza jambo hilo kubwa. Kwa maoni yangu, badala ya shule zote za sekondari kufundisha masomo haya, ningependekeza tukawekeza kwenye Ujenzi wa Vyuo vya Kisasa vya Ufundi katika kila Kanda. Kwa mfano, Kanda ya Kusini, Kaskazini, Mashariki, Magharibi, Kanda ya Kati, Kusini Juu pamoja

na Kanda ya Ziwa na Vyuo hivi vipewe walimu walio mahairi katika ufundishaji na vifaa vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo langu lingine, masomo yatakayofundishwa katika Vyuo hivyo, yawe ni masomo yanayoendana na shughuli kuu za uchumi wa Tanzania kama kilimo, ufugaji, madini, gesi asilia, ujenzi wa miundombinu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kwamba, nchi yetu kama nilivyosema awali ni nchi ya kilimo. Sasa nchi ambayo inategemea sana Sekta ya Kilimo kuleta maendeleo, ingefanya uamuzi wa kimapinduzi wa kuzalisha mbolea yake ya ndani badala ya kuagiza nje. Bahati nzuri tunayo gesi asilia, tunayo samadi, tungechanganya pamoja samadi na gesi asilia tungeweza kutengeneza mbolea badala ya kutumia zaidi ya shilingi bilioni 300 kuagiza mbolea kutoka nje. Jambo hili halifurahishi hata kidogo na wala siyo heshima kwa Taifa huru kama Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, ahsante sana. Mheshimiwa Prof. Shukrani Elisha Manya atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei na Mheshimiwa Charles John Mwijage ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia Mpango wa Maendeleo ya Taifa ambao umewasilishwa Mezani. Naomba nikubaliane na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango ambaye alisema, na naomba nimnukuu kwamba, furaha ya wananchi, furaha ya Watanzania imeongezeka baada ya Serikali yao kukamilisha miradi mikubwa ya *SGR*. Yeye alisema na *DP World,* lakini mimi naomba niweke na Bwawa la Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa wale ambao wamesafiri na *SGR* wote wanafurahia maamuzi, utashi na utekelezaji wa Serikali yao wa kufanikisha miradi mikubwa. Kwa

jinsi hiyo, ni kweli kwamba inadhihirisha kwamba kumbe Serikali ikiamua, ikapanga vyema, inaweza kufanya mambo makubwa ambayo yanaongeza furaha ya wananchi na kwa kweli hili Serikali heko sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu *SGR* imerahisisha usafirishaji. Kila mtu sasa hivi anatamani kusafiri kupitia *SGR* ili apunguze masaa mengi ya kusafiri kutoka Dodoma kuja Dar es Saalam. Tunaiomba Serikali yetu, kwa kweli vile vipande vya kutoka hapa Dodoma kuelekea Mwanza na vyenyewe vifanywe haraka kwa umahiri huo huo ili tuweze kurahisiha usafirishaji. Pia, ni kweli kwamba Bwawa la Mwalimu Nyerere limeongeza nishati, umeme umekuwa mwingi na mgao umepungua na hilo nalo limeongeza furaha ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa utashi huo huo ambao Serikali imeweza kufanikisha miradi hii mikubwa, furaha ya Watanzania itakuwa maradufu iwapo miradi ambayo imeendelea kuwa inatajwa mwaka hadi mwaka na yenyewe ikatekelezwa mapema kwa kadiri ya inavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano, Mradi wa Kusindika na Kuchakata Gesi *(LNG)*, Mradi huu ukikamilika au ukianza mapema ni kichocheo cha viwanda vya mbolea na viwanda vya kemikali, vyote ambavyo kwa sasa tunapoongea *BRT* tunaagiza mbolea nje. Kumbe kama *LNG* ingeanza mapema na baada ya hapo tunakapata viwanda vinavyotokana na *LNG* vya mbolea, maana yake tuta-*save* fedha nyingi inayotumika kuagiza mbolea, kumbe ikapatikana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa pili, Mradi wa Chuma na *Vanadium* wa Liganga, mradi ambao umeendelea kuwa unahuishwa mwaka hadi mwaka katika mipango na hotuba za Bajeti za Serikali, tunajenga reli kwa kutumia chuma kingi sana. Ingekuwa ni habari gani kwamba tungezalisha chuma chetu wenyewe na hivyo kikasaidia kutokutumia chuma ambacho hakitokani na viwanda vyetu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja yangu hapa ni kwamba, kwa utashi ambao Serikali imefanikisha miradi mikubwa,

basi miradi hii mingine nayo ambayo imeendelea kuwa inaongelewa mwaka hadi mwaka, mimi ningetamani rafiki yangu Mheshimiwa Prof. Mkumbo, Mpango useme lini? Tusiendelee kusema tu, yaani *LNG* tunasema tunapanga, tunapanga, tunapanda, tuseme ni lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vihatarishi ambavyo mimi ninaviona katika hili ni kwamba majadiliano yanachukua muda mrefu. Tumeendelea kuwa tunajadili, lakini hatuweki ukomo. Ningetamani ili tuweze kupata manufaa ya kazi na miradi mikubwa inayoendelea, tuangalie kwamba majadiliano yafupishwe ili ifikie mahali miradi hii ianze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunaongea habari ya bajeti na kubana matumizi, lazima tunapofanya majadiliano ya mambo haya makubwa kwa mfano, *LNG* na taasisi za kimataifa, tuzingatie kwamba watu wawekeze weledi mkubwa katika majadiliano ili Serikali isiendelee kupoteza fedha za kutoingia katika mikataba ambayo ni ya maslahi kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana tumeendelea mwaka hadi mwaka kulipa mabilioni ya fedha kwa sababu ya mikataba, kwa sababu tupo katika *level* ya majadiliano, basi tuweke weledi hapo na uzalendo wa kutosha ili tunapoingia mikataba tupate fedha na siyo tena tuhamishe fedha ndani kupeleka kuwalipa ambao ni wadau wetu wa nje na hatimaye Serikali ikapoteza fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuchangia katika mpango, napenda kutambua kwamba, mojawapo ya mambo ya msingi katika utekelezaji wa bajeti ni kubana matumizi ya fedha za uendeshaji (fedha za utawala) na badala yake kuwekeza fedha nyingi katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ni kuwepo kwa utendaji wa pamoja. Nilitafuta neno hili kwa Kiswahili sikulipata vizuri, lakini ni *synergy* baina ya Wizara na Wizara, taasisi na taasisi katika Serikali. Hili jambo ninaamini linaleta tija na matokeo na mwisho wake ni huduma bora kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano ambao napenda kuuweka mezani asubuhi ya leo. Wizara ya Nishati na Wizara ya Maji, Mamlaka za Maji nchini zimeendelea kuwa zinatumia gharama kubwa sana katika uzalishaji wa maji. *TANESCO* imeendelea kuwa inatoza gharama kubwa hizi ikihusisha gharama za *KwH, KvA* na *VAT* na gharama ya kuanzisha mtambo. Yaani zote hizi zinawekwa mteja anapotumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano, *DAWASA* Dar es Salaam na Pwani wanatumia shilingi bilioni 2.5 kwa mwezi kwa ajili ya kuzalisha maji wakiilipa *TANESCO.* Arusha wanatumia shilingi bilioni moja; *KASHWASA* (Kahama na Shinyanga) shilingi bilioni 670; *DUWASA* hapa Dodoma tunapokaa wanatumia shilingi milioni 700 kwa mwezi kuzalisha maji kwa ajili ya kutoa huduma ya maji. Kwa nini napendekeza jambo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunao umeme ambao unaonekana unatosheleza mahitaji, unaotokana na ukamilishaji wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, pendekezo langu ni kwamba, kwa sababu tunao umeme wa kutosha, badala ya Watanzania kuomba tupunguziwe bei ya umeme, Mamlaka za Maji zipewe *special tariff* ya umeme. Kupewa *special tariff* ya umeme maana yake ni kwamba watapunguziwa gharama ili waweze kuzalisha maji kwa bei ndogo na hatimaye hayo yanayotokea kwa kupunguziwa *tariff* wananchi waweze kupata maji kwa gharama nafuu. Pia, Mamlaka za Maji ziweze kuweka miundombinu nyingine mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni kwamba umeme umepunguzwa kwa *section* moja ya Serikali, siyo kwa wananchi wote, lakini kwa kuipeleka katika mamlaka za Serikali ukaipa *special tariff* maana yake ni kwamba, kila kitu huko ambacho kinakwenda kwa mwananchi, kinakwenda kikiwa katika gharama nafuu ambayo mwananchi anaweza kuimudu. Kwa hiyo, katika mpango huu, siyo jambo ambalo nimeliona katika Mpango, lakini napendekeza kwamba Wizara ya Nishati na Wizara ya Maji waweze kukaa pamoja halafu washushe *tariff* kwa hizi mamlaka za maji. Kwa mfano, kwenye *VAT,* Maji ni huduma, lakini unatoza *VAT* Taasisi ya Serikali na Serikali. Maji ni huduma, unatoza

gharama ya kuanzisha mtambo *KvA*, kwa hiyo, gharama inakuwa kubwa *unnecessarily. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pendekezo langu ni kwamba, naomba kuwe na *special tariff*. Mheshimiwa Prof. Mkumbo rafiki yangu ninaziombea mamlaka za maji *special tariffs,* bei iliyoshuka ya umeme kwa Mamlaka za Maji tupate maji kwa bei nafuu halafu Mamlaka za Maji ziweze kusambaza maji mengi kwa wananchi. Ninaamini pamoja na hayo, furaha ya wananchi itaendelea kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ahsante kwa nafasi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kusimamia mchakato wa kutengeneza mapendekezo na mwongozo huu ambao tunaujadili siku ya leo, maono yake na maelekezo yake ambayo ninaamini yamesheheni kwenye maandiko ambayo tumepokea ya mapendekezo ya Mpango na Mwongozo wa Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, nawapongeza pia Mawaziri wanaohusika kwa sababu ninaamini kusema kweli wamechakata vizuri yale maelekezo waliyopewa na Mheshimiwa Rais. Vilevile, nazipongeza na timu zao kwenye Wizara hizi mbili zinazohusika na Tume ya Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma maandiko yanayohusiana na hali ya uchumi ambayo wameeleza vizuri sana kwenye Mpango na Mwongozo utahitimisha kwamba, uchumi wa dunia, uchumi wa kanda na uchumi wa Tanzania sasa unaelekeza kwenye hali iliyokuwepo kabla ya UVIKO-19, utaona kwamba, hali ya uchumi kwenye nchi zote duniani kwa mfano,

ongezeko la pato limefikia kwenye 3.3% na kwenye nchi hizi ambazo zimeendelea utaona ongezeko la pato lao linakwenda kwenye 1.7% mpaka asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hivyo ilivyo kwa nchi zilizoendelea, haziwezi kuendelea kukuza uchumi wao kwa kiasi kikubwa kwa sababu *resources* zinakuwa *almost fully employed* na hawana uwezo wa kukuza sana mapato yao kama sisi tunavyostahili kukuza kwenye asilimia tano mpaka 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, utaona kwamba mfumko wa bei duniani umepungua kutoka 8.1% umefikia kwenye 5.9% katika kipindi cha mwaka huu tulionao. Kwa hiyo, naona kwamba maendeleo haya tunaona mwelekeo unatupatia fursa nyingi. Kwa mfano, ikiwa mfumko wa bei umeshuka; na ninyi mtakumbuka kwamba nchi zinazoendelea ikiwemo Marekani zilianza kutekeleza Sera ya Kubana *Money Supply* (Ujazi wa fedha) kwa kuongeza riba mara tu, *inflation* ilivyokuwa juu sana. Sasa, *inflation* imeshuka kwenye *two digit,* sasa hivi ipo kwenye 5.9% kwa wastani na kwenye nchi nyingine inashuka. Kwa mfano, wanaita *secure overnight financing rates (SOFR)* ambayo imekaa badala ya *LIBOR*. Sasa hivi ipo kwenye 3.5%. Hii inasema nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema kwamba, nchi ya Marekani inaelekea sasa kulegeza ile Sera ya Fedha ya Kubana na kwa hiyo, riba zitashuka na itatupatia fursa sasa ya kuweza kukopa kwa gharama nafuu sana ukilinganisha na zile ambazo tumekopea mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ni kwamba hii *SOFR* ni inasema ndiyo *benchmark* ambayo unaongeza kwenye ile *grace premium* ambayo mmekubaliana. Kila wakati ikipanda ina maana na gharama zako zinapanda hata kwa mikopo ya nyuma. Kwa hiyo, ninaamini kwamba gharama za ku-*service* mikopo zitapungua na kuchukua mikopo mingine zitapungua na ninaamini Serikali itakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mazuri sana yametokea kwenye nchi zilizo kwenye Kanda yetu ya *East Africa* na *SADC, inflation* imepanda sana. Kuna nchi kwa mfano Burundi,

*inflation* yao ni takribani 20%; ukienda *South Sudan, inflation* ni 40.2% na ukija hata kwenye nchi nyingine za *East Africa* zinakuwa zina *inflation* kubwa kuliko ya kwetu ambayo ni asilimia tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya hizi *inflation* kwenda juu ni upungufu wa vyakula, lakini sisi tuna vyakula na tuna-*reserve* kwenye *NFRA*. Kwa hiyo, naamini kwamba sasa tunaweza tukafaidi na tukaruhusu wananchi wetu wakanufaika kwa kuwawezesha kuuza chakula kile karibia na msimu mwingine unaingia kwa bei nzuri, lakini siyo tu chakula, na bidhaa nyingine ambazo zinazalishwa kwenye viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sasa bajeti yenyewe utaona kwamba bajeti ya mwaka huu imepanga kutumia shilingi trilioni 55.1. Sasa hilo ni ongezeko la 16.2%, ni ongezeko kubwa sana. Ongezeko la mapato ni 12.6% kutoka trilioni 34.6 hadi 38.46. Kwa hiyo, utaona kwamba matumizi yanakua kwa kasi kubwa sana ukilinganisha na mapato. Kwa hiyo, hilo ni jambo la kuangalia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba bahati mbaya kwenye matumizi, bajeti ya maendeleo sasa inapungua kwa uwiano wa bajeti yote. Inapungua, inakwenda kwenye 29.9%. Kwa miaka ya nyuma hii mitatu iliyoisha, bajeti ya maendeleo ilikuwa inachukua 33.7% ya bajeti yote. Mimi ninaamini kwamba tulikuwa tumejiwekea *some sort of indicative parameter* kwamba, bajeti ya maendeleo isipungue chini ya 30%, lakini naona kwa mwaka huu inakuwa ngumu kidogo kwa sababu pengine kuna uchaguzi, gharama zinakuwepo za ziada na tunafungua vitu vingi vipya kwenye miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuongeze matumizi ya kawaida, lakini tuangalie vizuri tusiondoke kwenye *benchmark* ya 30%. Tujaribu kwenda kwenye hilo. Niseme kwamba bajeti hiyo kwa namba imeongezeka kwa 7.4%, lakini bado uwiano wake kwa bajeti nzima siyo mzuri. Ubaya mmoja wa ongezeko kubwa la namna hii, halafu tunaweka kwenye ukomo, tunaunda *pipeline* kubwa ya miradi ambayo haitekelezeki ikamalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kinachotokea ni kwamba ile bajeti ya kawaida inakuwa *disbursed,* lakini bajeti ya maendeleo inabakia kuwa Mawaziri wameshapewa ukomo, kwa hiyo, Julai wana-*contract* ile miradi yote bila kujali kwamba, je, fedha itapatikana? Tunazungumzia *cash budget,* lakini inakuwa siyo *cash budget*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi imeshakuwa *contracted,* wameshapewa *advance payment,* kwa hiyo, unakuta ile miradi inaanza kukaa kwenye *pipeline,* fedha haiwi *disbursed* kwenye ile miradi. Hii ndiyo chanzo cha tatizo hilo unaloona la kusema kwamba, jamani sasa mbona hawalipi? Mbona wameondoka kwenye miradi! Wakandarasi hawafanyi kazi, wanaondoka, wanakimbia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba kwa sababu *pipeline* ipo na inakuwa *carried forward from a year to a year*. Ukiangalia *deficit* tunayopata kwenye makusanyo ni *five percent*, yaani kwa miaka mitano ukichukua tumefanya hesabu hizo ni *five percent* tuna-*miss* kila mwaka. Sasa, kila mwaka uki-*miss five percent* kwenye *40 trillion* ina maana kwa *five years* unakuwa umeshaunda *pipeline* ya vitu ambavyo havijalipika kwa sababu ya makusanyo, *10 trillion*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama hiyo ni ya kweli, lakini ukweli ninaamini kwamba kwenye *pipeline* Wizara ya Fedha ikiangalia vizuri itakuta kuna vitu vya kulipa. Wakandarasi wa kuwalipa na hawa wa chakula shuleni kama *10 trillion it is a lot of money*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hivi, Serikali sasa iwaagize Maafisa Masuuli waweke *line item* kabisa ya kulipa madeni haya na ninashukuru kwamba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu alivyo-*present* alisema kwamba mwaka huu hawataingia kwenye miradi mipya. Nafikiri *that is nice and it is a very good stance*. Wafanye ili waweze kuweka ile *line* walipe madeni ya zamani, halafu ndiyo tuanze sasa kuwekeza, lakini ile ya vituo vya afya vya kimkakati msituache solemba na msitutoe, acha ikae tu tutekeleze. Bwana asifiwe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, niseme hilo ni tatizo ambalo tumeliunda wenyewe na ni tatizo ambalo lazima tu-*deal* nalo. Ukiangalia vizuri sasa kwenye mambo mengine ya kimkakati utaona kwamba, kitu kitakachotutoa kwenye hali hii ya makusanyo na Serikali yenyewe inasema ni *private sector* kuweza kuwekeza. Miradi hii ya kimkakati imeingia kwenye *stream* sasa inazalisha, lakini *private sector* bado hawajahamasika kuanza kuwekeza na kuzalisha, wale wa nje na hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, naomba hivi, ili tujiridhishe kwamba kweli hakuna tatizo ambalo linasumbua watu kuwekeza, tutengeneze *international competitiveness index* yetu wenyewe. Tujiulize, watu wa nje wanatu-*rank* hivi, lakini tuchukue vile vigezo vichache tutengeneze kwamba, sisi bei yetu ipo hivi na tuweze kuiuza kwa wawekezaji kwamba kweli hii nchi yetu wanavyosema siyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna bwawa, umeme una-*stabilize,* reli na yenyewe itakuja i-*stream* na vitu vyote hivyo, ili kuanza kuuza hii nchi yetu vizuri zaidi na sisi tujiridhishe kweli tunakidhi mahitaji kwa sababu *competitiveness* yetu kulingana na nchi nyingine hapa Afrika ipo juu. Naamini tukitengeneza na tukifuatilia walikuwa wameanza hapo nyuma kidogo, walikuwa wanakaa Makatibu Wakuu wanaorodhesha mambo ambayo ni ya msingi ili kuweza ku-*boost business indicator* yetu, lakini Mheshimiwa Waziri ninaona siku hizi hiyo haipo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme cha mwisho kwamba, nafikiri tumefanya makubwa, na Bwawa la Nyerere limeleta mambo mazito. Baada ya kuleta mambo mazito sasa ni kwamba, yaani hakuna kitu muhimu kama umeme wa uhakika kwenye nchi. Nchi zote hizi hapa kwetu, nyuma huku, ukienda huko *SADC,* umeme ni matatizo. Sasa, hapa kwetu tunaanza kupata umeme wa uhakika, ni Mungu ametuletea hiki kitu, ni bingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutumie hilo na pia, tusibweteke, ila tuwaombe *TANESCO* wawe *flexible* katika kuingiza watu binafsi kuzalisha umeme. Tatizo la watu binafsi kuingia kuzalisha umeme, kwa mfano kule Ruhuji na Rumatali

watu binafsi wangewekeza fedha, hata wa nje wangewekeza kwa sababu, umeme unauzika *anywhere*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *issue* ni kwamba, tatizo ni *pricing model* ya *TANESCO*. *Pricing model,* sisi umeme wetu bei yake ni ya chini, kwa hiyo, mtu ukiwekeza kwa bei hii ya chini ambayo umeme unapatikana hapa kwetu, mwekezaji binafsi hawezi kupata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuwe *flexible*, tujue kwamba, tutafanyaje ili watu binafsi wawekeze, hata kama watapata *subside* kidogo kupunguza yale makali. Wawekeze halafu tuone namna gani tuta-*price* ule umeme wetu. Tusiongeze bei, lakini kwa sababu unakuwa mwingi, basi inaweza ikawa rahisi ku-*manage,* lakini tusizinyime *private sector* kuingia kuzalisha, siyo tu umeme wa maji, ila hata *geothermal* sasa ndiyo umekuwa umeme ambao una tija sana. Wenzetu hapa majirani wameingiza umeme mwingi wa *geothermal* ambao ni umeme unaozalishwa kwa namna ambayo inatunza mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nawaomba wenzangu wote wakubaliane na mapendekezo haya ili tuweze kuendelea mbele. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei. Mheshimiwa Charles John Mwijage, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga na Mheshimiwa *Eng*. Dkt. Leonard Chamuriho ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa mwaka 2025/2026. Awali ya yote, nawapongeza viongozi ambao walipata fursa ya kutuongoza katika kuleta mbele yetu Mapendekezo ya Mpango; Waziri wa Mipango, Waziri wa Fedha, na Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bunge inayohusika na Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza na nimepitia maandiko yao, kwa kiasi kikubwa ninaunga mkono mapendekezo yao na kwa sababu, ninayo fursa ya kushauri, ninaomba nishauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumzwa mafanikio na mengine yamewekewa picha, nami mafanikio ambayo yameandikwa tu, lakini hayakuwekewa picha, niyaseme. Linalofurahisha ni mafanikio yetu katika kuuzwa nje, tumeweza kuuza nje dola bilioni 14 na yenyewe inapaswa kuwa *bolded*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kusimamia vizuri, sifurahi kwamba, tumeagiza nje bidhaa za dola bilioni 16 na kupunguza nakisi kufikia dola bilioni 2.4, ambayo inatupeleka kule tulikokuwa mwaka 2019/2020, tulipokuwa na dola bilioni 1.3. Hayo ni mafanikio niliyoyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ambayo nachukua fursa hii kuwapongeza wakulima wa nchi hii ni kwamba, wakulima wa Tanzania wale wadogo wa jembe la mkono wameweza kuzalisha chakula tani milioni 22, ambayo ni asilimia moja ya 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Mipango, popote tuendapo tukikutana tunakunywa ile kahawa yetu, anieleze, hawa watu wanaozalisha chakula hiki, hao wa jembe la mkono, miaka 30, miaka 60, watakuwa na hali gani? Kwa sababu, tulikuwa nao miaka 60 iliyopita, hatuwezi kuwaacha, tunakwenda nao vipi? Nao mafanikio yao tumeyaona. Pia, wakusanya mapato wana mikiki yao, na hesabu zinaonesha wameweza kukusanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mafanikio ninapenda niliseme, ni pato la Taifa. Pato la Taifa limeongezeka mpaka shilingi trilioni 148 kutoka shilingi trilioni 141.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nipite kwenye michango. Eneo ambalo nataka kupendekeza mahususi, ni kwenye mapendekezo ya mwaka 2025/2026, yale ya miaka mingine sitashughulika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuzungumza hali ya dunia tumezungumza mazingira, lakini jambo moja, hatukwenda mahususi kuliangalia ni hali inayowahusu watu wa *SADC*, suala la ukame wa Zimbabwe na ukame wa Zambia. Wenzetu wana ukame mkubwa, lakini imedokezwa kwenye hotuba hapa kwamba, nasi kuna hatari ya mazingira, kama wanavyosema wataalamu wa hali ya hewa, na kwetu hali ya mvua siyo nzuri, tunajipangaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoshauri, ninakushukuru Mtumishi wa Bwana ninamwona pale, tufanye haraka twende kumwagilia. Tujenge mifumo ya kumwagilia Kanda ya Ziwa ambako *already* kuna maji. Twende kule kumwagilia kwa sababu, kilichompata mwenzetu Zimbabwe, kikampata Zambia, Mungu apishe mbali kinaweza kutupata, lakini ndugu zangu wa Bunda, ndugu zangu wa Geita, ndugu zangu wa Muleba wana maji, Mungu kawapa. Tukimbilie kule, kwa sababu mkono umpigao mwenzio unamfundisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, narudi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na wenzake. Wamezungumzia dhana ya kununua mafuta na kuyahifadhi yakiwa na bei ndogo kwa kuotea kwamba, yakipanda bei wataweza kuuza. Nakubaliana na suala hilo, lakini linahitaji uangalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa Kamati ya Nishati wakitaka kuzungumza jambo hilo, mimi ni *old model*, waniite wanieleze wanaweza kufanya mchezo huo namna gani? Kwa sababu, tunakwenda mbele haturudi nyuma, ninaishauri Serikali ianze kuwafundisha na kuwaelimisha wataalamu mahususi katika sekta hii. Siyo rahisi sekta hii kuingia na kufanya, inahitaji ujuzi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo ya Kamati ya Bajeti, kuna mambo yamependekezwa. Mojawapo wamependekeza kwamba, tuboreshe zao la nazi ambalo Tanzania tunaongoza Afrika na katika kumi bora tumo. Nakubaliana kwamba, tuongeze zao la nazi, lakini pamoja na hilo, nina mazao mengine tuwekeze nguvu za ziada. Nakubaliana na mpango wa Wizara katika kufanya *irrigation*. Tanzania

tunakwenda vizuri ingawa watu wengine hawajaona. Tulikuwa kwenye tani milioni mbili, tumekwenda kwenye tani milioni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalamu wanasema sisi tunaweza kufika kwenye tani milioni 10 na Afrika inaagiza nje tani milioni 16. Kwa hiyo, kuna uwezekano, Tanzania, kama tukichukua fursa hii kwa mwaka mmoja tu, haya ni mazao, ninazungumza bajeti ya mwaka 2025/2026, tunaweza kupata *potential* ya ku-*export* katika Afrika na tukaweza kupata kipato cha takribani dola bilioni tatu. Dola bilioni tatu kutoka kwenye mpunga! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine lenye fursa, nimewahi kumweleza Waziri wa Kilimo, nimekuwa niki-*share* naye kinachoendelea Uganda. Zao la kahawa limebadilika, limekuwa na *demand* kubwa. Uganda Kaskazini wameingia kwa nguvu wakiongeza maeneo ya kilimo, waki-*target* hilo zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo siri, Mheshimiwa Rais alipokwenda China alipata *deal* ya kuweza kuuza kahawa China na hakuna mtu anakula kama Mchina. Mchina akiamua kununua korosho yetu, tumepita. Sasa ameamua kununua kahawa. Tuongeze kilimo cha kahawa. Kwetu Kagera, Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Fatma amejasiria, Wilaya ya Muleba unaulizwa unalima wapi ulime kahawa? Ninalisemea suala la kahawa; haya mazao pamoja na nazi mliyosema, sawa, ninaunga mkono, lakini tuongeze mazao haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao lingine ni eneo lenye matatizo, kuna matunda yanayoning'inia. Tanzania tunayo fursa ya mifugo. Nimewahi kuzungumza hapa kwamba, *market* ya *gulf* ni dola bilioni tisa, lakini ninazo taarifa Malaysia wanahitaji nyama kutoka Tanzania tani 100,000. Leo tunauza nyama dola milioni 57. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni soko lililopo linalotusubiri na nimesoma andiko moja wamesema maneno siwezi kuyatamka hapa. Wanasema, ardhi tunayo, mifugo inakubali, lakini tumeangalia tu, yaani ukiisikia kwa Kiingereza ni tusi, yaani eti sisi tumeangalia tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa soko lipo, naomba, na hii ni biashara ya mwaka mmoja, tuwekeze zaidi kwenye sekta ya mifugo. Sekta ya mifugo, nina imani na *Treasurer Registrar* Bwana Mchechu, aisimamie *NARCO*. *NARCO* wanazo hekta 600,000, msiwaangalie walioko ndani ya *NARCO; NARCO* wawezeshwe wafanye kazi kwenye *business mind*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa kwenye Kamati ya Kilimo, wale tuliokuwanao, tulifanya mchakato, tulipitia takwimu tukaona zikiwekezwa shilingi bilioni 400 ndani yake, dola moja ingezaa dola 2.5. Watanzania wengi wanaopewa vitalu *NARCO* wanapewa vichaka na misitu. Hawajapewa *Ranch*, vile ni vichaka na misitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inapaswa iige mfumo wa Zimbabwe, mtengeneze *pastures,* muwape ng'ombe wa kisasa wawe wa nyama au wa maziwa, watu wanaingia na kuzalisha soko likiwa lipo. Tumefanya kazi, tumepata soko *gulf,* hilo la Malaysia, tuna *contact*. Sisi mwaka 2023 tulitaka kupata aibu, walikuja watu wanataka mbuzi hapa, tulikimbizana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta nyingine, nimemsikia Naibu Waziri wa Mifugo, sekta ya kufuga samaki ni aibu ya aibu, huwezi kusema. Katika nchi zinazofanya vizuri kufuga samaki Afrika, Tanzania haimo, Zambia imo. Ile Nchi ya Zambia haina ziwa, ni mabwawa yale. Watu wana mabwawa wanaita maziwa, sisi tunaongoza kwa maji. Maji ya kwetu huwezi kuogelea, huwezi kufanya lolote, twende tukafuge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri wa Mipango, namwona Naibu Waziri ananiangalia. Hatujafanya lolote, hatujatumia maji yetu. Mimi nina *square kilometer* 7,200 Wilaya ya Muleba; 10,200 Mkoa wa Kagera. Kama nimepewa vizimba, hakuna chochote kimefanyika, tunachezea maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Morocco wanapata dola bilioni moja kutokana na samaki. Misri anatuongoza, anapata *billions of monies*. Hayo ni mambo ya mwaka mmoja ninayozungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia *exports,* kwamba viwanda vinaweza ku-*export* zaidi. Kuna kazi ya kufanyika, *the Blueprint Regulated Reform*, Mheshimiwa Waziri wa Mipango aende akaipitie tena. Nimeipitia sana, yako makosa, lakini sehemu kubwa iko sawa, ile haiwezi kutekelezwa robo. Waziri ahamasishe viwanda ikiwemo kutekeleza ile *Blueprint Regulatory Reform*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kupunguza gharama. Kama alivyosema Mheshimiwa Prof. Manya, tupunguze gharama *(the cost of production)* hapa, na unaifanya makusudi kwa *Cross-subsidize*. *Bangladesh*, kwa nini watu wanakwenda kuzalisha kule *Bangladesh*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kukaa tukaangalia namna ya kupunguza kusudi watu waliokuwa wanazalisha Tanzania, wakahamia Zambia, Kongo, na Uganda warudi. Kuna watu walikuwa wanazalisha hapa Tanzania wako Uganda, tunawajua kwa majina. Kuna mzalishaji mmoja alikuwa Tanga, anaondoka kwenda Zambia, aliniaga. Nashukuru Serikali imekuja na mfumo wa kupitia kodi, mpitie kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimekuwepo kilio cha kuiomba Kariakoo irudi Ilala. Kariakoo ilihamia Kampala na Zambia. *Bring back our Kariakoo*. Tunataka watu waje hapa. Watu wachangamke, wafanye kazi saa 24, kama anavyosema Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, lakini lazima mwangalie *tax regime*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni makusanyo mazuri ya *TRA*. Ukienda mtaani, watu wa mtaani wanakueleza kwa majina, mabingwa wa kukwepa kodi. Unakuwa na mtu unampa jambo anasema na wewe unafahamiana na mkwepa kodi. Hao wakwepa kodi mwaambie inatosha kwa kodi walizokwepa. Tunahitaji kodi ili kutekeleza mipango yetu ya mwaka kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema nazungumzia mpango wa mwaka kesho. Tumefanya kazi nzuri kwenye miradi ya shilingi trilioni 10, na shilingi trilioni sita. Fikiria kama Taifa, kama tutachukua

shilingi trilioni 10 tukaziweka kwenye *production sector*, rafiki yangu Mheshimiwa Waziri wa Mipango, ndiyo unajenga uchumi jumuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwambia rafiki yangu Mheshimiwa Mwambe, alikuwa ananieleza mradi mmoja. Nikasema unauonaje? Akasema *super* sana. Nikasema, ulichungulia nje! Alichoniambia ni siri yangu na yeye. Tunataka tuwajumuishe watu, na kuwajumuisha watu ni kuwalazimisha kwenda katika shughuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa wa Kagera anakwambiaje? Watoto wa siku hizi huwezi kuwapeleka kwenye shughuli kama wagagagigikoko. Amekwenda akatafuta *excavator* Wizara ya Kilimo, wakampa matrekta. Vijana wanalimiwa, wanapelekwa shambani, wanafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaeleza *potential* ya mpunga, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ahsante umekuja. Tunataka mabonde yote ya Ziwa Victoria yalimwe. Tusije kuyalima baada ya ukame kuwa umetufikia kama Zimbabwe, na hayo ni mambo ya *short-term*. Tumefanyia kazi mambo marefu ya *long-term*, tunataka ya *short term*, ndiyo mpango wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kukopa, Kamati imependekeza kwamba tuache kukopa. Nimemsikia Mheshimiwa Dkt. Kimei, sawa, lakini akalegea kidogo alipozungumzia vituo. Mimi nasema, tukae chini kwa akili ya bishara na hesabu. Mradi unaoweza kulipa *immediately* ukopeshwe, turidhike kwamba hii inakuwepo, unaweka shilingi unapata mbili na nusu, kama nilivyopendekeza kwenye sekta ya mifugo na niko tayari kwenda kwenye Kamati. Muilete kwenye Kamati, sitahamia huko, nitakuja kuwaonesha tulipoishia kusudi mwanzie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono mapendekezo. Naomba tuendelee. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwijage na uzuri Mheshimiwa Waziri upo hapa. Moja katika sekta ambazo zinaelekea kufa sasa ni hii ya ufugaji wa samaki. Sababu ni moja

tu kwamba, tunawekeza nguvu zaidi kwenye kukusanya kodi kuliko kuwawezesha wajasiriamali kuzalisha kwa gharama nafuu. Leo samaki wanaotoka Zambia na China wanauzwa nchini kwa bei rahisi zaidi kuliko wanaozalishwa ndani ya nchi.

Hii ni changamoto, siyo kwenye samaki peke yake, lakini hata kwenye bidhaa nyingi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri upo hapa, ninadhani hili ulipe uzito wake. *(Makofi)*

Namkaribisha Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga. Atafuatia Mheshimiwa *Eng.* Dkt. Leonard Chamuriho na Mheshimiwa Cecil David Mwambe ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Nami naungana na Wabunge wenzangu kupongeza upande wa Serikali kwa maandalizi mazuri ya taarifa hizi na ninaipongeza Kamati yangu ya Bajeti na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Njeza, kwa kutusimamia vizuri kuweza kuishauri vizuri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anaendelea kuifanya. Hata wananchi kule majimboni wanaona jinsi fedha zinavyokwenda na ambavyo miradi inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, liko jambo ambalo nisipolisema wapigakura wangu wataona kwamba, Mbunge wetu namna gani huyu? Hawatanielewa kwa sababu, hata jana nimetoka jimboni, ilikuwa kila unachoeleza wanakukumbusha juu ya barabara, kipande kinachoanzia Itoni mpaka Lusitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali imetujengea barabara nzuri sana ya zege kutoka Lusitu mpaka Mawengi, takribani shilingi bilioni 179 zilitumika. Awamu ya pili wakaja upande wa Njombe, kutoka Lusitu hadi Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa bahati mbaya sana kazi ilianza vizuri sana, wananchi walishangilia sana, lakini kwa mkoa

wetu ule wa Njombe mwezi huu ni msimu wa mvua kali sana na mvua ikianza pale wananchi wana hofu ni kwa jinsi gani Mheshimiwa Bashe ataweza kuwapelekea mbolea kule Ludewa? Ni kwa jinsi gani pembejeo nyingine za kilimo zitaweza kwenda? Ni kwa namna gani wananchi wataweza kusafiri kwenda kupata matibabu Ikonda, Hospitali ya Rufaa Njombe na maeneo mengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kabla sijaendelea na mchango wangu naiomba sana Serikali iweze kuchukua hatua za haraka kuhakikisha kipande kile cha Lusitu kwenda Njombe kinaendelea vizuri. Niwe muungwana, ninamshukuru sana Mheshimiwa Bashungwa, haya maeneo ninayoyazungumza alikuja mwenyewe, akayaona. Kwa hiyo, nina imani haya ninayoyasema atakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudi tena kuendelea kuipongeza Serikali kwa Mpango mzuri wa Maendeleo wa Taifa. Naungana na Wabunge wenzangu ambao wameainisha sekta zile ambazo zinaweza kuinua sana pato la mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona pato la Taifa linakua vizuri sana, lakini pato la mtu mmoja mmoja hata katika Taarifa ya Kamati yetu tumeona bado ni changamoto. Sasa tunajiuliza, je, zile tafiti ambazo zinafanyika za kuandaa pato la mtu mmoja mmoja ni za usahihi? Wanatumia njia gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kukuta pale kwako, Madaba, kuna familia moja ina watoto wengi, lakini wanamudu mahitaji yote ya kila siku, lakini yanategemea jasho lao na namna wanavyozalisha shambani. Kila kitu wanategemea shambani, kitu cha dukani labda chumvi na sukari, lakini vitu vingine vyote ni kule. Watu kama hawa wanafanyiwa vipi tathmini kuweza kujua pato lao kwa mtu mmoja mmoja? Hilo limebakia swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, maeneo ambayo Wabunge wengi wameona yanaweza kusaidia kuinua pato la mtu mmoja mmoja, kwanza ni eneo la kilimo, tukiboresha eneo la kilimo kwa sababu ndiko eneo ambalo Watanzania wengi zaidi

wanapata ajira, nasi Wabunge wengi humu ndani tunatokana na wakulima, hasa pale kwangu Ludewa nako wananchi asilimia kubwa shughuli yao ni kilimo. Kilimo kimeajiri zaidi ya 65% hadi 70% ya Watanzania na kinatoa mchango mkubwa sana kwa usalama wa chakula. Vilevile kinachangia vizuri kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kuinua pato la mtu mmoja mmoja, eneo hili la kilimo hasa, tumsaidie mwananchi katika kuongeza tija, kwa hekari pale akitumia mbegu, anaandaa shamba, anakuzia mara moja, mara mbili palizi, zile gharama anazozitumia je, baada ya mauzo mwishoni anapata faida kiasi gani? Je, hiyo shughuli, anapata moyo anavutiwa kuendelea kuifanya kila mwaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, eneo hili tukimsaidia mkulima akapata soko la kutosha na hizi ruzuku za mbolea na mbegu, ambazo wanapewa, wananchi watazalisha zaidi kwa sababu watakuwa na uhakika wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa *NFRA* mwaka huu wamefanya kazi nzuri, wamenunua tani nyingi sana za mahindi na mwanzoni walikuwa wanalipa vizuri sana, lakini hapa mwishoni kuna wananchi wachache ambao kidogo kama mwezi hivi wamecheleweshewa malipo yao na huu ndiyo ulikuwa msimu wa kupeleka watoto vyuo vikuu. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo aweze kuingilia kati ili wananchi hawa wasivunjike moyo wa kuendelea kuzalisha mazao kwa wingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile watu wa *NFRA,* kwa sababu nchi nyingi za Afrika zinakabiliwa na ukame, na zina njaa, wangeweza kutafuta masoko mapema ili yale mazao wanayoyakusanya kule waweze kuyauza nchi jirani ambazo zina uhitaji mkubwa wa chakula. Kwa hiyo, kukiwa na soko zuri wananchi wengi watajituma kwenda shambani, watazalisha zaidi na pato la mtu mmoja mmoja linaweza kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko hili ni pamoja na kuruhusu ile mipaka iwe wazi kwa wafanyabiashara wa mazao ya chakula, wakiruhusiwa, ila tu wananchi wapewe elimu namna ya kuweka

chakula akiba kwa ajili ya familia yao mwaka mzima. Kwa hiyo, wananchi wakishakuwa na uhakika soko lipo, kwa kweli watazalisha kwa wingi zaidi kwa sababu watakuwa na uhakika wa kwamba wakizalisha mazao ya chakula wanapata kipato, eneo hili litainua sana pato la mtu mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la kilimo, mwaka huu kumekuwa na changamoto kubwa sana ya maghala, ma-*godown* au maeneo ya kuhifadhia mazao. Kwa mfano mazao kama mahindi, hapa kuna njia mbili; njia ya kwanza, Serikali itabirike kwamba huu ununuzi wa mahindi unaofanywa na *NFRA* ufanyike mfululizo miaka mitatu hadi minne. Hii itavutia watu binafsi kwenda kuwekeza kwenye ujenzi wa ma-*godown* na maghala ili waweze kuyapangisha kwa *NFRA,* lakini ikiwa mwaka huu wananunua miaka miwili hawanunui, inaweza ikawa changamoto na hii sasa itasababisha kuhitaji Serikali yenyewe iweze kujenga maghala ya kutosha ili wananchi waweze kuzalisha kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la uzalishaji kwenye kilimo ili kuinua pato la mwananchi mmoja mmoja linaenda sambamaba na miundombinu ya barabara za vijijini. Zile barabara za *TARURA* wanavyozitengeneza wanaweka ukomo kwenye uzito, kwa hiyo wanatengeneza barabara vizuri lakini wanazuia lori tani zaidi ya 10 lisipite pale, lakini maeneo yale ni ukanda wa uzalishaji mkubwa sana, una mazao mengi, unahitaji malori ya tani zaidi na wafanyabiashara kupeleka magari madogo madogo, wanaona ni hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe wito kwa Serikali kuainisha barabara za vijijini zile ambazo zipo kwenye ukanda wa uzalishaji ili ziweze kuwekewa kiwango kikubwa cha changarawe ili magari ya uzito wowote yaweze kuingia mashabani. Kama magari ya mizigo ya uzito mkubwa hayatoruhusiwa, kwa kweli tutarudisha nyuma sana maendeleo ya wakulima na pato la mtu mmoja mmoja linaweza kuathirika kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo linaweza kuinua pato la mwananchi mmoja mmoja ni eneo la uvuvi. Nchi hii imejaliwa kuwa na maziwa, bahari na wananchi wengi

wanajishughulisha humo. Kwa hiyo, kinachotakiwa ni Serikali kuona namna gani tunaweza kuwawezesha wananchi wale wa kando kando ya maziwa, bahari, mito mikubwa, mabwawa, wakawezeshwa kufanya ufugaji wa samaki kwa kutumia vizimba. Imefanyika sana Ziwa Victoria lakini yapo maeneo ambayo bado rasilimali ya maji hatujaitumia ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nashauri kwamba eneo hili tulitilie mkazo ili wananchi waweze kufuga samaki kwenye vizimba. Hii itasaidia kutengeneza ajira kwa vijana wengi ambao ni changamoto na hata wakina mama na watu wengine, pia hata usalama wa chakula utakuwa wa kiwango cha juu. Eneo la mifugo pia tukiweza kulizingatia itakuwa nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishukuru Serikali kwa kupiga hatua kwenye eneo la uwekezaji eneo la Liganga. Pale Liganga kuna miradi miwili, kuna ule mradi wa kimataifa ambao Serikali iliingia mkataba na ile Kampuni ya *Sichuan Hongda* ambao umekwama muda mrefu, lakini upo mradi wa Maganga matitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza eneo la Manganga Matitu kwa hatua iliyofikiwa, hata jana tulikuwa na mwekezaji kule ameshasaini mkataba na anakwenda kuanza ujenzi wa viwanda. Atazalisha tani milioni moja za chuma kwa mwaka. Kwa hiyo zile trilioni 2.9 iliyokuwa inaagizwa nje ya nchi sasa itaagizwa Ludewa. Kwa hiyo, hii ni hatua kubwa sana, na ni jambo la kupongeza na tuwaombe Serikali waongeze *speed* kwenye ule mradi mwingine mkubwa wa kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile eneo la makaa ya mawe pale Mchuchuma watu wa *NDC* kuna Mkurugenzi mzuri sana Dkt. Nicolaus. Aongezewe wasaidizi wazuri ambao wanaweza kumsaidia kufuatilia mambo yakaenda haraka na uwekezaji ukaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naomba na fidia ziweze kulipwa kwa wananchi wachache waliosalia wa Ketewaka na wale wengine wa Maganga Matitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja nashukuru sana kwa kupewa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kamonga. Namkaribisha sasa Mheshimiwa Dkt. Leonard Chamuriho, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia katika mapendekezo ya mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuiongoza nchi vizuri ili mipango hii ambayo tunakuja kujadili hapa iweze kutekelezeka kwa utulivu na ukamilifu wake kama ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapenda kumpongeza kwa utekelezaji wake katika utafutaji na upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya kutekeleza mipango hii. Vilevile ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwa mpango mzuri ambao ametuletea ambao nitauelezea hivi karibuni, vilevile na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa ajili ya mapendekezo au mwongozo aliyotupa kwa ajili ya bajeti inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ambao umependekezwa ni wa mwisho katika ile mipango ya miaka mitano ambao unaishia 2025/2026 na tunampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa sababu umeendelea kuweka misingi ya Tanzania tunayoitaka. Tunasema hivyo kwa sababu gani? Kwa sababu ameendelea kujenga juu ya sehemu ambayo tumefikia, hakuanzisha mambo mapya. Kwa hiyo, ina maana mipango hii ni endelevu, hivyo tunakwenda vizuri katika eneo la mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia katika ukurasa wa nne wa mpango wake, malengo mahususi mengi yanaelezea

kuendeleaza au kukamilisha. Kwa hiyo, ina maana ni mwendelezo wa yale ambayo yalikuwa yamepangwa hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tukiangalia vipaumbele vyake, ametuwekea vipaumbele sita ambavyo nitajikita katika kimojawapo katika mchango wangu, vipaumbele vyake ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi; pili, ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma ambacho ndipo nitakachochangia zaidi hapo, tatu, ni kukuza uwekezaji na biashara. Vilevile ameweka kipaumbele cha kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani, nitajikita zaidi katika viwanda vya malighafi au rasilimali za ujenzi. Ukiangalia malengo mahsusi ya mpango yapo saba. Nikiangalia lengo namba nne ambalo ni kukamilisha miradi ya kielelezo na kimkakati yenye matokeo makubwa ya uchumi linakuja swali, tujiulize, baada ya kuikamilisha nini kinafuata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo ningependa kuiangalia zaidi kwamba baada ya kuikamilisha nini kinafuata? Ni miradi ya bwawa la umeme, vilevile hata usafirishaji kama *SGR*. Tuangalie wenzetu walifanyaje walipokuwa na vitu kama au hali kama ambayo tumekutana nayo hivi sasa? Tuangalie mfano wa Msumbiji.

Mheshiiwa Mwenyekiti, katika mwaka 1979 wenzetu wa Msumbiji walikamilisha Bwawa la Cabora Bassa ambalo lilitoa *Megawatt* 2,075, wao walichokifanya wenzetu walichukua 45% ya umeme wote huo ukaelekezwa katika kiwanda kimoja cha uzalishaji wa *aluminium*, walivyoweza kuzalisha *aluminium* yote katika Kiwanda cha Mozal ambacho kinatoa tani 580,000 za *aluminium* kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini matokeo yake? Wamejikuta kwamba ule umeme wao 90% ya *aluminium* inayozalishwa Msumbiji yote wanapeleka Ulaya. Kwa hiyo, maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba unapata fedha ya kigeni kutokana na mradi wako wa mkakati, lakini vilevile ukiangalia nini

kimetokea baada ya kuweka kiwanda hicho ambacho kinazalisha *aluminium* kwa wingi, kimekuwa ndiyo kiwanda kikuu mwajiri wa nchi hiyo. Kimeweza kuzalisha ajira nyingi, kimeweza kuwapatia fedha za kigeni na kimeweza vilevile kuokoa pesa yao ya kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nini mapendekezo yangu kwa hilo? Mapendekezo yangu ni kwamba katika umeme wetu huu ambao na sisi baada ya kuzalisha umeonekana ni mwingi kuliko mahitaji yetu ya sasa hivi, ina maana tusipange kuuwashia taa tu, tulenge viwanda vya kimkakati. Kwa kusema hivyo tuangalie ni viwanda vipi ambavyo vinaweza kuwa vikatuokoa na sisi kama ambavyo viliwaokoa Msumbiji katika hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jirani yake hapo, kuna siyo machimbo maana hawajaanza kuchimba, kuna akiba kubwa ya chuma katika eneo la Liganga na ukiangalia chuma katika ulimwenguu huu haijawahi kutosheleza. Vilevile chuma katika uchakataji wake upo wa aina mbalimbali. Chuma bora zaidi ni kile ambacho kinachakatwa kwa umeme. Kwa hiyo, tukiweza kupata vile vinu vya awali vya kuchakata chuma ambavyo wanaviita *blast furnished,* lakini baada ya hapo tukawa na vinu vya kuchakata chuma kwa umeme *(electrical furnish)* ambavyo vitaweza kutupatia chuma bora ambacho ndicho kinaweza kikatupatia manufaa ya haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia chuma ambacho kimetumika katika reli ya *SGR,* chote kinatoka Japani kwa sababu ni nchi chache sana ambazo zinatengeneza chuma cha ubora huo, lakini siri ni kwamba wamefanya hivyo kwa sababu wana vinu vya kuchakatia hivyo ambavyo vinahitaji nishati kubwa na sasa nishati kubwa tunayo, hivyo tunaweza kujielekeza huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihamie kwenye sehemu nyingine vilevile ya vifaa vya ujenzi ambavyo ni malighafi ya saruji maarufu kama *clinker*. Ukienda bandarini pale Dar es Salaam au Tanga utagundua kwamba kuna uagizaji mkubwa sana wa hii bidhaa *clinker* kwa ajili ya matumizi yetu ya ndani, na hata kwa matumizi ya nchi za nje vile vile ambao ni jirani zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ina maana kwamba hii ni fursa. Pia ukiangalia nini ambacho kinatuzuia sisi kutengeneza *clinker* hapa nchini kwa wingi? Ni kwa sababu malighafi tunayo, lakini nishati. Sasa suala la nishati ya kutengenezea *clinker* ni gesi na umeme. Tukijikita kuwekeza katika kutengeneza viwanda ambavyo vinaweza vikazalisha *clinker* ambavyo vipo vinavyotengeneza *cement,* vikipewa uwezo au vikirahisishiwa kupata umeme wa bei nafuu, vikirahisishiwa kupata gesi ya bei nafuu, maana yake ni kwamba hii *clinker* ambayo ilikuwa inaagizwa kutoka nje itakuwa sasa inatengenezewa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia hapa, ni wapi tunaagiza *Klinker* kwa takwimu za mwaka 2023 kutoka *UAE* tunaagiza tani milioni 196, kutoka Saudi Arabia, tunaagiza tani 146 kutoka Pakstani, tunaagiza tani 99 kutoka Kenya, tunaagiza tani 19 na kutoka China, tunaagiza tani moja. Sasa zote hizi tunaweza tukazitengeneza hapa nchini kwa kutumia viwanda vyetu na rasilimali yetu wenyewe kwa sababu tunayo; udongo tunao, *limestone* tunayo, chokaa tunayo, kilichokuwa kinapungua ni nishati. Sasa baada ya kukamilisha hivi viwanda vya mkakati maana yake ni kwamba tuvitumie katika kutengeneza viwanda hivi ambavyo vitarahisisha upatikanaji wa malighafi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda zaidi, vilevile nchi hii udongo wa kutosha tunao, tunaweza kabisa kutengeneza vigae vya kwetu wenyewe na matofali ya kuchoma yenye kiwango kikubwa. Matofali ya kuchoma tuliyonayo hivi sasa, hivi viwango vyake ni vidogo lakini tukichoma matofali ya kiwango kikubwa sana, matofali hayo huwa yanakuwa ghali sana maana ndiyo yanayotumika katika kuweka matanuri ya kutengenezea *clinker* na kadhalika, yote yale tunaagiza kutoka nje lakini *material* yote tunayo hapa. Je, hatuwezi kutumia nishati yetu nafuu sasa kutengeneza hayo matofali ambayo tutayatumia wenyewe na kuweza kupeleka nchi za nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatusaidia katika kuongeza ajira, itatusaidia katika kuongeza fedha za kigeni na vilevile itatupunguzia mahitaji yetu ya fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda unanitupa mkono. naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Leonard Chamuriho. Mheshimiwa Cecil David Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, na Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi mchana huu kuchangia kwenye hoja iliyopo mbele yetu ambao ni Mpango wa Taifa wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo matatu kimsingi ambayo ningependa niyachangie leo kwa nia ya kutaka kuboresha mpango wetu. Jambo la kwanza kabisa ni suala la Liganga na Mchuchuma, lakini nataka kusema kuhusiana na reli ya kusini pamoja na reli ya kati kwa maana ya *SGR*. Nitaongea pia kuhusu masuala ya madeni ya wakandarasi kwa nia ya kutaka kuchechemua uchumi wetu, na pia nitatoa ushauri kwenye masuala ya kilimo kwa maana korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi ya peke kabisa, nami niungane na wote waliompongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Rais na kwamba uzalishaji wa korosho umeongezeka sana. Nampongeza pia na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuwapatia pembejeo wananchi wa Mtwara, Lindi, Ruvuma na Mikoa yote inayolima korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongezeka kwa uzalishaji wa korosho hivi sasa tunapitia changamoto kidogo. Changamoto kubwa iliyopo ni suala la usafirishaji. Serikali ilitoa maelekezo kwamba korosho yote inayozalishwa Mikoa ya Mtwara, Lindi na maeneo mengine ikiwezekana isafirishwe kupitia Bandari ya Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ninaongea mbele yako mwaka huu tunategemea tutakusanya zaidi ya tani 400,000; ndiyo maana nilisema ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha kwamba amepeleka pembejeo za kutosha kwa

wakulima wa korosho. Uzalishaji kwa kweli umeongezeka ukilinganisha na miaka yote na kama nilivyosema, ni kazi kubwa pia ya Waziri wa Kilimo na wasimamizi wote wa Sekta ya Kilimo na wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto tuliyo nayo ni ya usafirishaji. Mpaka sasa hivi korosho zilizokusanywa mpaka mnada wa jana na wa leo *MAMCU* ni zaidi ya tani 200,000, zinakaribia kufikia tani 220,000; lakini korosho hizi zinasafirishwa pekee kwa kutumia Bandari ya Mtwara. Tumekusanya kwa kipindi cha zaidi ya mwezi mmoja sasa, lakini korosho ambazo tunategemea kuziondoa karibuni ni tani 400,000 tu kwa kutumia meli iliyoletwa na yenye uwezo wa kubeba makasha 175. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba mwaka jana mwezi Februari walibadilisha maamuzi wakaanza kuisafirisha korosho kutumia Bandari ya Dar es Salaam, na ndipo korosho zile zilikwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wamekuwa wakilalamika kuhusu ughali wa gharama ya kusafirisha kupitia Bandari ya Mtwara. Hivi sasa kontena la futi 40 kutoa Mtwara kwenda India ni kuanzia dola 1,900 mpaka dola 3,300, lakini kontena hilo hilo kulitoa Bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi za India na Vietnam haizidi dola 800 mpaka dola 1,000, zipo hapo *between*. Sasa tazama gharama hizi zilivyo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafute namna ya kufanya ili kuwawezesha wafanyabiashara kupunguza gharama zao za usafirishaji ili iweze kuleta tija kwa mkulima. Kwa hiyo hii ilikuwa sehemu yangu ya ushauri. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri hili alifanyie kazi ili kuweza kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hapa kwamba kuna suala la madeni ya wakandarasi, tumesikiliza vizuri sana kuhusu mpango na hotuba zote zilizopita mbele yetu. Ukiangalia *LAAC* na *PAC* pamoja na ile nyingine, ni kwamba wakandarasi wamekuwa hawalipwi kwa wakati, kitu ambacho kimepunguza sana mzunguko wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi nilipata bahati ya kuuliza na nikamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kwamba ni lini mkandarasi aliyepewa kazi ya kujenga Barabara ya Lindi – Mtwara – Kibiti ataanza kazi? Anasema Serikali ina mpango wa kutaka kujenga barabara hii upya. Hata hivyo kwa hatua za dharura amepatikana mkandarasi ambaye atakwenda kujenga madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumetoka majimboni hivi karibuni tu. Ninataka niseme kwamba mpaka sasa hivi mkandarasi hajafanya *mobilization* na wala hajafika *site,* hivyo, uwezekano wa kuanza kazi hiyo mapema ni mdogo. Kwa hiyo, kuna tishio pia hata kwenye namna ya kusafirisha hizo korosho tunazozitaja hapa kwa sababu barabara ya Mtwara mvua zikianza kunyesha hata wiki moja kuanzia sasa barabara hii itajifunga na kwa hivyo haitaweza tena kupitika, tutalazimika sisi kupita Songea. Hiyo ndiyo hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri apeleke hao wakandarasi, kama anasema Mheshimiwa Rais amekwishatoa fedha basi wapewe *advance* ili wakaanze kazi hii mapema ili kuweza ku-*rescue*. Hali ni mbaya, barabara nzima unaweza ukasema *almost* imekufa. Pamoja na nia njema ya Serikali na kwa sasa ameamua kuanza kutengeneza madaraja, basi kazi hiyo ikafanyike mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la mpango ninataka nishauri, kwamba mpango bora wa nchi yoyote, ambao pia ni kama *manifest,* unakuwa na tarehe mahususi ya ukamilishaji wa miradi ya kimkakati. Mradi wa Liganga na Mchuchuma sasa hivi ni zaidi ya miaka 50 hadi miaka 60. Tangu sisi tukiwa watoto wadogo tunasikia zinaongelewa habari za Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imepigwa hatua kidogo sasa hivi walau wananchi wameanza kulipwa fidia. Tunataka sasa tuone utekelezaji wa mradi huu ili kuweza kutuletea tija. Mheshimiwa Eng. Dkt. Chamuriho hapa alikuwa anaongea na kutoa ushauri kwa Serikali, lakini pia na Mheshimiwa Profesa Manya nilikuwa ninamsikiliza wakati ule na hata ndugu yetu Mheshimiwa Profesa Kaijage, ambaye naye ni Profesa, kwa namna anavyolishauri

Bunge. Tunachotaka kifanyike, cha kwanza, ndiyo, kwamba Serikali ilikuwa na nia njema kabisa ya kutengeneza reli ya kati kwa kiwango cha *SGR.* Awamu ya pili ya reli ilikuwa ni reli ya Kusini inayoanzia Mbamba *Bay* itapita huko Songea itakuja mpaka Mtwara bandarini yenye urefu wa kilomita 1,000; lakini kilichopo mpaka sasa kwa sababu mpango huu hauna tarehe mahususi ya ukamilishaji wa miradi hii kuna wakati mwingine Serikali haitimizi wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kipande cha Tabora – Isaka chenye urefu wa kilomita 165 kimetengenezwa kwa asilimia 6.62 tu. Kipande cha Mwanza – Isaka chenye urefu wa kilomita 341 utekelezaji wake ni 60.62%. Sasa ukija kuangalia hapa sasa hivi kipande kinacholeta tija ni cha Dar es Salaam – Dodoma, tena tija yenyewe ni abiria kwa sababu uzalishaji wa hapa Dodoma wa mazao ya kilimo na mengine si mkubwa kiasi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunashauri Reli ya Kati ikamilike kwa wakati uliokusudiwa; mpango wake uoneshe tarehe mahususi ya kukamilisha Reli ya Kati, mpango wake uoneshe tarehe mahususi ya kuhakikisha ule Mradi wa Liganga na Mchuchuma unaanza kutelezwa, ambao pia utajenga na Reli ya Kusini ili kwenda sawa na lile jambo lililokuwa linaitwa *Mtwara Corridor. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi hakuna mjadala wa *Mtwara Corridor* kwa sababu *components* nyingine za *Mtwara Corridor* hazijatekelezwa. Uchumi wa watu wa Kusini *in a way* umelala. Huwa tunachangamka wakati wa hizi habari za korosho na habari nyingine, lakini kimsingi kuna mambo ambayo Serikali inatakiwa itumie nguvu kubwa kuyatekeleza ili iweze kuleta tija inayokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona sasa hivi; mwanzoni walikuwa wanasema kwamba Mradi wa Liganga na Mchuchuma hauwezi kuanza kwa sababu kulikuwa kuna madini ambayo hayatumiki pale, lakini sasa hivi kuna madini ambayo ni *very rare* yanayotakiwa huko duniani nayo yapo kwenye Mradi huu wa

Liganga na Mchuchuma. Kwa nini, Serikali isianze kuutekeleza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapata wasiwasi kwamba kuna mikono hapa inayozuia utekelezaji wa mradi huu, kwa sababu mkandarasi yupo na mazungumzo yalianza tangu mwaka 2011, lakini mpaka sasa hivi mradi hauendelei na mkandarasi hakuna chochote anachokifanya. Serikali inasema inafanya mazungumzo lakini mazungumzo hayo yanafanyika kwa siri kubwa. Sisi Wabunge tunaotokea kwenye maeneo haya kwa kweli tunasikitika. Tunatamani sana tuone uchumi wetu unakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hili suala la reli wananchi wa maeneo mengi wameshindwa kuendeleza maeneo yao wakiamini utekelezaji wa ujenzi wa Reli ya Kusini utaanza karibuni. Sasa tutoe ruhusa kwa sababu hakuna mpango wa kutekeleza ujenzi wa reli hii *in the near future*. Tunasikia sasa hivi wanataka kuboresha Barabara ya Mtwara – Masasi na anatafutwa mkandarasi. Sisi tulipewa taarifa kwamba barabara hii itaanza kujengwa hivi karibuni ikiwa ni pamoja na kubadilisha taa zilizopo barabarani eneo la Ndanda, Nanganga na maeneo mengine, kwa sababu taa ziliwekwa zikiwa zina mwanga hafifu, ombi ambalo tumekwishalileta Serikalini. Kwa hiyo, tunategemea hivi karibuni mambo haya yote yatafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la msingi kuliko yote, ili kupunguza matumizi makubwa ya *forex* kwenye kuagiza chuma kwenye hivi vipande vilivyoanza, basi tunashauri kabla utekelezaji wa Reli ya Kusini haujaanza kama ambavyo mzee wangu hapa amesema, ikiwezekana tutafute hizo *electrical furnace* kwa sababu tunao umeme wa kutosha. Sisi hatuna haja hivyo vitu wavilete Dar es Salaam. Katika hatua za awali kule kule Songea, kule kule Madaba, kule kule huko Namtumbo na kwingine inawezekana kuweka kiwanda cha kuchenjua chuma hii ili tuanze kujenga Reli yetu ya Kusini kwa kutumia chuma chetu wenyewe kwa gharama nafuu sana tofauti na ambavyo imekuwa *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Reli ya Kusini itaanza kuleta tija mara moja kwa sababu inakwenda kusafirisha makaa ya mawe,

Reli ya Kusini itakwenda kusafirisha na bidhaa nyingine zilizopo eneo lile na kujipatia fedha; si kwa lengo la abiria pekee yake. Kwa hiyo, hilo tuombe na tushauri; na ndipo tutakapokwenda kuonesha ile tija ya *Mtwara Corridor,* lakini na matumizi mazuri ya Bandari ya Mtwara. Siyo kutegemea tu mazao kama korosho na sasa tunaona hapa uzalishaji wa korosho umeongezeka, lakini bandari inashindwa kuhudumia korosho hizi. Ndani ya mwezi mmoja tumeondoa tani 4,000 kati ya tani 2,000 zilizozalishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine la *NLG.* Miaka miwili iliyopita sisi Wabunge wote wa Mikoa ya Mtwara na Lindi tulikuwa tunaimba sana kuhusiana na suala la *NLG* na tuliaminishwa utekelezaji wake utaanza hivi karibuni ili kuweza kusisimua uchumi wa maeneo hayo. Inasikitisha kuona kwamba tulichokuwa tunaambiwa wakati huo na kilichopo sasa hivi *field* si vitu vinavyofanana. Hatufahamu mazungumzo yameishia wapi na mradi huu unaanza kutekelezwa lini. Kwa hiyo, nimwombe atakapokuja ku-*wind up* pamoja na kuwa na *timeframe* na nimshauri kabisa Mheshimiwa Waziri kwamba, katika miradi yote ya kimkakati kuwe kuna *timeframe;* hivi vitu visiwe *infinity,* ni lazima tuseme kufikia tarehe 5 Oktoba, wakati fulani tumalize mazungumzo na mkandarasi ili utekelezaji uanze wakati fulani. Tukiacha tu vikawa vile ambavyo vinafanyika ni ngumu kuvitekeleza na uchumi wetu unazidi kushuka chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niunge mkono kabisa hotuba hii, lakini pamoja na mpango huo bado ninasisitiza kuhusu kuhakikisha kwamba miradi hii mikubwa ya kimkakati anaiwekea *timeframe* ili kuweza kuleta tija kwa nchi yetu. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mwambe. Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, atafuatiwa na Mheshimiwa Reuben Kwagilwa na Mheshimiwa Abdullah Mwinyi, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka

2025/2026 na Mapendekezo ya Mwongozo ya Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nitangulie kuishukuru Serikali na kuipongeza kwa kutuletea mpango mzuri na mapendekezo mazuri kupitia kwa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, Waziri wa Nchi, Mipango na Uwekezaji. Huyu ni rafiki yangu na *schoolmate* wangu wa *high school (Pugu High School)*. Pia, taarifa nzuri imesomwa na mapendekezo kutoka kwa rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, tunapongeza kwa hatua hii ambayo Serikali imetuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ningependa nichangie katika maeneo matatu. Eneo la kwanza ni katika sekta ya utalii; eneo la pili ni miundombinu ya barabara za vijijini; na eneo la tatu nitakwenda kwenye michezo kwa sababu mimi ni mwanamichezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepiga hatua kubwa sana katika sekta ya utalii kutokana na filamu ambayo iliongozwa na Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; na katika miaka ya karibuni tumeshuhudia watalii wakiongezeka na hivyo fedha za kigeni nyingi zikapatikana hadi kufikia 25% ya fedha zote ambazo zimekusanywa katika mwaka 2022/2023 kutokana na sekta hii ya utalii. Watalii wameongezeka hadi kufikia 3,784,254 kwa mwaka 2023/2024. Sasa, kwa mujibu wa mapendekezo yaliyotolewa tuna lengo la kufikisha watalii 5,000,000 ifikapo Mwaka wa Fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba tumekuwa na changamoto nyingi katika sekta hii. Ndiyo maana inatufanya sasa pamoja na kwamba sisi Taifa letu kuwa ni la pili kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii bado hatupo hata kwenye 10 bora katika kuingiza fedha nyingi za utalii hapa duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nipende kwanza niainishe changamoto ambazo zinakabili sekta hii, ambazo ni ubovu na ukosefu wa miundombinu ya kuweza kuvifikia vivutio hivi, hasa kwenye hifadhi zetu pamoja na mapori yetu ya akiba.

Pia, kuna bajeti ndogo ya kutangaza vivutio hivi ndani na nje ya nchi yetu; vilevile kuna changamoto katika ubunifu wa vyanzo vipya hata vile ambavyo vinaonekana kabisa bado hatujaweza kuviingiza katika mtiririko wetu kuvifanya viweze kujulikana, lakini pia viweze kutumika katika kutuingizia fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto ya huduma ya utafiti. Mara nyingi tumekuwa tukitegemea watafiti kutoka nje ya nchi pale wanapoguswa na mambo mbalimbali na wakati mwingine taasisi ambazo zinahusika na shughuli za utafiti kama *Tanzania Board of Tourism* ambayo hata hivyo imekuwa ikipewa mtaji mdogo sana kwa ajili ya kufanya kazi hii na wakati mwingine hata wataalam wamekuwa wakikosekana. Mfano, halisi ni kule katika ule mji uliozama wa Rhapta ambao ulishamiri kuanzia Karne ya Saba kabla Kristo mpaka Karne ya Nane baada ya Kristo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufuatilia nimegundua kwamba kuna Profesa mmoja anafanya kazi kule ya kuendesha utafiti, lakini anadhaminiwa na taasisi mbalimbali za nje. Sisi kama Watanzania hatuwekezi vya kutosha; lakini hata wataalam anaowatumia walio wengi wanatoka nje ya nchi. Ile kazi, kwa sababu ule mji ulizama na ulitafutwa kwa miaka mingi watu wa Ulaya waliandika maandiko mengi kuutafuta ule mji. Unakuta wale *diving archeologists* wengi wanatoka nje ya nchi, lakini sisi hatuna hata mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba Serikali iliangalie katika mpango huu itenge bajeti kwa ajili ya utafiti, lakini pia kwa ajili ya kuwaendeleza wataalam hasa katika zile fani ambazo hatuna watalaam, lakini ambazo ni za muhimu ambazo zitatuletea hawa watalii. Kama watu wameandika maandiko mengi kuanzia karne iliyopita hadi karne hii kule Ulaya ni wazi kabisa kugundulika kwa Rhapta kuanzia miaka hii ya 2000 ni kwamba kutaleta watalii wengi, kama ambavyo watu walikuwa na hamu ya kujua hii Rhapta ilipotelea wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kusema kwamba kuna kumbukizi za kihistoria na kiutamaduni zilizopo Kilwa Kisiwani. Kwa hakika Tanzania tumejaliwa kwa kiasi kikubwa sana kuwa na

kumbukizi za utamaduni na kihistoria *(historical and cultural tourism),* lakini nazo bado hazijaendelezwa kwa kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali yetu kwa kuziona kumbukizi zilizopo Kilwa Kisiwani, vilevile imeziona kumbukizi kama zile zilizopo katika Milima ya Umatumbi, Kumbukizi za Majimaji ambazo zimepata *GN* mwezi Machi mwaka huu, pia mapango kupitia *GN* namba 163 na 166, likiwemo pango refu kuliko yote. Serikali imewekeza kiasi cha kutosha na inajenga jumba la makumbusho kule na pia inakwenda kutengeneza ngazi za kushukia kwenye lile pango kubwa kuliko yote katika ukanda wetu huu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye Dola ya Kilwa katika Karne ya 11 hadi 15 ambayo ilishuhudia maendeleo makubwa na hata kuwavutia watalii tangu Karne ya 13. Mtalii wa kwanza maarufu kuja Kilwa Kisiwani alikuwa ni Ibn Battuta katika mwaka 1331 na alishuhudia mambo mengi ya kistaarabu yakiwa yamefanyika katika Dola ya Kilwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na fedha zinatengenezwa Kilwa, ambayo ndiyo sehemu ya kwanza kutengenezwa fedha za sarafu ambazo tunaziona leo. Pia, kulikuwa na msikiti mkubwa, wanaita Msikiti Mkuu wa Karne ya 11. Ule msikiti ilikuwa watu kutoka Rwanda, Burundi na Kongo wasiokuwa na uwezo wa kwenda *Macca* na *Madina* walikuwa wanakuja kuhiji pale. Tunazishukuru Serikali ya ufaransa kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania waliweza kuufukua kwa sababu ulikuwa unaelekea kuzama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kule Kilwa pembezoni ya ule Msikiti wa Ijumaa au Msikiti Mkuu kuna sehemu ambayo Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikwenda kupata baraka kule wakati anapigania uhuru mwaka 1958; na alifikia kwenye nyumba inayojulikana kama nyumba ya buluu *(blue house)*. Ile nyumba ipo hadi leo. Alikuwepo mzee mmoja ambaye alishikilia karabai usiku ule wakati wale wazee wakiwa wanampa baraka yule mzee akiwa ameongozana na mzee wetu mwingine shujaa Mzee Kawawa, mama Bibi Titi Mohamed pamoja na Mzee Oscar Kambona na wengine kama akina Lau

Nagwanda Sijaona. Ile nyumba imetelekezwa mpaka leo, haijapewa uzito unaostahili Kilwa Kisiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nyumba pia ambayo katika kumbukizi nilimsikia Shekhe Mkuu wa BAKWATA na Mufti wa Tanzania Shekhe Abubakar Zubeir Ally Mbwana katika mazungumzo yake wakati fulani akielezea historia ya Uislamu katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliitaja Kilwa kama ndiyo sehemu ya kwanza ambayo watu wake ama Waislam wake wa kwanza kwenda kuhiji Madina. Walikwenda kundi la kwanza katika Karne ya Sita na walimkuta Mtume Muhammad *(Swallallahu Alayh Wasallam)* akiwa hai. Wale Waislamu wa Kilwa walipoona kwamba Waislamu wenzao hawakurudi, kundi la pili ilikwenda tena katika Karne ya Sita na lilikuta Mtume Muhammad akiwa amekwishafariki wiki mbili zilizotanguliwa. Hii ni simulizi ya kweli ambayo Shekhe Mkuu wa BAKWATA aliye hai leo alisimulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo tunaona kwamba wale Waislamu walipotoka kule walirudi na Quran ya kwanza Afrika Mashariki; kuna nyumba pale ipo ambayo Quran ya kwanza ilifikia, ni pale, siyo sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna sehemu inaitwa Nguruni, sehemu ambayo tunashukia ukitoka huku upande wa Bara ya Kilwa Masoko kuna sehemu ambayo kuna gati ya kushukia. Pale ndiyo fedha ya Kilwa ilikuwa inatengenezwa, lakini hakuna kumbukumbu zozote katika maeneo hayo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali iangalie na ikiwezekana iwekeze katika *museum* inayohusika na utamaduni wa watu wa Kilwa ambao unaenda sambamba na utamaduni wa dini ya kiislam. Haya mambo ya kuwa na *museum* hizi ambazo zinaendana na utamaduni wa kidini zipo. Ukienda Ethiopia unazikuta, ukienda Ephesus unazikuta, ukienda Makka na Madina unazikuta, ukienda Jerusalemu unazikuta, ukienda Thessaloniki unazikuta na ukienda Galathia unazikuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo zinaingiza fedha nyingi kwa wale wenzetu. Kwa hiyo hata sisi tukiwekeza katika eneo hili, basi fedha nyingi itaingia kupitia utalii wa kihistoria na kiutamaduni. Suala la pili ni kuhusiana na suala la michezo. Mheshimiwa Waziri…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa muda wako umekwisha tafadhali.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika mbili.

**MWENYEKITI:** Naomba hitimisha tuna changamoto ya muda.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ya bajeti alihitimisha kwa kusema kwamba atafanya jitihada za kuweka *VAR* katika mashindano ya ligi yetu kuu hapa nchini Tanzania. Tumeshuhudia mambo mengi ya hovyo yakifanywa na waamuzi wetu katika ligi kuu ya Tanzania bara. Mfano mzuri ni mechi ya tarehe 19 mwezi uliopita ulishuhudia mwenyewe Mheshimiwa Waziri, lakini tunamshukuru Waziri…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda umekwisha tafadhali.

**MHE. FRANSIC K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Reuben atafuatiwa na Mheshimiwa Abdullah Mwinyi na kama muda utaruhusu Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja mbili zilizoletwa na Serikali, lakini vilevile na taarifa yetu ya Kamati ya Bajeti ambayo imewasilishwa na Mwenyekiti wetu kwa ustadi mkubwa sana Mheshimiwa Mzee Oran Njeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/2026 pamoja na mambo mengine, taarifa hizi mbili zimetoa vipaumbele mahususi 10. Vipaumbele hivi vimejaribu kuonesha namna ambavyo tunakwenda kushughulika na uwekezaji kwenye sekta za uzalishaji. Katika hivi vipaumbele mahususi 10, ninataka nizungumzie kipaumbele kimoja tu, kuongeza wigo wa kinga ya jamii ambapo kimsingi mpango unalenga kuongelea bima ya afya kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechagua kuongelea kipengele hiki kimoja au kipaumbele hiki kimoja mahususi kwa sababu bima ya afya kwa wote inakwenda kumgusa kila Mtanzania kwa maana ya kwenda kuleta ustawi wa jamii. Vilevile, bima hii ya afya kwa wote inakwenda kuliingiza Taifa kwenye historia ya kila Mtanzania kupata huduma ya afya katika mazingira yanayofanana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa tunaongelea bima ya afya kwa wote na kwa maana tunaongelea kipaumbele hiki cha kinga, kuongeza wigo wa kinga ya jamii nataka tutazamie maeneo machache ya eneo la afya ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya yakiwa kama sehemu na tunayahesabu kama sehemu ya maandalizi ya mpango huu wa bima ya afya kwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa tuna vituo vya kutolea huduma za afya 12,266. Katika hivyo, vituo vipya ni 1,324. Kazi kubwa sana hii imefanyika. Hivi sasa ninavyozungumza tukielekea kwenye huu mpango wa kuandaa bima ya afya kwa wote, nchi yetu ina *digital X-ray* 346, ina *ultrasound* 677, ina *CT scan* 34 (zote hizi ni kazi za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan) na *MRI* za kutosha kulingana na kanda tulizonazo. Vilevile, Serikali imetoa mtaji wa karibia shilingi bilioni 100 kwa *MSD* ili kuweza kununua madawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya ni sehemu ya maandalizi ya kuelekea mpango wa bima ya afya kwa wote. Vilevile, Mheshimiwa Rais mwaka jana alitoa kibali cha ajira cha

kuajiri watumishi 13,187 wakiwemo watu wa Sekta hii ya Afya. Vilevile, Serikali inasomesha wataalam ndani ya vyuo vyetu, wataalam bingwa nje ya nchi wapatao 1,251; mradi ambao unatugharimu shilingi bilioni tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi, ikiwa tunataka kwenye mpango wetu huu wa mwakani kujiandaa na jambo hili kubwa la bima ya afya kwa wote, mambo yafuatayo ni muhimu tuyafanye:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, tupitie upya vyanzo vya mapato kwa ajili ya bima ya afya kwa wote. Mwaka jana kwenye *finance bill* tulipitisha vyanzo viwili. Kwanza tulipitisha 100% kwenye ushuru wa *ethyl* na tulipitisha asilimia mbili kwenye ushuru wa bidhaa za pombe, bidhaa za *cosmetics* pamoja na bidhaa nyingine. Mpaka sasa kwenye vyanzo hivi viwili tulivyopitisha tumekusanya shilingi bilioni 22 peke yake kwenye lengo la kukusanya karibu shilingi bilioni 173 kwenye vyanzo hivi viwili. Hii inatu-*alarm* kwamba ni muhimu tukafanya tena tathmini na kuendelea kutafuta vyanzo vingine vipya kwa ajili ya mpango huu kabla hatujaanza kuutekeleza 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo tunatakiwa kufanya ni kuanzisha kwa mfuko wa kugharamia wasio na uwezo pamoja na wanawake wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano, tuanzishe Mfuko. Ni muhimu sana kuanzisha mfuko hivi sasa kabla ya 2026 kwa sababu, fedha ikiwa Mfuko Mkuu wa Serikali haina rangi. Hamna iliyochorwa kwamba hii ni ya bima ya afya kwa wote. Hata hivi sasa tunavyozungumza ni hatari sana kuwa shilingi bilioni 22 zimekaa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na namwomba Mungu kwamba ziwepo kwamba zipo. Ni muhimu tuanzishe Mfuko ili fedha hizi ziende ziwekwe kule badala ya kukaa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali; ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, sheria ile tuliyoipitisha tulisema Waziri wa Sekta kwa maana ya Waziri wa Afya pamoja na Waziri wa Fedha waweke utaratibu wa namna ya kusimamia Mfuko huo. Kwa sababu, kimsingi fedha hizi kama hatuzitumii hivi sasa *as long as* tunataka kuzitumia kwa ajili ya bima ya afya kwa wote ni lazima ziwekezwe na sio kuwekwa; zinatakiwa

kuwekezwa. Sasa kama hatujawa na hiyo *structure* kamili ambayo ndiyo tafsiri ya sheria ya bima ya afya tuliyonayo, fedha hizi tutakuta tumezitumia kwenye mambo mengine na hii itakuwa ni jambo baya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ambalo lazima tulifanye, kanuni za sheria ile tuliyotunga mwaka 2023 (Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote), si tu kwamba ziwe tayari, lakini zifahamike na kila Mtanzania tukiwemo sisi Wabunge, zifahamike na kila mwajiri, zifahamike na kila mwajiriwa, zifahamike na kila mwananchi. Ndugu zangu, jambo hili la bima ya afya kwa wote, duniani kote wakati wa kuanza limeleta rabsharabsha na purukushani nyingi sana. Mataifa makubwa walivyojaribu hivyo walipata purukushani kubwa sana. Bahati tuliyonayo ni kwamba tumepitisha sheria mapema mwaka 2023, tuitumie muda huu kufika 2026 tuwe tumejipanga kuandaa *structure* na haya mambo ninayoyashauri pamoja na mambo ambayo Serikali inayafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa nchi ya jirani hapa, sitaki kuwataja, mnajua kinachoendelea pale kuhusu bima ya afya kwa wote. Kwa hiyo sisi tutumie muda huu kwamba tumepitisha sheria mapema, tuziandae *structures* zote mapema zikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo tutapaswa kulifanya ni elimu. Wananchi wetu wanapaswa waelimishwe kwa sababu tukishatoka kwenye haya makundi maalum ambayo tumeyalenga: wanawake wajawazito, watoto wenye umri chini ya miaka mitano, watu wasiojiweza; kitakachofuata baadaye ni kuwa-*take on board* wananchi wote na yapo mambo pale ambayo wananchi kwa upande wao watatakiwa wayafanye. Kwa hiyo ni vizuri elimu wakaanza kuipata sasa kabla ya 2026; hali kadhalika elimu iwafikie waajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la muhimu kufanya, tumekubaliana kwa pamoja mtekelezaji wa jambo hili atakuwa ni *NHIF*. Ninatambua hoja zote za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu *NHIF* zilishakuwa *cleared*. Kwa hiyo udhaifu ule ni kama haupo tena. Kwa hiyo tunatarajia sasa, kuelekea bima ya

afya kwa wote, *NHIF* itakuwa imejipanga. Katika kujipanga kwao wahakikishe wanakuwa na ofisi kwenye kila wilaya ya nchi hii, ikiwezekana kila halmashauri ya nchi hii…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante naomba Mheshimiwa hitimisha, ahsante tunakushukuru.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nihitimishe hoja ya mwisho kwamba, zoezi la utambuzi tusitegemee tu zile takwimu za *TASAF* kwenye kutambua watu wasiokuwa na uwezo kwenye kupata bima ya afya kwa wote. Lazima tushirikishe mamlaka nyingine kama Serikali za Mitaa, tushirikishe viongozi pale kwenye *grassroot*.

**MWENYEKITI:** Ahsante muda umekwisha.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdullah Mwinyi.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia huu wasaa wa kuchangia katika mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo lazima yawe maendeleo ya watu (*people centered)*. Maendeleo ya vitu ni njia tu ya kutufikisha kule kwenye maendeleo ya watu. *Infrastructure;* barabara, umeme, maji, elimu, vyote vile ni njia ya kupeleka maendeleo kwa watu *(people centered development)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa huu ni mpango wa mwisho wa miaka 25 ni vyema tu tukaanza tukaangaza macho kama kweli tumepata *people centered development* katika hii miaka 25. Kwa hakika maendeleo makubwa yamepatikana. Ukiangalia kipato cha kila Mtanzania kimepanda mara dufu kwa kipindi hichi cha miaka 25. Ukiangalia kwenye afya (*infant mortality)* vile vichanga vilivyokuwa vinakufa kwa idadi kubwa

sasa hivi vimepungua. Ukiangalia kwenye elimu, ukaangalia idadi ya watu ambao wamekwenda shule *(access)* kwa idadi ya namba na idadi ya *percentage* imekuwa mara dufu. Ukiangalia *life expectancy,* Mtanzania anatarajiwa kuishi kwa umri gani, umri umepanda mara dufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika haya maendeleo na mpaka hapa tulipofika tumepata manufaa makubwa. Ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba maendeleo yajayo yatakuwa makubwa zaidi na yatakuwa kwa haraka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo ningependa kuzungumzia mambo matatu: Elimu, mradi mkubwa wa kimkakati wa *LNG* na kama nitapata fursa nizungumzie ajira kama *strategic bottleneck* ya maendeleo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni mambo matatu. Elimu ni *access*, elimu ni *quality*, elimu ni *relevancy*. Mambo matatu, *access*; Watanzania wangapi wana fursa ya kwenda shule? Elimu la pili; *quality*. Elimu yetu ina kiwango gani? Suala la tatu, *relevance*. Katika ulimwengu huu tuliokuwa nao, elimu ile inatusaidia vipi? *Is it relevant* kwa leo? Sasa kwa hakika *access* kuhakikisha wanafunzi wetu wanakwenda mashuleni tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali limebakia hapa kwenye *quality* na kwenye *relevance*. Kwenye *quality*; ulimwengu wa sasa elimu ya chuo kikuu haina umuhimu mkubwa sana kwenye ajira. Makampuni yote makubwa unayoyajua ulimwenguni wala hawatazami kama umekwenda chuo kikuu au la. Wewe kama una *degree*, kama una *masters*, kama una *PhD* na mwenzio aliyemaliza *form six;* yule kijana wa *form six* anaweza akapata kazi kabla yako. Hizo kampuni za *google*, *Microsoft*, *apple;* ile *fortune 500* ya Marekani, *degree* yako si muhimu sana. Kama unayo unaweza ukaingia *intern* kama mwenzako aliyemaliza *form five* na *form six. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo nini kitu cha muhimu? Kitu cha muhimu ni *skills*. Skills tunazipata wapi? Katika ulimwengu wa leo *university* zote kubwa unazozijua hapo zinatoa

kozi kwenye *internet* bure, tena kozi za elimu na *study* za leo *(data scientist, coding)* bure. *Ivy League University,* wewe ukiwa na *bundle* yako unaweza ukaingia kijana wako akajifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini naligusia hilo? Naligusia hilo kwa sababu moja ya msingi katika mitaala yetu ya elimu. Ni muhimu sana vijana wetu waweze kuzungumza na kufahamu Kiingereza vizuri. Kiswahili lugha yetu, Kiswahili tukienzi, lakini ili tusome tupate *skills,* lugha ya *internet*, lugha ya hizi kozi za kiulimwengu bure ni lugha ya Kiingereza. Ndiyo hoja niliyokuwa nazungumza ya tatu *(relevance)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *emphasis* yetu katika elimu lazima tufikirie hayo mambo matatu: la kwanza *access, la pili quality, quality* ya namna gani? Kulingana na ulimwengu wetu wa leo. Tatu, *relevance*; ndio haya. Tusifikirie maisha yana-*revolve* ndani ya nchi yetu; ajira ni *global*, ajira ni ya kimataifa leo hii. Lazima tuhakikishe Watanzania na vijana wetu wa Tanzania wanazungumza kwa umahiri angalau lugha mbili *(bilingualism),* Kiingereza na Kiswahili. *(Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kimkakati tumeifanya mingi na *impact* yake ni kubwa sana, lakini mradi mkubwa zaidi mara dufu kushinda yote kabisa ni Mradi wa *LNG* ambao mpaka sasa hivi unasuasua. Mradi wa *LNG* kwa muhtasari, tuyazungumze tu. Hakuna mradi ndani ya Bara la Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara wenye ukubwa kama mradi huu wa *LNG*, utaongoza tukiweza kuukamilisha. Watanzania kwa kawaida yetu, mradi wowote ule, mabadiliko ya aina yoyote ya kiuchumi lazima maneno yawepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuwasihi Serikali yangu sikivu kuhakikisha mradi huu mazungumzo yanakamilishwa na unaanza. Hivi karibuni tumezungumza sana kuhusu dira na kwa miaka 25 iliyopita, uchumi wetu wa Tanzania umekua kwa kiwango cha asilimia sita mpaka saba. Wataalam wetu hapa wakasema, ili tufike kule tunakotaka kufika lazima kitokee kitu ambacho kinaweza kukuza uchumi *into double digits,* yaani 8,9,10 na kuendelea. Mwarobaini wa hilo ni *LNG*. *(Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *LNG* ukianza hapa Tanzania, ule mwaka wa kwanza *directly* kuingia katika Serikali ni dola bilioni saba kila mwaka. Hatujapata hiyo *double digit growth* tukiweza kukamilisha hilo? Sasa kwa hakika kabisa ningependa Serikali yangu kuweka mkazo na kuweka fikra zake zote kuhakikisha makubaliano yanakamilika. Kwa mfano maneno mengi, tatizo la *LNG* tofauti na wote tulivyokuwa tunafikiria (namalizia), kwamba, maliasili unaweza ukaitoa tu ardhini wakati wote, sio kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya leo mambo yanabadilika. Kuna teknolojia ambazo zinaweza kufanya kilichokuwa ardhini hakina thamani tena. Sasa muda unakwenda, kuna *renewable energy* ambazo zinatumika kwa kasi juu kubwa sana. Kuna *technology* inaweza ikafanya yale yaliyokuwa ardhini hayana thamani tukashindwa ku-*access.* Sasa tufanye haraka sana ili mradi huu wa *LNG* ukamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdullah Mwinyi.

Waheshimiwa Wabunge naomba turidhike kwamba mchana tutaendelea na uchangiaji na tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya na nitawasoma watano wengine ambao watachangia mchana kwa kuanzia. Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mheshimiwa Zaytun Seif Swai na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje. Wengine watasomwa muda ukifika.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Bunge linarudia

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nasitisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.01 Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## KAMATI YA MIPANGO

**MWENYEKITI:** Kamati ya Mipango.

Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

### Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**na**

### Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, anafuatia Mheshimiwa Shally Josepha Raymond na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru sana wewe kwa kunipa hii nafasi ya kuchangia kwenye hoja ambayo iko mbele yetu, lakini ninachukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, pia ninamshukuru sana na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wetu wa Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila na Dkt. Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuleta hizi hoja mbili hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nina mambo mawili ambayo ninapenda kuchangia leo; la kwanza ni kuhusu vipaumbele vya mpango wa Serikali kwa mwaka ujao wa fedha. Pili, ninachangia vyanzo vya mapato kwa ajili ya huu Mpango wa Serikali ambao ninaenda kuchangia leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri alianzisha *guiding principles* ambazo zita-*guide* utekelezaji wa huu mpango. Sasa nami nataka nimwongezee baadhi ya *guiding principles* na ninamwongezea hizi *guiding principles* kwa sababu huu mpango wetu ni wa mwaka mmoja. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na *guiding principles* ambazo ni za *short run* za mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni lazima tuje na mipango ambayo ni hai *impact intervention*. Mipango ambayo ndani ya mwaka mmoja itatuonesha matokeo fulani, kwa hiyo, hiyo ni mojawapo ya *guiding principle* Mheshimiwa Waziri, ambayo unahitaji kwenda nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hatuhitaji ku-*spread thinly*; ku-*spread thinly* ni kwamba tunaenda na vitu vingi, vyote tunataka tuvifanye kwa wakati mmoja. Lazima tuwe *very focused* kwa sababu tunaenda kutengeneza mpango wa mwaka mmoja. Kwa hiyo, tuangalie vile vipaumbele ambavyo tunaweza tukavifanya, *don't spread too thinly. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni *issue* ya *convergence programing*, tunapopeleka mradi fulani, *let say* wa kujenga shule.

Tunategemea watu wa *TANESCO* waende, watu wa *RUWASA* waende, na watu wa kupima ardhi waende. Sasa hili limekuwa tatizo kwenye miradi ya Serikali. Unakuta mtu anapeleka kiwanda halafu umeme haujafika, barabara haijafika na maji hayajafika. Sasa hili ni tatizo. Kwa hiyo, mojawapo ya *principle* ambayo Mheshimiwa Waziri, unatakiwa ui-*integrate* kwenye mpango wako ni kwamba, kama umepanga kupeleka kiwanda sehemu fulani, hakikisha kwamba umeme na maji vitaenda na ardhi vilevile itapimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, *principle* ya mwisho kama nilivyosema, huu ni mradi wa mwaka mmoja. Lazima tutumie *short run strategy,* kwa sababu ni muda mfupi wa mwaka mmoja na tunaleta mpango wa kufanya ndani ya mwaka mmoja, hata mikakati yetu lazima iwe *confined within one year*. Kwa hiyo, nimesema nimwongezee Mheshimiwa Waziri kwa sababu alikuja na zile *principles* ambazo zita-*guide* huu mpango wake, nikasema nimwongezee hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa la pili ni kuhusu vipaumbele, wenzangu wameongea hapa, tunaenda kutengeneza mpango wa mwaka mmoja. Kimsingi kuna mambo ambayo yamekuwa yakifanyika na Serikali, tunahitaji kuyaendeleza lakini kuna mambo mengine mapya tunaweza tukayaibua kwa ajili ya kutekelezwa ndani ya mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nami ninaomba nieleze maeneo machache; la kwanza ni *SGR*, wote ni mashahidi na wenzangu wamesema hapa. Tumeshaona *impact* ya *SGR*, nimeona Mheshimiwa Waziri ametoa *data* kwamba, idadi ya watu waliosafiri kwa *SGR* imeongezeka na mapato yameongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi bado haujakamilika, ni eneo ambalo Serikali inahitaji kwenda kuwekeza. Katika mwaka huu mmoja, tunataka tuone sasa *milestone* kwamba *SGR* imeishia Dodoma. Je, ndani ya huu mwaka mmoja, *SGR* itaishia wapi? Ndiyo kitu ambacho nilikuwa nasema, *high impact intervention,* lazima tuwe *very focused*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Niseme, hii nchi yetu kama tunataka kuikomboa kwa wakulima, lazima wakulima wetu wawe na uwezo wa kulima mara nne kwa mwaka. Kama wananchi, wakulima wasipoweza kulima mara nne kwa mwaka, kwa kweli Mheshimiwa Waziri tutakuwa tunaidanganya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Mheshimiwa Bashe sasa hivi amekuja na *slogan* yake ya kuwekeza kwenye umwagiliaji. Kwa hiyo, moja ya vipaumbele ambavyo unatakiwa uende nacho, ni kwamba unahitaji kuhakikisha ile miradi ya umwagiliaji ambayo ameanzisha iende sasa kuanza kutekelezwa na ile ambayo ilikuwa kwenye *terminal stage* ikalete *impact* na ndiyo maana yangu ya *high impact intervention*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kuona miradi ya umwagiliaji ina *impact*, watu walime kwa mwaka mara nne ili hata inapotokea kuna *drought,* basi ile miradi ya umwagiliaji inaweza ika-*feed* eneo kubwa la Tanzania. Kwa hiyo, hilo lilikuwa ni eneo la pili ambalo nimependa kueleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni lazima tujibu hoja za wananchi na tujue kero kubwa za wananchi ni nini? Kero kubwa za wananchi ni maji vijijini; watu wana shida ya maji. Sasa ndani ya huu mwaka mmoja, tunaendaje kutatua kero ya maji vijijini? Kuna visima vilichimbwa, havijafanyiwa *installation* na *distribution*. Kwa hiyo, lazima tuangalie ni visima vingapi vimechimbwa hatujafanya *distribution*, usambazaji haujafanyika. Huko ndiyo tukajikite na ndiyo maana yangu ya *high impact intervention*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu maboma; wananchi wamejitolea sana kujenga maboma ya zahanati, madarasa na maboma ya ofisi za vijiji. Hili ni eneo ambalo ni kero kwa wananchi lakini ni hitaji kwa wananchi. Kwa hiyo, katika huu mpango wako Mheshimiwa Waziri, nategemea kuona sasa kwamba, ndani ya huu mwaka mmoja tutajibu zile kero za wananchi ambazo tukienda kwenye mikutano wanasema, lini mtakamilisha boma letu la zahanati na maboma yetu ya madarasa? Tujikite ndani ya huu mwaka mmoja tukamilishe yale

maboma ambayo tumewaambia wananchi, mkijenga maboma Serikali inakuja kumalizia. Kwa hiyo, hili ni eneo mojawapo ambalo nimeona nishauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kuna vituo vya afya vilipewa fedha, milioni 500, kwanza, ninashukuru Serikali, lakini ukiangalia vile vituo, kuna *services* hazijakamilika, hazina *OPD* na hazina wodi. Sasa tunaendaje mwaka unaokuja kwenda kujenga vituo vya afya vipya wakati kuna vituo vipo ambavyo vimejengwa, lakini kuna *services* zingine hazitolewi. Kwa hiyo, nilitegemea kwenye hili sasa Mheshimiwa Waziri aje na programu ambayo sasa tunaenda kuhakikisha kwamba tunakamilisha vile vituo ambavyo tayari vimeshaanza kufanya kazi na vimeshaonesha matokeo. Tuwajengee wodi na tukamilishe zile *OPD* ambazo hazipo, kwa hiyo, hilo ni eneo mojawapo ambalo nilitaka kushauri vilevile tulifanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la barabara na madaraja. Wote ni mashahidi, kuna madaraja ya kimkakati na kuna barabara za kimkakati. Kuna barabara ambazo ni kiungo kati ya wakulima, viwanda na walaji; Kuna madaraja ambayo ni viungo. Haya ndiyo maeneo ambayo ni *high impact* na tukienda kuyawekeza tutaona hata *celebration* ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri anahitaji sasa kuyaingiza, kule kwangu nina Daraja la Sanza, Mheshimiwa Waziri analijua ambalo kimsingi lina-*connect* halmashauri nne na lina-*connect* mikoa miwili. Sasa tunaacha madaraja ambayo ni ya kimkakati, tunaenda kuwekeza kwenye madaraja ambayo hayana *impact*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nami ninashauri, kwenye huu mpango wa mwaka mmoja, kuna madaraja ambayo tayari wakandarasi wamepatikana. Kwa nini tusiende kuwekeza kwenye yale madaraja? Wapewe mikataba waanze kufanya kazi? Pia, kuna madaraja yameshaanza kujengwa na kuna barabara zimeshaanza kujengwa. Kwa nini tusiende kuwekeza kwenye zile barabara ambazo wakandarasi wameanza kujenga, wanadai, wakamilishe, hiyo ndiyo *essence ya high impact intervention*.

Tunataka kuona matokeo ndani ya huu mwaka mmoja kulingana na zile fedha ambazo tunapeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la *industrial parts*, viwanda vyote vime-*concentrate on eastern zone*, Pwani, Tanga na Mtwara. Viwanda vichache sana vipo Kanda ya Kati, Kanda ya Kusini na kwingine. Sasa tunapotaka kufanya *distribution* ya *resources*, kutengeneza ajira lazima kuwe na *even distribution* ya hizi *investment*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu, katika huu mwaka ambao wanaenda kufanya, nashauri watengeneze *master plan* ya ku-*distribute* hivyo viwanda vikae kwenye *zones*, watengeneze *zones* za viwanda. Viwanda visi-*concentrate* katika eneo moja, viwanda ku-*concentrate* eneo moja ni kukosesha fursa baadhi ya maeneo. Kwa hiyo, hilo ni eneo ambalo nami ninashauri walifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la vyanzo vya mapato, hizi kelele zote tunazopiga, kama hatuna fedha *is the wastage*. Kwa hiyo, lazima tushauri Serikali ni jinsi gani tunaweza kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, tuna sekta isiyo rasmi kubwa sana ambayo haichangii kwenye mapato, ambayo tunaiita *informal sector*. Ninashauri Wizara ya Mipango waje na mkakati kwanza wa utambuzi wa hii sekta, wawatambue walioko kwenye hii sekta, watengeneze *register,* waangalie mfumo mzuri, wanawezaje kuchangia kwenye pato la Taifa. Kwa sababu kinachotokea, wanasumbuliwasumbuliwa tu; leo wakimbizwe huku, kumbe tunaweza tukaja na mpango mzuri wa kuwa-*identify*, tukawawekea sehemu fulani wakachangia na inawezekana ikawa na *impact* kubwa sana. Kwa hiyo, hili ni eneo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni suala la kubana matumizi, nami ninashauri, katika huu mpango tunaoenda kuutengeneza, Serikali itarudi kubana matumizi. Hususani kwenye masuala ya usafiri; kwa mfano, kuna haja gani sasa hivi magari ya Serikali yakatumia mafuta wakati kuna gesi? Kwa mfano, sasa hivi

tuna *SGR*, kuna haja gani sasa hivi watumishi kutoka Dar es Salaam wanatumia mabasi kuja Dodoma, wakati tuna *SGR* wanaweza wakapanda pale, wakakuta magari yapo huku Dodoma. Kwa hiyo, hayo ni maeneo ambayo ninashauri Serikali vilevile iweze kuangalia katika kuyashughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, upande wa ardhi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha, tafadhali.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaendelea kuishukuru Serikali na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Chaya. Nilimwita Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, simwoni, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninakushukuru na ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai. Kama siku nyingine, ninashukuru kwa Mwenyezi Mungu kunipa nafasi hii nami kuweza kuchangia chochote katika mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninatoka kidogo, siyo mbali sana na walivyochangia wenzangu, lakini ni kwa sababu ya kujenga. Kama tunavyojua sote tunajenga nyumba hii, hatuna sababu ya kugombea fito.

**MWENYEKITI:** Samahani, Mheshimiwa Mchungahela, baada ya Mheshimiwa Mchungahela atafuata Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Zaytun Seif Swai ajiandae. Mheshimiwa, ninaomba uendelee.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ninavyozungumza, kwamba nitajaribu kuchangia kwa

lengo la kutengeneza mtangamano wa mpango huu, kwa sababu huu mpango ndiyo msingi mkubwa wa bajeti yetu inayokuja hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona mgonjwa anaendelea kuumwa licha ya kuwa amepewa dawa, tafsiri yake ni nini? Kwamba, dawa aliyopewa siyo sahihi, lakini hii inaashiria nini? Kuna mambo mawili yanaweza yakajitokeza hapo. Jambo la kwanza, inawezekana maabara haijafanya uchunguzi sahihi wa changamoto ya mgonjwa, pia inaweza ikawa daktari ameshindwa kupata tafsiri sahihi ya ripoti ya maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kesi yetu sisi hapa, ni moja kwa moja kwamba, maabara imeshindwa kutoa majibu sahihi ya tatizo la mgonjwa. Kwa nini? Kwa sababu, daktari wetu sisi ni mahiri sana, Daktari wetu kwa maana ya Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mahiri. Amefanya jitihada nyingi za kutaka kutibu mgonjwa huyu kwa kwenda huku na huku akijaribu kutafuta jinsi gani ya kumtibu. Ni vema kwamba tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa lakini bado pia tunahitaji kufanya zaidi kwa sababu tumechelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya fununu ya kushuka kwa mfumko wa bei, lakini bado taarifa hizi zimekuwa siyo njema au hazina tija katika uchumi wetu. Bado kumekuwa na changamoto ya shilingi yetu kuwa dhaifu dhidi ya pesa za kigeni na hali hii inasababisha deni letu la Serikali kuongezeka kwa kasi siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kuwa, tumekuwa na mkakati mzuri sana wa kukopa, kwa sababu mara kwa mara tumekuwa tukijielekeza kukopa katika kiwango ambacho kwamba deni hili liwe himilivu, lakini pamoja na mkakati na umahiri huo, bado deni hili limekuwa likiongezeka kwa kasi kubwa na sababu kubwa ni kwamba bado hatuja-*interact* baadhi ya *factor* ambazo ni muhimu kwa ajili ya kufanya pesa yetu iimarike, kwa nini? Kutokuimarika kwa pesa hii, kunasababisha *impact* kubwa sana ya *exchange rate* kwenye deni hili. Ukiangalia hili Deni la Taifa, Deni la Serikali utakuta kwamba eneo kubwa la kukua kwake kunategemeana na *rate* ya *exchange* na riba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichokikopa siyo kikubwa ukilinganisha na hali halisi ya deni lenyewe. Sasa kutokana na hali hiyo bado tumeona kwamba jitihada kubwa zinazofanyika hazina *impact* hasa katika eneo hili la kuimarisha pesa ya shilingi, kuimarisha uchumi kwa ujumla na kufanya uchumi wetu uwe wenye manufaa na tija kwa *society* yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia mjengeko wa riba kwenye mfumo wa pesa, unaweza ukakuta viashiria vya haya mambo ninayoyasema. Kwenye riba ya kibenki, imepungua riba kati ya benki na benki na riba ya kibiashara ni kama bado imebaki palepale, iko juu. Ukienda kwenye riba ya dhamana za Serikali unakuta imekwenda mara dufu, hali ambayo inasababisha na kushawishi wawekezaji kuacha kuwekeza katika *production activities* kwa maana uzalishaji wa bidhaa ambazo ndiyo muhimili mkubwa wa usafirishaji kwenda nje na wanafanya kazi ya kununua dhamana hizi kwa maana ya kuwekeza kusudi kuwapatia pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata *role* ya benki ambayo inatakiwa ifanyike unakuta haifanyi sawasawa, benki nao wame-*concentrate* katika kukopesha Serikali, hali kadhalika, kukopesha wawekezaji au watu ambao tayari wamepevuka wana uwezo wa kupata *capital* kutoka katika vyanzo vingine. Unakuta benki imejielekeza huko haitaki yaani imekosa uthubutu kabisa, benki imekuwa na uwoga, benki imeshindwa hata kutoa fursa kwa wananchi wa kawaida katika ku-*enjoy* mikopo katika maeneo hayo kwa kisingizio *cha risk* (hatari).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hali hii kwa sababu ukizingatia kwamba hawa wananchi ndio wengi lazima athari yake ya kiuchumi utaiona pale kwamba watakosa pesa za kuwekeza na mwisho wa siku hakutakuwa na kitu chochote ambacho kitakuwa kimefanyika kwa ubora wake. Mipango ambayo tunayo, mipango mingi sana imekuwa haiendani na uhalisia na changamoto tulizokuwa nazo kama nchi kwa uchumi wa nchi hii. Mipango mingi imekuwa ikienda nusunusu tunakwenda sehemu tunagota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa hali jinsi ilivyo hii mikoa ya kusini hii mikoa imekaa kimkakati Mkoa wa Mtwara, Lindi, Ruvuma na Iringa ni mikoa ambayo imekaa kimkakati, lakini ni mikoa tajiri sana kwa uzalishaji wa chakula, pia ni tajiri katika masuala ya utalii, hali kadhalika ni tajiri kwa sababu ya mipaka iliyokuwa nayo. Inapakana na nchi ambapo nchi hizo ni tegemezi katika mikoa hii, lakini licha ya kuwa na hiyo hali bado hakuna mkakati mkubwa wa waziwazi kabisa wa kuonesha kwamba mikoa hii ina utajiri huo. Bado imeachiwa yenyewe ikihangaika katika kufanya uwekezaji mdogomdogo wa mtu binafsi. Tunahitaji uwekezaji mkakati katika mikoa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninategemea katika Mpango huu nione Reli ya *Standard Guage* ikitoka Mtwara kuelekea Mchuchuma mpaka *Mbamba Bay,* kwa ajili ya nini? Maeneo hayo yana uzalishaji wa Chuma cha Liganga, lakini pia na makaa ya mawe ambayo ni muhimu sana katika uchumi wa Tanzania pamoja na uchumi wa dunia kwa sasa hivi kwa maana ya nishati ya makaa ya mawe. Hali kadhalika, chuma ambacho sasa hivi dunia nzima imekuwa kikipatikana kwa kiasi kidogo sana kwa hiyo kama tungejikita katika maeneo haya bila shaka hii *gap* inayotokana na masuala ya *exchange rate,* lakini na pia kutokukua kwa uchumi, yangepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda ninaona niunge mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mchungahela ninakushukuru sana. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, atafuatia Mheshimiwa Zaytun Seif Swai na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niwe miongoni mwa wachangiaji jioni yetu ya leo. Ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na kuweza kusimama jioni hii. Mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti, nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote na Manaibu Waziri yale mawazo ambayo tulitoa kwenye Kamati yetu mengi wameya-*accommodate,* ninaomba niwapongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wetu tunaenda kufanyia maboresho, lakini tukiwa bado tuna *advantage* ya baadhi ya mambo ambayo ninaomba niyataje ambayo yanatupa nafasi nzuri kama Taifa. Tunaenda kufanya maboresho ya Mpango sisi kama Taifa tukiwa na amani ya kutosha, lakini pia tunaenda kufanya maboresho kukiwepo *SGR,* lakini na *TAZARA* ni *advantage* kwetu kubwa sana kama Taifa, lakini tunaenda kufanya maboresho ya Mpango tukiwa na uhakika juu ya umeme baada ya uzalishaji kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaenda kufanya maboresho katika Mpango ambao utakuja tukiwa na uhakika uwekezaji mzuri ambao umefanywa kwenye bandari yetu na *efficiency* kwenye bandari yetu imeongezeka. Pia tunaenda kufanya maboresho tukiwa na uhakika na *tax calendar* ambayo kwa vyovyote vile mwekezaji anapokuja ana uhakika wa uimara wa sera zetu ndani ya miaka mitatu. Vilevile, tunaenda kufanya hayo maboresho tukiwa na uhakika juu ya *geographical position* ya Taifa letu ambayo Mataifa mengine hawana fursa kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na uhakika juu ya ukuaji wa uchumi ya Taifa letu pamoja na mitikisiko ambayo imetokea duniani uchumi wa Tanzania umezidi kuwa bora ukilinganisha na uchumi wa nchi nyingine. Tunaenda kufanya maboresho haya tukiwa na uhakika wa Soko la *East Africa* lenye idadi ya watu milioni 302 kwa hiyo tuna soko la kutosha, lakini miundombinu yetu ukilinganisha na nchi majirani zetu bado tuna miundombinu iliyo bora sana; lakini tunaenda kufanya maboresho tukiwa bado tuna fursa kwenye uchumi wa bluu. Vilevile, tunaenda kufanya maboresho tukiwa na uhakika wa *food security,* tuna chakula cha kutosha kama Taifa. Tunaenda kufanya maboresho kukiwepo na vivutio vya kiutalii huwezi ukalinganisha na majirani zetu wote. Tunaenda kufanya maboresho tukiwa na madini mengi ambayo huwezi ukalinganisha na Mataifa mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie maeneo ya changamoto ili mpango wetu uweze kuwa vizuri tukiwa na orodha ndefu hii, nimezitaja tu kwa uchache *advantages* ambazo tunazo kama Taifa. Uwepo wa *SGR* ni jambo jema, lakini *SGR* hii ili tuanze kupata matunda yake ni pale ambapo ujenzi

wake utakamilika kwenda kufika Mwanza, Kigoma na huko kwingine nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe katika Mpango tusije tukaingia kwenye ile wanayoita *Dutch disease* kwamba tunafika mahali ambapo tuna-*concentrate* eneo hilo tukaacha reli zetu zingine kwa maana ya *Meter Gauge Rail* tuhakikishe inaendelea kuwepo lakini kubwa zaidi ni uwepo wa *TAZARA* na maboresho ambayo yanafanyika ninaomba tushukuru waasisi walioona mbali. Tuhakikishe kwamba *TAZARA* tunaiboresha na niiombe Serikali katika Mpango ni wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na tawi ambalo linaanzia Tunduma kwenda *Kasanga Border* ili tuweze ku-*access DRC* kwa njia ambayo ni fupi kuliko njia zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itakuwa inasaidia Taifa kuhakikisha kwamba tunaenda huku ambapo mzigo upo mwingi ambao hautiliwi mashaka ambao ni Katanga kwa ya Lubumbashi na siyo kule Kalemie. Niombe wakati tunaendelea na ujenzi wa reli ni vizuri pia tukaendelea kufanya *research* tufanye utafiti hii reli yetu ya kisasa inapokuwa imekamilika inafika Mwanza, na Kigoma mzigo upi ambao tunategemea kwenda kuuchukua? Itakuwa si jambo jema mpaka tunamaliza ujenzi halafu hatuna uhakika juu ya mzigo kwa maana ya shehena tunaloenda kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri pia waendelee kufanya utafiti; je, kwa kukamilika kwa ujenzi wa reli hiyo msongamano wa malori ambayo yapo Tunduma utapungua na utapungua kwa sababu zipi? Ni vizuri *researchers* wakatujia na majibu kwa nini mzigo ambao unaenda Tunduma kama kweli utapungua utahama utaenda Kalemie jambo ambalo sitaki kuamini. Kwa hiyo, ipo haja ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha Reli yetu ya *TAZARA* ili iweze kusaidiana kuhakikisha kwamba Bandari yetu ya Dar es Salaam inaendelea kuwa *competitive* ukilinganisha na bandari za wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya kumalizia vipande hivyo ambavyo vimebaki iongezeke ili tuweze kunufaika na uwepo wa *SGR* pale ambapo hatutakuwa tunasafirisha abiria peke yake maana wachumi wanatuambia faida katika reli inapatikana pale

ambapo unasafirisha mzigo. Sasa tunafurahia habari ya kusafirisha abiria, lakini ili tuweze kuona *return on investment* ambayo inaonekana ni pale ambapo tutakuwa tumekamilisha ujenzi wa vipande hivyo vingine na reli yetu ianze kuhudumia sheheni ya mizigo. Niiombe Serikali katika jambo ambalo tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba tunakamilisha kwa wakati ni ujenzi wa *SGR* pasi na kusita kwa sababu iwayo yoyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba katika Mpango ni vizuri tukasititiza ni uwepo wa Sera za Kikodi ambazo zinatabirika. Ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha tume ambayo inaenda kufanya mapitio juu ya kodi zetu ili kama Taifa tupate kodi stahiki kwa sababu sasa hivi kile ambacho tunakusanya *against GDP* ni kidogo. Sasa hivi kwenye Mpango tunakusudia kwenda 13%, lakini tukifika 15% ya *GDP* hapo ndiyo tutasema tunakusanya kodi ambayo ni stahiki na tushindane na Mataifa mengine hicho ndiyo kiwango ambacho kinakubalika, 13% bado ni kiwango ambacho hakikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera za Kikodi ziwe zile ambao zinatabirika. Mwekezaji anataka anapokuja kuwekeza hapa awe na uhakika kwamba kodi zake anaweza aka-*plan* hata baada ya miaka 10 anajua kiasi gani ambacho alikuwa analipa kama kodi kulikoni kila baada ya miaka miwili inabadilika kwa kweli haileti tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninaomba niongelee ni juu ya suala zima la upatikanaji wa mitaji. Mitaji inaweza ikapatikana ndani ya nchi au kutoka nje ya nchi. Kutoka nje ya nchi tunaweza tukapata *either* kwa kukopa, tukapata kama msaada, lakini tukapata wawekezaji ambao wanaweza wakawekeza kwa kutumia hisa kwa maana ya kununua *shares* kwa *DSE* ambayo ipo Tanzania. Vilevile, namna nyingine ya kupata mitaji ni kwa kutumia *DSE* kwa maana ya kwamba ndani ya Tanzania Watanzania ambao wangependa kwenda kununua *shares* wakienda *DSE* wakute *shares* zipo

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu niiombe Serikali wana misuli ya kutosha, wana uwezo wa kukopa nje ya nchi; ndani ya

nchi waachie *private sector* ili wasiwe wananyang'anyana hicho kidogo ambacho kinapatikana kwenye benki zetu kiasi kwamba benki zinaona namna iliyo bora kwa sababu kwenda kuwekeza Serikalini kwa maana ya *treasury bonds* na *bills* ni sehemu ambayo unaenda kuwekeza na hakuna *risk* yoyote. Kwa hiyo benki yoyote janja au yeyote ataona bora afanye biashara na Serikali, kwa hiyo maana yake ni kwamba tunaiua *private sector* lakini hali kadhalika hata *interest rate* ambazo zinatozwa Serikali inatoa 16%. Kwa hiyo, kwenye benki inakuwa hiyo ndiyo kama *benchmark* hata unaposema tupunguze *interest rate* wanatazama je, ya Serikali tunapata ngapi? Kama Serikalini unapata 16% kwa nini akija Kandege usimwambie 20% ni vizuri Serikali ikatafakari ili Watanzania walio wengi ambao wanataka kuwekeza wapate *interest rate* zilizo chini ndani ya benki zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niunge mkono hoja na ninakushukuru kwa fursa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kandege, ahsante sana. Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje na Mheshimiwa Joseph Kasheku ajiandae.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia na kutoa maoni yangu kwenye mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2025/2026. Kwanza ninaomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutatua changamoto nyingi za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kuchambua Taarifa zote mbili zilizopo Mezani hapa, Mapendekezo ya Mpango pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na tuliweza kutoa maoni yetu na maoni mengi yameingizwa kwenye Taarifa hiyo ya Kamati na ninaunga mkono hoja maoni yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye masuala machache ili basi niweze kushauri jinsi gani tutaweza kuboresha Mpango yetu kwa kiasi kikubwa. Jambo la kwanza ni katika utekelezaji wa miradi yetu ya kimkakati na kwenye hili tumeona mara nyingi kwamba miradi ya kimkakati na mikubwa inachelewa kwa sababu ya kutokuwa na *coordination* nzuri ndani ya Serikali. Tumeona Wizara zetu bado hazisomani, lakini taasisi za umma ndani ya Serikali hazisomani na hivyo kuchelewesha miradi mikubwa ya kimkakati kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kukutana na wenzetu wa Shirika la Mandeleo ya Taifa *(NDC)* na walitueleza changamoto mbalimbali ambazo wao wenyewe wanakutana nazo ambazo zinawakwamisha kutekeleza miradi hii ya kimkakati kwa haraka. Wenzangu wameongelea hapa sana mradi mkubwa huu wa Liganga na Mchuchuma na tumeona kwamba kama Taifa ni jinsi gani tunachelewa kunufaika na faida za mradi ule kwa sababu ya kuchelewa kutekeleza kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita kwenye mradi mmoja wa Magadi Soda wa Engaruka. Mradi huu wa Engaruka wa Magadi Soda umeainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Tatu wa Miaka Mitano na ni mradi ambao unaonesha dhahiri kwamba ukitekelezwa kwa haraka, basi kama Taifa tutaweza kunufaika na faida nyingi kupitia mradi huu. Mradi huu cha kwanza utachochea ajira nyingi za Watanzania, lakini pia utachochea uanzishwaji wa viwanda vipya. Malighafi ya magadi soda inatumika na viwanda vingi ikiwemo viwanda vya kemikali, viwanda vya kutengeneza kioo, lakini pia kwenye kilimo wanatumia sana magadi soda kwenye kutengeneza mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mradi huu tutaweza kuongeza mapato ya Serikali kupitia kodi na tozo mbalimbali. Pia, tutaokoa fedha nyingi za kigeni ambazo ni takribani dola milioni 120 na zaidi ambazo kwa sasa zinatumika kwenye kuagiza malighafi hii ya magadi soda nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na manufaa haya utaona kabisa ni dhahiri kwamba mradi huu ukitekelezwa kwa haraka, basi tutaweza kupata manufaa mengi katika nchi yetu.

Pamoja na manufaa haya Shirika letu la Maendeleo ya Taifa *(NDC)* walituambia wana changamoto kubwa, Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini wanatakiwa walipe leseni ya uchimbaji wa madini ambayo ni takribani dola 153,000 na *NDC* wamekwama wameshindwa kulipa dola hizi na hivyo kuzuia na kuchelewesha mradi huu kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia hii unaona kabisa kwamba ni dhahiri ndani ya Serikali wenyewe kwa wenyewe pia tunajichelewesha kwenye kutekeleza miradi hii muhimu na ya kimkakati. Kamati imeshauri vizuri sana kwamba kwa miradi ile ambayo inatekelezwa na taasisi za umma ndani ya Serikali basi tuweze kuwa na utaratibu wa msamaha wa kodi au tozo mbalimbali ili kuweza kufanya miradi hii inatekelezwa kwa haraka na Taifa liweze kunufaika na faida zinazotokana na miradi kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo mwenzetu wa *NDC* walituambia ambayo inafanya mradi huu usitekelezwe kwa wakati ni ukosefu wa miundombinu sahihi ambayo inaelekea kwenye mradi. Kwenye Mradi huu wa Engaruka kuna barabara za kimkakati, barabara kutoka Mto wa Mbu kwenda Selala lakini kuna Daraja ambalo linaelekea pia kwenye mradi Daraja la Mto wa Athumani ambapo miundombinu hii haijapewa kipaumbele ijapokuwa inaenda kwenye mradi wa kimkakati kama huu. Ninashauri pia Serikali iweze kutoa kipaumbele kwenye miundombinu yote ambayo inaelekea kwenye miradi ya kimkakati kama hii ili basi utekelezaji wa miradi kama hii uweze kwenda kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwenye Sekta ya Utalii, mara nyingi tumeona kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa malazi ya kulaza wageni wetu, Kamati ya Bajeti mara kwa mara imekuwa ikishauri Serikali iweze kufanyia kazi na ichukue hatua kwenye suala hili bado suala la malazi ni changamoto kubwa. Pamoja na jitihada kubwa ambazo anafanya Mheshimiwa Rais wetu, jitihada za kukuza sekta hii ya utalii, ninashauri Wizara yetu ya Mpango basi iweze kuweka mikakati thabiti ya kuendana na jitihada hizo ili basi tuweze kupata

wawekezaji mahiri na wa uhakika wa kuwekeza katika sekta yetu hii ya utalii na kujenga hoteli yenye hadhi ya kulaza wageni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imekuwa ikikutana na wadau mbalimbali wa utalii na wametueleza changamoto ambazo zinasababisha wawekezaji wengi kusita kuwekeza kwenye sekta hii muhimu ya utalii kwa ujenzi wa hoteli. Moja ya sababu kubwa waliyotueleza ni mikataba mibovu ya uwekezaji ambayo inaweka ukomo kwenye uwekezaji wa hoteli, ukomo wa miaka 15. Vilevile, mikataba hiyo haielezi wazi kwamba, kama mwekezaji hajarudisha faida yake ule uwekezaji utabaki kuwa wa nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni kwamba, wawekezaji wale hawapewi hati ya maeneo ambayo wanawekeza na hii ni changamoto kubwa. Hii changamoto kwanza inawafanya wawekezaji waogope kuwekeza kwenye yale maeneo kwa sababu, siyo ya kwao, lakini vilevile changamoto hii inawazuia wawekezaji wetu wasiende kukopa kwenye taasisi za fedha. Hivyo, naomba sana Wizara ya Mipango na Uwekezaji wakishirikiana na Wizara ya Kisekta waweze kuangalia kwa kina hizi changamoto, ili basi waweke sheria na kanuni ambazo haziwabani wawekezaji kuwekeza kwenye sekta hii ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia tu, naomba niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Mkoa wetu wa Arusha ametuletea miradi mingi ya maendeleo na kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 hadi Septemba, 2024 tumepokea zaidi ya shilingi trilioni 2.7 ambazo zimeelekezwa kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Mkoa wetu wa Arusha unachangia takribani asilimia 4.7 kwenye Pato la Taifa na kuipa nafasi ya sita Kitaifa. Bado Mkoa wa Arusha una nafasi kubwa sana ya kuwekeza kwenye rasilimali zake na ninaamini kwamba, Wizara ya Mipango na Uwekezaji ikiangalia kwa jicho lingine Mkoa wa Arusha wanaweza wakaongeza zaidi uwekezaji kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia; kuna viwanda kama vya *General Tire* na *Kiltex* ambavyo hapo awali vilikuwa vinachangia sana kwenye pato la Taifa. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Mipango na Uwekezaji iangalie ni jinsi gani itaweza kuvifufua viwanda hivi, ili basi viweze kuchangia zaidi kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zaytun Swai. Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2025/2026. Nimesoma mpango wenyewe, pia, nimesoma na kusikiliza hotuba ya Waziri wa Mipango na Uwekezaji, pia, nimesikiliza nakusoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nimesoma taarifa ya kamati na nimefanya marejeo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa, ule wa 2024/2025. Kwa kurejea hizo zote na kusikiliza kila walichokizungumza kuhusiana na mpango huu wa mwaka 2025/2026 imenikumbusha na nikakumbuka kwa sababu, nafahamu unapoizungumzia Tanzania unazungumzia mambo matano au sita ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, unapoizungumzia Tanzania, unazungumzia *human development,* unazungumzia maendeleo ya watu. Tunazungumzia Sekta ya Maji, Sekta ya Elimu na Sekta ya Afya. Tunazungumzia mazingira na masuala ambayo yanahusiana na watu kwa sababu, tumesema maendeleo ya vitu ni lazima yaende na maendeleo ya watu. Kwa hiyo, unapoizungumzia Tanzania, moja ya jambo la msingi ni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili la msingi, siyo kwa umuhimu, lakini kwa kuyataja ni Sekta ya Utalii, *tourism industry* au *tourism sector,* lakini unapoizungumzia Tanzania unazungumzia

*agricultural sector,* ndiyo sekta ambazo ni za msingi, zimeishika Tanzania. Huwezi kuweka miradi yoyote ambayo iko nje ya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ni *extractive industry*, sekta ya uziduaji, kwa maana ya uchimbaji wa madini. Huwezi kuzungumza maendeleo, mipango na uwekezaji wa Tanzania bila kuzungumza hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano ni *logistics,* usafiri na usafirishaji na kwingine tunakopambana sana ni viwanda na biashara. Bado tunaendelea kujipanga, lakini mambo ya msingi ambayo tunategemea katika kukusanya mapato, tunategemea katika kutawanya mapato ni katika mambo hayo matano ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, nimesema nimesoma hayo yote na nimeeleza kwamba, Tanzania *is about those five industries,* basi niwapongeze sana Wizara ya Mipango chini ya kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, pia, kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba pamoja na, mmeongezewa kifaa kingine hapo, ndugu yetu Stanslaus Nyongo ambaye pia, ni Daktari, *if I am not mistaken.* Naibu Waziri pale, pamoja na timu nzima ya Wizara ya Mipango na Uwekezaji bila kuwasahau watendaji ambao najua wanakimbia sana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, Tanzania inapata mipango ya watu ambao wametoka kwenye mifupa ya watu wa Singida, akili zao zimekaa sawa, ndiyo wanaoongoza Wizara hizo mbili za msingi na kwa sababu, natoka huko ni lazima nijimegee hapo kipande, niwapongeze sana ndugu zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Kamati, wametu-*direct*. Wao waliupata mpango kabla na wakajadili mapendekezo, wametoa maoni, niwapongeze sana, wamefanya kazi kwa niaba yetu, lakini niwakumbushe. Moja, nasema nawapongeza kwa sababu, kama mtu amesoma mpango na amesoma nyaraka hizo ambazo nimezitaja, lazima ataona namna ambavyo watu hawa na watendaji wao wamehakikisha wanayashika yale maeneo matano ya msingi niliyoyataja na mapendekezo mengine. Hapo kuna maeneo sijayataja, kwa

mfano TEHAMA na vitu vingine ambavyo ni *cross cutting,* vinapita katika hivyo vyote. Wamegusa karibu vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo langu ni moja tu; Mheshimiwa Waziri na timu yako, ukiangalia *integrated labor force survey* ya Tanzania, nimefuata ya 2021, mwisho utaona nguvukazi ya Taifa namna ilivyogawanywa iko *pyramid.* Namna tulivyogawanywa kwenye mfumo wa elimu, yaani kwenye *level* za elimu kwenye nchi, kwenye *labor force* utaona kwamba, ni *pyramid.* Tulisema *pyramid* juu kabisa ndiyo kwembamba ambako kuna wasomi wa vyuo vikuu asilimia 1.8, *vocational training* ni asilimia 1.3 na 16.5% ndiyo elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliobaki wote ni elimu ya msingi. Kwa hiyo, kwa kusema hivyo ni kwamba, wanaoongoza uchumi, ambao ndiyo *labour force* ya nchi hii ni elimu ya sekondari na kushuka chini. Kwa hiyo, wakati tunapanga mipango yetu ni lazima tutafute namna tuta-*address* hilo suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote zilizoendelea walishika *tertiary* ambayo tunazungumzia kuwa ni vyuo, *vocational training.* Kwenye hilo sina mashaka kwa sababu, mimi niko Kamati ya Elimu, kuna namna ambavyo na sisi kule tunakimbizana kuhakikisha kwamba, upande wa kujenga ujuzi na wa *vocational training* tunakimbizana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe mipango yetu msiwe mnasahau hata siku moja kwamba, bado tunategemea mtindo huo katika *labour force.* Kwa hiyo, ni lazima tuhakikishe kwamba, tuna-*address* hayo mambo na tunayaweka katika mipango yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nilizungumza yale mambo matano, leo nitachagua moja tu na nitajielekeza katika *logistics,* usafiri na usafirishaji. Mwaka 2004 nilipata kusoma na kusikiliza mahali, wakati huo sisi kwa umri wetu tulifanya marejeo, lakini niliwahi kumsikiliza Rais wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamini Mkapa akizungumza kuhusu kiongozi shupavu na akamtaja kwa sifa kadhaa na nitatumia tatu kati ya hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alisema, kwanza kiongozi shupavu ni lazima awe na maono na dira katika malengo yake aliyojiwekea. Ni lazima awe na malengo katika jambo lake kwa sababu, ni kiongozi, lakini la pili, alizungumzia kiongozi shupavu ni lazima awe madhubuti katika kusimamia rasilimali watu kuelekea malengo na dira ambayo yeye anaiona, kama kiongozi kwa sababu, ni lazima muwe na kiongozi kwenye jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kuwa king'ang'anizi na madhubuti katika kuyasimamia malengo na maono ambayo yeye alikuwa nayo. Kwenye nukta hii na mimi nimeyarudia maneno hayo aliyoyasema Hayati Benjamini Mkapa kwa sababu, mimi ni miongoni mwa wanafunzi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika namna anavyoyaendea mambo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii nafasi ninaomba wote tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa sababu, kwenye suala la *logistics,* usafiri na usafirishaji, mwaka jana tuliona namna ambavyo nchi iliingia kwenye mtikisiko, tukizungumza kuhusu uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam, *DP World,* na hakuyumba. Ninasema hivyo kwa sababu, hata mimi ningekuwa kwenye hiyo nafasi ningefanya kama alivyofanya kwa sababu, kila kiongozi mwenye maono anapoingia kwenye madaraka hakuna anayetaka kupita bila kuacha alama na kwa sababu, kulikuwa na mtikisiko yeye alisimama imara mpaka leo,

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kushindwa kusema kifua mbele kwamba, kwa miezi mitano kuna mambo ambayo yamefanyika bandarini. Nitayataja kwa mfano kwa sababu, kwenye Wizara wamesema na mengine sisi tunayaona, mengine watayataja wao kwa vielelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtikisiko ulikuwa mkubwa, lakini leo naomba niwaambie mambo yanayoendelea kwenye Bandari ya Dar es Salaam na niwapongeze sana watu wa Bandari ya Dar es Salaam pale *TPA,* Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mamlaka ya Bandari ndugu yetu Mbosa. Kwanza, sisi kama vijana tunajiskia fahari sana kwa sababu, yule ni kijana mwenzetu na ana-*perform* vizuri kiasi kwamba, wengine tunaamini kama ameaminika na amefanya vizuri kuna vijana wengine wataaminiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini, mtoto mdogo akinawa mikono vizuri anakaribishwa kula na wakubwa. Kwa hiyo, Bandari ya Dar es Salaam tunafanya vizuri kwa sababu, Mheshimiwa Rais alikuwa imara wakati tunapitisha *DP World* na hakuyumba. Sasa leo nasema hapa kwa sababu, mimi natoka Singida, nimeona kuna vitu vimefanyika pale Bandarini na kuna makusanyo yanafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwa miezi mitano kuanzia Mwezi Aprili mpaka Septemba, Serikali imeweza kukusanya mapato takribani Shilingi za Kitanzania bilioni 325.3 ambayo sasa, Serikali kwa kuona namna hiyo na niwaambie hapa, Mheshimiwa Waziri inawezekana hizi *statistics* baadaye mwakani tukizirudia zitakuwa tofauti sana kwa sababu, nimwambie Waziri hiki kimefanyika wakati ule wanarekebisha mifumo. Yaani wakati wanafanya *procurement,* wakati wanaleta utaratibu mwingine mpya na haya yote yanaendelea kwa hiyo, wameweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu hii *five months* mmeweza, lakini kwa sababu, Serikali kupitia *TPA* inapanga kufanya *investment,* inapanga kufanya uwekezaji wa takribani shilingi trilioni 1.922 kwenye miradi mitatu ambayo wameitaja hapa, ikiwemo ujenzi wa Bandari ya Kisiwa cha Mgao huko Mtwara, huo ni mmojawapo. Naamini tukiendelea hivi, hata sisi watu wa Singida tutapata mradi wa umeme wa upepo sasa, maana yake mambo yanaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, nilisema ni *social development enthusiast,* napenda mambo yaende na haijalishi nani atakuwa anasababisha yaende. Kama kuna mtu akikaa pale anafanya maamuzi ambayo sisi kama nchi tunatoka hatua moja tunaenda nyingine, mimi nitamuunga mkono. Ndiyo maana mwaka jana wakati watu wanajiuliza, hivi uwekezaji wa bandari unalenga kutatua nini au tunapata nini? Mimi nilijiuliza kama uwekezaji wa eneo kama bandari utakuwa unatusaidia kuongeza mapato kama Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakuwa unatusaidia kuongeza ufanisi katika utendaji wa bandari, kama utakuwa

unatusaidia kuchochea ukuaji wa uchumi, nitaunga mkono na niliunga mkono na leo ninaunga mkono na ninaomba wasiache kusema. Tafadhali wafuatilie vizuri wapate taarifa. Naomba waongee kwa sababu, ni lazima tu-*set standard,* lazima kama kiongozi akiamua kusimamia jambo lake hebu wampe *benefit of doubt,* kama mtu unaona kuna *informed decisions,* mtu anafanya maamuzi ambayo yamefanyiwa tafiti na wataalam na unaona kuna namna kwa sababu, mtu anayefahamu, ambaye ni mtaalam, kuna namna ambavyo anaweza akazungumza zikaonekana kama *theory,* lakini zikafanyiwa utafiti na wakaona kuna namna wanaenda, kwa nini wamkwamishe mtu kama huyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ni sehemu moja tu nimesema ambayo naona hata sisi watu wa Singida tunaweza tukanufaika. Mpaka sasa hivi ninavyozungumza, haya yote ninayoyataja hapa, kwanza *TRA* wamekusanya mapato sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat, hujaunga mkono hoja, tafadhali.

Mheshimiwa Justin Lazaro Nyamoga, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo na Mheshimiwa Joseph George Kakunda ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameturuzuku uhai huu ambao tuko nao na tunapata fursa ya kuchangia mpango huu ili kuboresha na hatimaye kuendelea kuimarisha uchumi wa nchi yetu na kuyafanya maisha ya Watanzania yaendelee kuwa bora. Jambo ambalo wananchi wanatutarajia kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia mambo machache ya kushauri. Kwanza ni kuhusu vyanzo vya mapato na ni pili baadhi ya maeneo ya vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama zingefuatiliwa taarifa zangu za kuchangia mpango ambapo hii ninachangia ni mara ya tatu, mara zote nimeshauri kuhusu uongezaji wa mapato kwa kutafuta vyanzo visivyo vya kodi. Moja ya chanzo ambacho nimekizungumza sana ni chanzo cha biashara ya *carbon* au hewa ya ukaa. Nimekuwa nikichangia chanzo hiki na nikachukua muda wa kujiridhisha umuhimu wake na namna ambavyo kinaweza kikaboresha mapato na kupunguza vyanzo vingine vya kikodi ambavyo vinawaumiza Watanzania na nitajaribu kutoa mifano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina hudumu katika Kamati ya TAMISEMI na ziko halmashauri ambazo tayari zimeingia kwenye biashara ya *carbon.* Nitatoa mfano wa Wilaya ya Tanganyika ambayo mwaka jana imepata shilingi bilioni 14 kupitia biashara ya *carbon* kwenye misitu yake. Ipo mikoa ambayo mapato yake ya ndani hayafiki shilingi bilioni 14, lakini Tanganyika siyo peke yake ambayo ina mapato na ina misitu inayoweza kusajiliwa na kuingia katika biashara ya *carbon.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara ya TAMISEMI. Nimekuwa nikifuatilia ushauri ambao Kamati imekuwa ikiutoa, nimeona wakianza kutoa semina na mafunzo kwa Halmashauri, ili ziweze kuingia kwenye biashara hii. Sasa kama halmashauri zetu zikipata chanzo kikubwa cha mapato ya ndani ambacho siyo cha kikodi. Mfano, mapato yake yakawa ni shilingi bilioni tano, bilioni 10, bilioni 12, kama hivi tunavyoona maana yake ni kwamba, tunawapunguzia Watanzania mzigo wa vyanzo ambavyo ni vya kikodi na kwa hiyo, uchumi wao utakuwa kwa sababu, tumepata mbadala ambao si chanzo cha kikodi. Hili jambo linawezekana

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hapa nimezungumzia Wilaya ya Tanganyika ambayo inafanya biashara ya *carbon* kwenye eneo la misitu, lakini turudi kwenye vyanzo vingine vinavyoweza kufanyika kwenye biashara ya *carbon.* Hapa tujiulize, kwa mfano,

faida za *SGR* ni pamoja na kupunguza idadi ya mabasi yanayotoka Dar es Salaam kuja Dodoma, kile kiasi cha *carbon* kilichokuwa kinazalishwa na yale mabasi, sisi kama nchi tunaweza kusajili kama mradi na tukapata mapato. Mapato yake yanaweza kuwa makubwa kuliko nauli ambazo Watanzania wanalipa. Swali la kujiuliza ni je, tayari *TRC* wamesajili? *TRC–SGR* kama moja ya miradi ya *carbon*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishashauri kwa mfano, Mradi wa Mwendokasi, *DART,* pale Dar es Salaam, kwamba, kwa sababu, tulipunguza mabasi katika Jiji la Dar es Salaam maana yake ni kwamba, idadi ya mabasi madogo tuliyopunguza ile *carbon* iliyokuwa inazalishwa tungeweza kufanya kuwa mradi ukaingiza mapato katika Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam. Je, *DART* walisajili ule kama mradi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachokosekana ni weledi na utaalam katika kusajili miradi hii na kupata mapato. Tuombe ndugu zetu wa Wizara ya Mipango na Uwekezaji kuangalia fursa hii kwa sababu, mara zote tumesema fursa hii siyo ya muda wote, upo wakati itapotea na sisi kama nchi tutakuwa tumepoteza fursa ya mapato yasiyo ya kikodi ambayo yangeweza kupunguza utegemezi wa mapato ya kikodi ambayo kwa vyovyote vile yanawaumiza Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nirudie kusema kwamba, hatua zinaonekana. Kituo kinachosajili kipo pale Chuo cha Kilimo Sokoine, kinafanya vizuri, kinasajili miradi, lakini bado Serikali inatakiwa kuwekeza kwa kiwango kikubwa kufanya maeneo husika, hasa Serikali za Mitaa na Halmashauri, kuelewa umuhimu wa kusajili miradi na kuhakikisha kwamba, tunapata mapato ambayo siyo ya kikodi. Hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kushauri ni kuhusu sekta ya kilimo na hapa nirudie ambalo wengi wamesema. Nchi yetu haiwezi kuendelea kwa kutegemea kilimo cha kutegemea mvua, bado tunahitaji kuwekeza kwenye umwagiliaji. Niipongeze Wizara ya Kilimo kwa sababu, ukiangalia tulipewa takwimu na Kamati ya Bajeti kwamba, lengo ilikuwa

tufikie hekta milioni 1.2, lakini hadi sasa tuko hekta 727,000 siyo padogo ni hatua kubwa sana tumefikia na hii ni 60%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mpango wetu unaelekea mwishoni, lakini kuvuka 60%, kama ni mtihani nadhani tayari tuko kwenye C. Bado kidogo mpaka mwaka huu uishe, kama ni matokeo tunaweza kupata B, lakini ushauri wangu ni kwamba, bado tunahitaji miradi ambayo bado haijakamilika ikamilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mabwawa 18 ni mabwawa matatu ndiyo taarifa inasema yamekamilika kabisa. Maana yake ni kwamba kuna haja ya kuwekeza fedha, ili haya mabwawa mengine yaliyosalia kukamilika yakamilishwe na kama tunataka kujiridhisha tunaweza kujifunza kwenye maeneo ambayo haya mabwawa yamekamilika ni jinsi gani hali ya uchumi wa wananchi kwenye haya maeneo inabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi na ni dhahiri kwamba, hamna namna wala hamna njia nyingine ambayo tunaweza kusonga mbele kama hatutoi kipaumbele katika uboreshaji wa kilimo. Kwa kweli, Wizara ya Kilimo inafanya kazi nzuri sana, *integration* ni kitu muhimu, haya mabwawa yakishakamilika ndiyo sasa tutajua ni aina gani ya mbolea, mbegu, viuatilifu vinahitajika na kuwekewa ruzuku ili kukuza kilimo kwenye hilo eneo, tukifanya hivi tutaona kabisa uchumi unakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo inabidi tuliangalie kwa sababu hakuna namna tunaweza kukwepa kukuza uchumi wa nchi yetu bila kuangalia ukuaji wa Sekta ya Kilimo, pia hatuwezi kuangalia Sekta ya Kilimo nje ya kuangalia Sekta ya Umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza jambo hili, katika kufanya kilimo vizuri, kwenye mipango yenu angalieni vizuri jinsi ambavyo halmashauri zinavyotenga bajeti kwa ajili ya uendelezaji wa kilimo. Wote wanategemea mapato mengi kutokana na kilimo, lakini hata vitabu vitakatifu vinasema huwezi ukavuna mahali ambapo hukupanda! Sasa wao wanategemea mapato makubwa kutoka kwenye kilimo ambacho asilimia ya bajeti yake

ni ndogo sana, maana sisi tunazipitia mara kwa mara hizi bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya kuweka kiwango cha bajeti ya ya kilimo na yako maazimio haya ya Kimataifa yamewekwa, nchi inatakiwa itumie asilimia fulani, hivyo hivyo, maazimio haya yashuke kwenye halmashauri kwamba, kwenye Sekta ya Kilimo ni lazima tuweke asilimia fulani kwa sababu ndiko tunakotegemea mapato makubwa, kama huwekezi kwenye kilimo mapato yatakuwaje? Sasa ndiyo pale unaweza kuanza kutafuta vyanzo vya mapato na hupati kwa sababu uwekezaji wako kwenye kilimo ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko haja pia ya Wizara ya Kilimo kuangalia namna ya kuzielekeza vizuri Halmashauri kuhakikisha kwamba huo upangaji wa bajeti unalenga katika maeneo ambayo yatakuwa na tija katika kukuza uchumi ili mapato ya Halmashauri yaweze kukua pia uzalishaji wa mazao kwa wananchi uweze kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ningependa kushauri leo ni kuhusu mpango mzuri wa matumizi ya fedha hasa pale ambapo zinakuwa zimekusanywa. Katika maeneo ambayo tathmini na majadiliano mbalimbali tunayoyafanya tumeona hayo maeneo yanahitaji *attention* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni ukarabati wa shule kongwe za msingi. Shule nyingi za msingi zilijengwa miaka ya 1970 na 1980 kidogo, kwa hiyo shule nyingi zimechakaa. Pia, miradi mbalimbali inajenga shule mpya. Kwa hiyo, zile shule mpya zinakosa uwiano au kufanana na hizi shule ambao zimechakaa. Ni eneo ambalo pia Serikali inaweza ikazielekeza Serikali za Mitaa -halmashauri kujenga shule kongwe vizuri. Kwa hiyo, wanaweza kuwaelekeza kwamba, kipaumbele kiwe kwenye hilo eneo ila lazima kupeleka fedha nyingi, hata kama watapeleka, lakini hata utengaji wa fedha kwenye halmashauri ulenge kwenye maeneo yenye matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni ujenzi wa *hostel* za wasichana na *hostel* za wavulana kwa sababu kumejitokeza kusahau kwamba hata watoto wa kiume nao ni watoto, siyo kwa sababu ni wa kiume basi ni mkubwa, ndiyo maana ukifuatilia takwimu sasa hivi, ujenzi wa *hostel* nyingi za wasichana umesababisha wasichana wengi wanamaliza, lakini watoto wengi wa kiume wanaacha shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udahili unakuwa mwingi, lakini umalizaji unakuwa mdogo! Hivyo, kwa sababu sasa hivi kupitia miradi mbalimbali shule nyingi za sekondari zimejengwa kwenye maeneo mbalimbali, lazima tujielekeze kwenye kuhakikisha kwamba, kwa sababu ya umbali sasa Halmashauri na Serikali kuananza kuwekeza kwenye ujenzi wa *hostel* kwa sababu ya kufuta ule umbali. Hiyo itasababisha *performance* ya wote, watoto wa kike na watoto wa kiume kufanya vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa, ambapo ule umbali wa kutembea unakuwa mrefu na hivyo inakuwa ni changamoto kubwa *crosscutting* kwa nchi nzima na kwamba kila unapokwenda, ukiacha maeneo machache ya mjini, watoto wanatembea umbali mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ninawapongeza wote ambao wanaendelea kuandika na kupata maoni yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Justin. Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, ajiandae.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ambayo nimepata ili na mimi niweze kuchangia kwenye mpango wetu huu wa maendeleo wa Taifa. Nami nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Naibu Mawaziri na wataalam wote walioshiriki kuandaa mpango huu, bila kuisahau Kamati nzima ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kabisa kwamba, naunga mkono hoja maana kuna msemaji amesifia

vizuri, ametoa mchango wake, amemsifia Rais na akawasifia Mawaziri wanatoka kwake, akashindwa kuunga mkono hoja hii. Nami nikajua ndiyo maana Mawaziri wote wawili wameoa Mkoa wa Kilimanjaro, maana sasa kama huungi mkono hoja kidogo anasababisha waje kule kwetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kupongeza Serikali kwa namna ambavyo inasimamia mpango huu. Nianze kwa kusema kwamba, kuna maneno ambayo ningetamani sana tuyaone kwenye mpango wetu. Sijayaona moja kwa moja kwenye hotuba na pengine yapo kwenye tafsiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona mahali ambapo tumeonesha nia thabiti ya kwenda kuwa na bajeti ambayo tunaweza *kui-fund* wenyewe kwa 100%. Sijaona mahali kwenye huu mpango ambapo tunayo nia ya kwenda kuhakikisha bajeti yetu kwa miaka hii ya hivi karibuni, mwaka 2025 tutatoa utegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua sasa hivi tuko kwenye 70%, lakini ni lini tutafikia 80%, 90% na 100%? Pia, hata kwenye mapendekezo ya Kamati wamesema na wamelitaja hilo kwamba, ni eneo ambalo na wenyewe wanategemea kuliona, kwamba, angalau sasa katika kila mpango tuseme mpango huu pamoja na mambo yetu yote tuliyoweka, tunategemea utegemezi wa bajeti yetu kwenye mikopo, misaada, mikopo ya nje tutaisogeza kutoka kwenye hii 30%, tutabaki na 10% na kuendelea. Kwa hiyo, hilo nategemea tuanze kuliona kwa siku ambazo zinakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nilitegemea pia kuona ni namna gani mpango huu unakwenda kuongeza *tax base*. Mheshimiwa Rais wakati anaongea na ile Kamati ya kwenda kumshauri kuhusiana na mambo ya kodi alisema kabisa kwamba, Tanzania wanaolipa kodi moja moja wanaonekana ni milioni mbili tu, sasa nilitegemea kwenye mpango utuoneshe ni namna gani tumekusudia kwenda kuongeza *tax base,* badala ya kwamba ni watu milioni mbili au taasisi milioni mbili, tunatoka milioni mbili, tunakwenda milioni mbili na laki tano, milioni tatu na kuendelea ili *Tax base* ikiongezeka, maana yake mzigo wa *tax* kwa wale

wachache ambao wanatambulika utakuwa umepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye miradi ya kimkakati. Ninaipongeza sana Serikali na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwamba, miradi hii ya kimkakati imeshaonekana tayari inaleta tija. Leo tunaongelea *SGR* tayari inafanya kazi, leo tunaongelea bandari, wameelezea mafanikio ambayo yalikuwepo kwenye yale maono na tayari yameshaanza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea Bwawa la Mwalimu Nyerere, juzi nimeona nadhani wale ni *songas*, mkataba wao umeisha na wala hatuna haraka wala wasiwasi wa kuwaongezea Mkataba kwa sababu umeme tayari tunajitosheleza. Vilevile, naona jinsi ambavyo shirika letu la ndege linavyoendelea kupambana, kwanza, kutoa usafiri ndani ya nchi, lakini kuendelea kupambana kimataifa. Tumeanza safari za Afrika Kusini, Marekani, Uarabuni na nyingine zinakwenda Zanzibar na kadhalika, kwa maana ya kwamba kutoka nje na kuja Zanzibar moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, juhudi za Serikali kuhakikisha Dodoma kama Makao Makuu inaendelea kuwa ndiyo makao makuu ya nchi, inapendeza na tunaona kabisa Serikali inafanya juhudi. *Airport* inaendelea na miradi inaendelea, kwa hiyo, ninaipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii miradi imetupima sana uwezo wetu wa kutekeleza mambo, ili sasa tuendelee tusikate tamaa na tusiridhike ni vizuri sasa ile miradi mingine ambayo inazungumziwa sana *LNG*, Liganga na Mchuchuma, tuweke *timeframe* kwamba, ni lini na hii inaingia kuongeza nguvu katika pato letu la Taifa, miradi mikubwa na kuonesha kwamba uchumi wetu unakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la utalii, kwa sababu Moshi Mjini ni moja ya vituo vya utalii katika Kanda ya Kaskazini, ni eneo la muhimu sana. Nimeona nia ya Serikali kuhakikisha kwamba utalii wa mikutano, utalii wa michezo na utalii wa kimatibabu, unakwenda kujumuishwa katika kutangazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye takwimu, kwenye yale majedwali pale, naona kama kuna tatizo. Tumesema tunategemea kutoka watalii milioni mbili kwenda milioni tano, lakini mchango wao kwenye Pato la Taifa, milioni mbili kwenda milioni tano ni zaidi ya mara mbili ya idadi ya watalii tunaowapata. Pia, *expenditure* ya kila mtalii kutoka dola 230 kwenda dola mia tano hamsini na kitu kwa mwaka 2026, mchango ni kama mara mbili, lakini mchango wake kwenye pato la Taifa tunasema utatoka 17.5% kwenda 18.9%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa wakati watoa hoja wanaenda kuhitimisha hili wanifafanulie vizuri, kwa sababu kimapato tumesema *expenditure* ya mtalii mmoja itatoka zaidi ya dola 200 na kwenda zaidi ya 500, tumesema idadi ya watalii tunategemea itoke milioni mbili kwenda milioni tano. Sasa inakuwaje kwenye mchango tumesogea asilimia moja tu? Nadhani kuna kitu hapa nitaomba watufafanulie ili na sisi tuweze kufahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kusisitiza kwamba, pia kwenye eneo la utalii tuangalie namna ya kuongeza utalii unaotokana na *manmade attractions*, vitu tunavyovitengeneza. Nilishasema tena Dubai ina utalii maradufu ya sisi na vitu vyao vingi ni *man made*. Kwa hiyo, tuendelee kuangalia vitu ambavyo ni *man made* ambavyo vinaweza kutusaidia kwenye utalii wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo lingine, sijaona mahali ambapo wameelezea au tumeonesha namna makusudi kwamba, sasa hivi hawa watalii milioni mbili tulionao, tuna vitanda kiasi gani na tutakapopata watalii milioni tano, tunao uwezo wa kuwa-*accommodate*? Tunavyo hivyo vitanda? Tuna sera ambayo itasababisha hivyo vitanda vijengwe? Tuwe na hoteli za kutosha na kuwa-*accommodate* hawa watu ambao ni mara mbili pamoja na miundombinu mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango wameelezea vizuri hali ya uchumi kwa *regional integration* zote. Wameonesha *SADC* na *position* yetu, wameonesha *East African Community* na *position* yetu. Sijaona mahali ambapo wameonesha uchumi wetu utawezaje kunufaika kwa kuwa kwenye hizi *regional integrations,*

kwamba, ni kitu gani cha kimkakati cha kuhakikisha kwamba tunahakikisha tunakipata mapema. Kwa mfano, tunakuwa *supplier* wa chakula kwenye *regional integration* (*SADC* pamoja na *EAC*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tuna *position* gani katika *manufacturing* katika hizo jumuiya mbili? Ilitakiwa mpango utuelekeze moja kwa moja. Hapa nikumbushe kwamba wakati tunapambana na *SGR* kwa haraka kuhakikisha inakwenda nchi kama Congo, tukumbuke pia kuna mpango wa kutoa treni kutoa Afrika ya Kusini kuja Angola mpaka Congo. Ni namna gani sisi tutahakikisha ya kwetu inafika mapema na *benefits* tunaanza kuzipata kabla ya hiyo nyingine haijaja? Kwa sababu dunia ni ushindani, sasa hatuwezi kutengeneza reli yetu taratibu wakati *competitor* wameanzia kule Afrika Kusini na wakafika kabla yetu. wakifika kabla yetu watakuwa wamesha-*cement position* yao kwenye hiyo na sisi tutapata shida ya kupata *return* kwenye uwekezaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye sekta za muhimu za Kilimo na Uvuvi. Ninaelewa kabisa juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha haya maeneo ambayo ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu, yanaendelea kuwa imara na yanaendelea kusaidia uchumi. Hata hivyo, kuna eneo ambalo ningetaka kuliona kwenye mpango; kwa mfano, ni namna gani haya mafuriko yanayotokea tunaya-*capitalize* ili kuhakikisha tunajenga mabwawa ya umwagiliaji yatakayosaidia kilimo, maeneo yote ambayo yana umwagiliaji. Pia, kwa mfano, ni namna gani Sekta ya Ngozi ambayo nimeiongelea juzi kwamba, 95% ya ngozi inayotoka kwetu inauzwa *West Africa* kama chakula. Kwa hiyo, maana yake bei yake siyo nzuri kama ingeenda kwenye *manufacturing*. Ni namna gani kwenye uvuvi nako tunahaikisha inakwenda kwenye *manufacturing*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pamoja na mambo mengine ambayo nitachangia kwa kuyaandika, niunge mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Priscus. Mheshimiwa Joseph George Kakunda, atafuatiwa na

Mheshimiwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nianze kwa kutoa pongezi nyingi sana kwa maandalizi ya mapendekezo ya mpango wa mwaka, pamoja na bajeti yake kwa mwaka 2025/2026. Ninaunga mkono kwa sababu wamezingatia vipaumbele vikuu vitatu vya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawakumbusha, kipaumbele kikuu cha kwanza alikitangaza siku alipoapishwa. Alisema, "nikisema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, semeni kazi iendelee." Kwa maana ya kwamba, yeye alikuwa amezamilia kutekeleza miradi yote mikubwa ya kimkakati ambayo ilikuwa imeanzishwa na mtangulizi wake, ndiyo maana akasema kazi iendelee, hivyo hicho ndiyo kipaumbele chake cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele chake cha pili alikuja akakitangaza baadaye kwamba, yeye atazingatia zaidi huduma za jamii kwa maana ya Sekta ya Afya, Elimu, Maji halafu baadaye ndio uchumi. kipaumbele kikuu cha tatu alikuja akakiandikia barua kabisa kwa watanzania, kudumisha amani na utulivu wa nchi. Kwa hiyo, niwapongeze kwamba, kwa kweli mmetembea kwenye vipaumbele vikuu vya Mheshimiwa Rais na mmeweza kutupatia dondoo kwamba, vipaumbele hivyo vinazingatiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikipitia kimoja baada ya kingine, miongoni mwa kazi alizozisema Mheshimiwa Rais kazi iendelee, ilikuwa ni mradi wa ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kwa ajili ya kufua umeme na kusambaza umeme kwa Watanzania, kwa lengo la kuwa na umeme wa uhakika ndani na ziada ya kuuza nje. Pia, niipongeze Serikali kwamba, kwa hatua ambayo imeripotiwa sasa hivi, tunakwenda vizuri na uwezekano wa kuukamilisha kabisa huo mradi katika mwaka huu wa fedha 2024/2025 na mwaka ujao 2025/2026 ni mkubwa sana, Watanzania tujipongeze sana kwa mradi huu kwa sababu ni ukombozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza inawezekana tukapata viwanda vikubwa kwa sababu tuna uwezo wa kuvipata umeme. Hilo ni jambo ambalo limetajwa na wataendelea kulikamilisha, hilo ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa pili ni Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Viwango vya Kimataifa ambayo treni za mwendokasi zitapita humo. Tayari Watanzania wameanza kusafiri kutoka Dar es Salaam - Dodoma na juzi treni ya mchongoko imeanza kuja kutoka Dar es Salaam - Dodoma na kwa kweli imeleta matumaini makubwa sana kwa Watanzania. Hata hivyo, mradi huu bado una vipande vya kuendelea kujengwa, kutoka Makutupora – Tabora; Tabora – Isaka; Isaka – Mwanza; Isaka – Rwanda; Tabora – Kigoma; kutoka Uvinza – Msongati; vilevile Urambo - Mpanda - Kalema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umetajwa kwenye mpango, ninaomba usiishie kutajwa tu Serikali iendelee kutumia mbinu zozote zile ili kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika kwa muda. Mradi huu una faida kubwa sana kwa nchi, wasije wakashindwa na changamoto halafu wakaishia njiani, naomba niwatie moyo kwamba, endeleeni kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalenga kuongeza usafirishaji wa mizigo kutoka tani 200,000 mpaka tani milioni 10 na zaidi. Hiki ni kitu kikubwa sana. Mradi huu ukikamilika tunalenga kuajiri watu 600,000 ambao watakuwa ni *permanent employment*, watu zaidi ya milioni nane watasafiri kwa sababu sasa muda wa kusafiri utapungua kutoka saa zaidi ya 40 kutoka Dar es Salaam – Kigoma hadi saa chini ya 10. Kwa hiyo, ni jambo ambalo ni kubwa sana tunalifanya Tanzania naomba sana kutokana na umuhimu wa miradi hii, Serikali ifanye kila mbinu inawezekana kutekeleza miradi hii kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna changamoto na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuna wakati alilazimika kwenda nchi *guarantors*, siyo lazima nizitaje, kuhakikisha kwamba mradi huu unaendelea kuondoa changamoto ambazo zinajitokeza ili uweze kuendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna Mradi mwingine wa Bomba la Mafuta *(EACOP),* nao ni mradi muhimu sana ambao inatakiwa waendelee kufanya kazi na Nchi ya Uganda ili kuhakikisha kwamba mradi huu nao unakamilika kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanapoona kwamba miradi hii inachelewa kidogo kidogo wanaanza kujiuliza hivi kama nchi *are we serious?* Lazima tuhakikishe kwamba hii miradi ya kimkakakti inakamilika. Wito wangu kwa Serikali ni kwamba, watumie mbinu zozote zile ambazo zinawezekana ili miradi hii ikamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kumung'unya maneno, kwa sababu tumeiona dhamira ya Mheshimiwa Rais katika kuendelea kujenga na kukamilisha miradi hii basi mwakani 2025 ile kauli ya "Mitano Tena" itumike ili kusudi aendelee kusimamia miradi hii iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ambayo iliachwa na mtangulizi wake ni kama vile barabara za lami, madaraja makubwa, viwanja vya ndege, bandari, ujenzi wa meli na vivuko na kadhalika ni sehemu ya kipaumbele cha Mheshimiwa Rais cha "Kazi Iendelee", na tumeona ambavyo utekelezaji unaendelea vizuri. Kipaumbele kikuu cha pili ni cha huduma za jamii, elimu afya na maji. Huyu ni Rais pekee ambaye ametoa fedha nyingi katika kipindi cha miaka mitatu na nusu tu iliyopita kuliko Rais yoyote ukilinganisha takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe mfano, katika Halmashauri ya Wilaya yangu ya Sikonge fedha za elimu pekee imepokea zaidi ya bilioni 19 katika kipindi cha miaka mitatu na nusu, haijawahi kutokea. Ni jambo ambalo Mheshimiwa Rais analitilia mkazo sana. Isipokuwa kuna changamoto zake ambazo ni muhimu sana ziwe kwenye mpango. Kwa mfano, wenzangu wamezungumza kuhusu maboma ya madarasa, mabweni, zahanati na vituo vya afya. Sisi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tunakwenda vijijini tunatembelea wananchi na tunaona jinsi ambavyo wananchi wanakuwa wamejitolea nguvu kwa kweli naomba sana nguvu za wananchi zisipuuzwe kwenye mpango.

Ziwepo kwenye mpango na ionekane kabisa kwamba Serikali imedhamiria kukamilisha maboma ambayo yalianzishwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha tatu cha Rais ni amani na utulivu. Sitaki kuzungumza sana kwenye eneo hilo kwa sababu inafahamika jinsi ambayo wanaendelea kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za jumla; ajira ni changamoto kubwa sana. Tumejenga madarasa, afya na zahanati, lakini ujenzi wa *infrastructures* uliofanyika haulingani na watumishi walioko kwenye shule, kwa maana ya walimu katika ngazi zote; msingi, sekondari, vyuo vya ufundi, vyuo vya maendeleo ya wananchi *(FTC),* vyuo vingine vya kati na vyuo vikuu kote kuna shida ya walimu. Maeneo haya yote yanahitaji mkakati kabisa ambao utabuniwa hata kwenye ngazi ya Baraza la Mawaziri kwa sababu ukimuuliza Waziri wa Fedha atakwambia mimi nalia kwa sababu ya *wage bill.* Hii *wage bill* ni lazima watafute njia za kurekebisha ili watu wapate huduma iliyotarajiwa na zile *infrastructures* ambazo zimejengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya ushauri ni mawili tu; Mpango unazungumzia sana kuhamasisha uwekezaji. Hatuwezi kuhamasisha uwekezaji kama hakuna ardhi ya uwekezaji *(land bank)* na ardhi ya uwekezaji haiwezi kupatikana kwa sheria ya sasa hivi ya vijiji, ardhi inamilikiwa na vijiji na ardhi ikimilikiwa na kijiji huwezi kupata *tittle deed.* Ninaomba sana Sheria ya Ardhi ifanyiwe marekebisho ili tuweze kupata ardhi ya uwekezaji *(land bank)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kukamilisha miradi ambayo ilianza kutekelezwa zamani kwa mfano, Barabara yetu ya Mwanza – Tabora - Ipole - Mbeya haijakamilika. Ninaomba Serikali waweke kipaumbele kwenye barabara hiyo ili ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, hili la barabara nitawafuata Waheshimiwa Mawaziri tuongee vizuri. Ninashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph George Kakunda, ninakushukuru sana. Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nami fursa hii. Ninaomba kwanza nami nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Profesa Kitila Mkumbo na Dkt. Mwigulu na Naibu Waziri Mheshimiwa Nyongo na watendaji wao wote wa Wizara zao zote mbili kwa kuandaa vizuri mpango huu na pia kwa mwongozo wa bajeti 2025. Tunawashukuru sana na hongera sana kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaipongeza sana Serikali chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Pamoja na changamoto zilizopo duniani huko, lakini pato la Taifa limeendelea kukua kwa 5.1% mwaka 2023. Kwa taarifa hii tuliyosomewa hapa pato la Taifa kuanzia Januari hadi Juni limekua kwa wastani wa asilimia 5.4, lakini kwenye ripoti ya Tanzania *Economic Outlooks* inasema kwamba *real GDP* 2024 itakuwa 5.8. Kwa hiyo hongera sana kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye taarifa zao pia wamesema kwamba tunatarajia pato la Taifa kukua kwa mwaka 2025 wastani wa 5.8 mpaka 6.1 ambayo itakuwa 2026. Ukuaji huu wameeleza kwamba unategemea utekelezaji endelevu wa miradi ya kimkakati; na miradi hii kimkakati wameeleza kuwa ni ya ni miundombinu ya nishati, miundombinu ya barabara, kuongeza mikopo sekta binafsi na kuendeleza sekta zingine na mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuzungumzia kuhusiana na kuendeleza miundombinu ya nishati na barabara. Ni kweli kwamba wameuona umuhimu wake na ili uchumi uendelee na pato la Taifa liendelee kukua hatuna budi kuimarisha maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi nilizungumza hapa, niliuliza swali kuhusiana na mradi wa umeme wa njia kubwa ambao unatoka Songea – Namtumbo – Tunduru – Masasi

unaenda mpaka huko kwingine Mtwara; kwamba ni kwa nini umesimama. Hili walilolisema hapa, kwamba ukuaji wa uchumi unategemea pia miundombinu hii ya umeme; lakini mradi ule sasa hivi umesimama kwa sababu hawajalipwa fedha, lakini pia watu ambao wamepitiwa na mradi ule nao hawajalipwa fidia. Vilevile, mradi huu watu wenyewe wanaopitiwa kutoka Songea mpaka Masasi fidia yake ni bilioni mbili tu na milioni mia nne; na wamebaki wako na taharuki, kwamba mwaka huu wakalime wapi. Walitegemea wakilipwa hizo hela waende wakatafute maeneo mengine wakakate pori lingine ili waweze kulima; sasa mpaka leo hazina haijawalipa hela. Kwa hiyo tunaomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapochelewesha miradi kama hii pia wanawachelewesha watu kiuchumi na pia tutachelewesha ukuaji wa pato la Taifa kama wenyewe walivyosema hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu makadirio ya bajeti ya mwaka 2025/2026. Serikali wamesema hapa kwamba inatarajia kukusanya mapato kutoka vyanzo vyote vya jumla ya trilioni 55 na bilioni 61 huku mapato ya ndani yatakuwa ni trilioni 38.962. Dhamira hii ni kuhakikisha kwamba mapato ya ndani yanagharamia bajeti kiasi cha 70%. Ninaipongeza sana Serikali kwa sababu *projection* hizi ni nzuri, lakini pia kugharamia bajeti ya Serikali kwa 70% ni jambo kubwa sana; tumetoka mbali. Ninakumbuka wakati tunaingia hapa Bungeni na akina Mzee Mkuchika na akina Mzee Ole-Sendeka, Serikali ilikuwa na uwezo wa kugharamia 27% mpaka thelathini na kitu, lakini leo wanazungumza kwamba Serikali itaenda kugharamia bajeti mapato ya ndani zaidi ya 70%, hii ni pongezi kubwa sana kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye fedha hizo, jumla ya kiasi hicho trilioni 65, kama tulivyosema, makusanyo ya ndani trilioni 38, lakini kati ya hizo trilioni 38 za makusanyo ya ndani wamepanga kwamba zitatumika hizo trilioni 38 kwenye matumizi ya kawaida halafu matumizi ya maendeleo ni trilioni 16. Sasa ukitazama hapa utaona kabisa kwamba zile trilioni 16 ni zile ambazo tunaenda kukopa zote kwenye mikopo nafuu na mikopo ile ya ghali pamoja na misaada kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba lazima wataalam tuangalie hapa; uchumi duniani umebadilika, kwa maana ya kwamba kuna *inflation* kubwa sana huko juu na wenzetu sera yao kubwa ya kupunguza *inflation* ni kuongeza riba ya mikopo kiasi kwamba sasa hivi mikopo ina riba ya juu sana. Sisi hapa tunategemea kwenda kukopa huko takribani trilioni 15 kwenda 16 ya bajeti yetu, maana yake ni nini? Tunakwenda kukopa kwenye riba kubwa. Kwa hiyo, tuangalie hizi hela za ndani matumizi yake yawe ambayo yanastahili ambayo yatawezesha kupunguza gharama ya kuendesha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wizara za kisekta watu wa mipango waangalie Wizara za kisekta zinapokwenda kupanga matumizi ya fedha za bajeti zao, wapunguze gharama zisizokuwa za msingi ili kuhakikisha kwamba tunapunguza mzigo wa Serikali wa kwenda kukopa ili fedha zingine hizi ziweze kusaidia katika miradi ya maendeleo ya ndani. Kwa sababu hapa inaonesha kwamba hela nyingi za mapato ya ndani tutakwenda kutumia kwenye matumizi ya kawaida. Ndiyo, utaniambia matumizi ya kawaida, ni kweli, inalipa kwanza mikopo, inatoa mishahara na pia inagharamia shughuli za Serikali. Sasa hapo inapogharamia shughuli za Serikali matumizi yake katika mpango huu ni lazima yaangaliwe ni ya aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine ni kwenye makusanyo; mtazamo pia wa *revenue reforms.* Tunashukuru sana Mheshimiwa Rais alivyounda Tume hii ya kuchukua maoni kwa wananchi mbalimbali, kwa walipakodi mbalimbali pia na kwa wasiolipa kodi. Ninaamini kabisa kwamba Tume hii itatufanyia kazi nzuri sana; ni hatua nzuri sana kwa sasa hivi. Ninaomba tuiunge mkono ili ifanye kazi yake vizuri, ije na matokeo chanya ya kuongeza wigo wa kukusanya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine pia ni eneo la miamala ya fedha katika simu zetu au katika *mobile money transactions.* Kuna ongezeko kubwa sana la miamala ya fedha katika simu; eneo hili linaonyesha linafanya kazi vizuri sana. Katika muda huu tu wa mwezi Agosti miamala milioni 310 ya fedha kwa kutumia simu imefanyika. Kwa hiyo eneo hili tunatakiwa tuliangalie vizuri sana na kiutalaam. Hili ni eneo zuri sana la kukusanya fedha.

Kwa mfano, ukikusanya *average* shilingi 1,000 kwa muamala mmoja ni bilioni 310. Kwa hiyo eneo hili nalo lazima tuliangalie sana katika kuongeza mapato ya Serikali, tusilionee haya, tusiliache hivi hivi, eneo hili lina *transaction* nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunatumia sana simu, ukiweka hela kwenye simu mara imekwisha. Kwa hiyo ni lazima Serikali iangalie kitaalam hasa katika eneo hili, kukusanya fedha ili kuweza kuongeza mapato kwa Serikali. Kwenye eneo hili *mobile money account* zimekua kwa asilimia 116. Mwaka 2019 tulikuwa na *account* milioni 25.8, lakini tunapozungumza hapa leo tuna *account* 55.8. Kwa hiyo hili ni ongezeko kubwa sana la *account* kwenye eneo hili, hili eneo tuliangalie kwa maana ya kuchukua pato letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwamba, ni lazima tuangalie sana kuwaendeleza wananchi wetu vijijini katika uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umewasha *mic* basi naomba kuunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa kwa kujali, ninakushukuru sana pia kwa mchango wako.

Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatia Mheshimiwa Hussein Nassor Amar na Mheshimiwa Athuman Almasi Maige ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia mpango wetu wa mwaka mmoja. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mipango, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Vilevile niipongeze sana Kamati ya Bajeti kwa kutupa maelekezo ambayo kwa kweli yametusaidia sana katika kutuonesha wapi tunakokwenda na vile ambavyo ni vipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza niipongeze Serikali, kuna mabadiliko mengi sana ambayo yamefanyika. Niseme wazi kabisa kwamba Serikali yetu ni Serikali ambayo inajali

matatizo ya watu. Mambo mengi sana ambayo yamefanyika kwenye utekelezaji wa Ilani, lakini pia kwenye mipango mingine iliyopita yalijikita kwenye maendeleo ya watu na kutatua changamoto za watu. Kwa hiyo, niipongeze sana Serikali yetu kwa kazi kubwa ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Baba wa Taifa alisema kwamba, maendeleo ya kweli ni maendeleo yanayojihusisha na watu na sisi Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ni Serikali ambayo imekuwa inajihusisha na changamoto za watu. Kwa hiyo, nina kila sababu mimi kama Mbunge kijana kujivunia Serikali yangu kwa kazi kubwa ambayo imeifanya, lakini pia kwa malengo ambayo imekuwa ikiyafanya mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwenye mambo mawili kwenye kuzungumza. La kwanza litakuwa ni suala la Wizara ya Habari na Mawasiliano, lakini la pili itakuwa ni Wizara ya Nishati, haya mambo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye haya mambo mawili jambo la kwanza ninaanza na Wizara ya Habari na Mawasiliano. Kwanza nimpongeze Waziri wa Habari Mheshimiwa Jerry Silaa kwa kazi nzuri ambayo anaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeusoma mpango huu na 90% ya kinachozungumzwa humu ndani kinazungumzia uchumi wa kidigitali. Uchumi wa kidigitali ni uchumi ambao unabebwa na Wizara ya Mawasiliano kwenye hatua kubwa na kwenye mambo mengi, kwa maana teknolojia na upatikanaji wa mawasiliano ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kwenye vipaumbele vya Serikali kuna uchumi wa kidigitali hapa wanauzungumzia lakini pili wanazungumzia kuboresha ukusanyaji wa mapato. Niseme, Mheshimiwa Waziri wa Habari na Mheshimiwa wa Mipango hatuwezi kujadiliana kwenye Taifa hili mipango mingi ya ukusanyaji wa kodi mipango mingi ya kuhakikisha kwamba Taasisi za elimu zinakua na mipango mingi ya kuhakikisha kwamba mifumo ya Serikali inasomana kama tutakuwa hatuna uhakika wa *access* ya *internet* kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Access* ya *internet* kwenye Taifa letu ndio msingi wa maendeleo ya sasa; kwa sababu asilimia inazungumzwa hapa zaidi ya watu milioni 36 kwenye Taifa letu wana *access* ya *internet,* lakini milioni 12 tu wanatumia *2G* siyo *3G* wala siyo *4G* wala siyo *5G* kwa maana kwamba *internet* yenye *speed* kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni nini ninachotaka kukizungumza na nini ambao ni ushauri wangu. Nimezungumza hapa na nimesoma kwenye ripoti ya Kamati. Wanasema, kuimarisha mradi wa ujenzi wa minara, lakini pia wanasisitiza sana kuongeza matumizi ya teknolojia ya akili bandi (*artificial intelligence)* katika Taasisi za Serikali. Hatuwezi kujadiliana *artificial intelligence* kwenye Taifa ambalo *internet* iko chini kwa kiwango ambacho mambo mengi ya Serikali yanakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Watanzania kwenye kukusanya kodi unakwenda kulipia kodi taarifa utakayopewa ni kwamba mtandao upo chini. Utakwenda kusoma kwenye *online course* utaambiwa leo huna *access* ya *internet* lakini pia unaweza ukasafiri kutoka hapa kwenda Dar es Slaam ni maeneo mawili au matatu tu ndiko kutakuwa na uhakika wa kupata *internet the rest there is no internet,* sasa nini lazima kama Serikali ikifanye? Hatuwezi kujadiliana kwamba tusubiri miaka mitano, hatuwezi kujadiliana kwamba tusubiri miaka mwili. *Internet* ni kitu ambacho kiko sasa ambacho kinatumika hata dakika hii. Kwa hiyo ni muhimu Serikali ikafanya kazi kubwa kwenye kuimarisha misingi au mifumo ya upatikanaji wa *internet* nchini na hili niliombe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 90% ya vijana wamejiajiri na wamejiajiri wako mitandaoni wako kwenye maduka ya mitandaoni wanauza vitu. Hawa watu wanapokosa *internet* wanakuwa wamekosa mambo mengi na baadaye na sisi tunakuwa tumekwamisha shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, kuna mambo kwa mfano aliyazungumza Kamishna wa Ushindani wa Kenya, anaitwa David Kemei alisema: "*Ujio wa Star Link ni kwamba utalazimisha kampuni na huduma za mawasiliano katika Nchi ya Kenya kufanya kazi*

*kwa ubunifu. Tunataka kampuni za ndani zitikiswe ili zitoe huduma katika ubora wake*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe hatuzungumzii kwamba lazima twende kule *Star Link,* tunachotaka ni kuwa na uhakika wa *internet* kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo wakati Waziri akiwa Mheshimiwa Nape Nnauye, alisema: "*TTCL mmejikita kwenye kujenga na kusimika minara, mnapambana na makampuni ya Voda na ya Tigo mmeacha fursa ya kutumia fiber, Mkongo wa Taifa kuusambaza zaidi ili kupatikana kwenye nchi yetu ili internet iwe ya uhakika na Taifa letu liweze kusonga mbele*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana Wizara ya Mipango hili jambo ikaliongelea kwa ukaribu sana na ikachukua hatua za haraka kuhakikisha tuna uhakika wa upatikanaji wa mawasiliano nchini *especially* kwenye mawasiliano ambayo yamechukua zaidi ya 88% ya Watanzania wanaotumia simu na wana *access* ya *internet*. Kwa hiyo, Wizara ya Mipango lazima iliangalie hili jambo kwa haraka, kwa sababu sasa hivi kodi ya Taifa hili inakusanywa kwa kupitia mfumo, lakini Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza mifumo lazima isomane. Tatu, tumekuwa tunafanya hadi *operation.* Ukisoma ripoti za Muhimbili zinazungumza. Kuna mambo ya *operation* yanafanyika yanatokea kwenye mataifa mengine kwa kutumia mifumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokosa uhakika wa mifumo kuna vitu vingi vinadondoka na kukwama. Utashindwa kukata tiketi, unataka *SGR* ifanye kazi, tiketi zinapatikana. Tunataka *ATCL* ifanye kazi, yote hii ni mitandao. Kwa hiyo, ni muhimu sana Wizara ya Mipango ikahakikisha kwamba inalifanyia kazi sana hili suala la upatikanaji wa *internet* kwenye Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mataifa ya jirani yameshatuacha. Kwa hiyo, sisi kwa sababu *digital economy* yetu imebebwa na *internet,* ni vema Waziri wa Mipango na Waziri wa Sekta husika wafanye kazi kubwa kuhakikisha kwamba *internet* inapatikana kwa uhakika kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* amezungumza, moja kati ya changamoto inayoikumba *TTCL* ni kushindwa kutumia fursa. Fursa waliyonayo ni upatikanaji wa mkongo wa Taifa ambapo wao wana mamlaka nayo. Kwa hiyo, ni vema wangelifanyia kazi hilo jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambapo nataka kushauri kwa niaba ya wananchi wa Makete ni suala la nishati. Ukisoma ripoti ya Kamati na ukisoma mipango ya Serikali, moja kati ya mpango mkubwa ni kuongeza uzalishaji viwandani (bidhaa za viwandani), lakini pili, kwenye uwekezaj; hatuwezi kuimarisha uwekezaji kama nishati itakuwa siyo ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali, naipongeza Wizara ya Nishati kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya kuhakikisha kwamba upatikanaji wa nishati kwenye Taifa letu umekuwa ni mkubwa na inapatikana vizuri. Hata hivyo, tusijisahau, alipokuja Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko pale Makete alisema: *"Moja ya changamoto kubwa tuliyokutana nayo kama Taifa, tuli-relax kuongeza vyanzo vingine vya kuzalisha umeme, tukawa tumetulia ndiyo maana baadaye tukapata hii changamoto kubwa ya kukosekana kwa umeme."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali, tuna vynazo vya umeme. Ukiangalia ukiwa unatoka Dar es Salaam unaelekea Moshi utakuta vibao vimeandikwa kuna upepo mkali. Serikali lazima itumie fursa ya kuvuna umeme kupitia upepo. Ukienda Singida kuna changamoto hiyo, kwamba tuna mradi mkubwa wa uzalishaji umeme kwa kutumia upepo, lakini haujafanya kazi hadi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ambaye natoka Makete tuna Bwawa la Rumakali ambapo Serikali inakusudia kwenda kuhakikisha kwamba inazalisha umeme. Naiomba Serikali wakati wowote tuna haja ya kuwa na umeme wa kujitosheleza kwenye nchi yetu. Kwa hiyo, ninaomba kama tunakwenda kuboresha uzalishaji wa umeme ni vema kwenye yaleyale maeneo kama ni Makete kwenye eneo la Rumakali fidia zilipwe kwa wakati ili miradi ianze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi, kwa jinsi ambavyo Serikali ya Mama Samia imesambaza umeme vijijini kwenye *REA* tuna haja kubwa sana ya kuwa na umeme wa uhakika, kwa sababu unavyosambaza umeme kwa wingi ndivyo pia ambavyo unatengeneza maendeleo yawe ni makubwa. Mfano mkubwa ni huu, Mgodi wa *Geita Gold Mining* ni mradi ambao kwa muda mrefu ulikuwa hautumii umeme wetu ndani ya nchi. Ni kwa sababu walikuwa hawana umeme wa uhakika, lakini kwa sasa Serikali yetu imefanikiwa wanatumia umeme wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa mgodi mmoja tu wa Geita ni sawasawa na umeme wa Mikoa miwili ya Njombe na Iringa kwenye matumizi. Kwa hiyo, kama tunaenda kuwekeza kwenye viwanda na kama tunaenda kuwekeza kwenye migodi lazima tuongeze uzalishaji wa umeme kwenye Taifa letu, ni muhimu sana. Niiombe Wizara ya Nishati kwamba kwa sababu tuna miradi mikubwa kama *SGR,* pia tuna migodi na Mheshimiwa Rais amekuwa akivutia sana wawekezaji kwenye Taifa letu, ukisomo kwenye ukurasa namba 25, ni vema tukawa na umeme wa uhakika ili wananchi wetu waweze kuwa na umeme wa kujitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa alisema maendeleo ni maendeleo ya watu. Kwa hiyo, tukijishughulisha na shida za watu mojawapo ni kupatikana umeme wa uhakika kwenye makazi yao. Hayo yalikuwa ni mawazo yangu na naiomba sana Serikali iyafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni upatikanaji wa *internet* ya kujitosheleza kwenye nchi. Pili, nishati ni muhimu sana kupatikana kwenye Taifa letu. Najua kwamba Serikali imekusudia kufanya mambo makubwa; sisi tunaiunga mkono *and I am very proud of my country, especially* utendaji wa Mheshimiwa Rais wetu. Mheshimiwa Rais wetu anatufanya mtaani leo tunajivunia na tunatembea tunatamba ni kwa sababu amefanya kazi kubwa kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nawatakia kila la heri watu wa Mipango. Sisi kama Wabunge tuko tayari kuwaunga mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Festo Richard Sanga, nakushukuru sana pia kwa kuheshimu muda.

Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, atafuata Mheshimiwa Athuman Almas Maige na Mheshimiwa *Engineer* Samweli Xaday Hhayuma ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu na kuweza kuchangia. Pia, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha nyingi sana kwenye miradi ya maendeleo nchini na Nyang'hwale ikiwa ni miongoni mwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale Mama hatumdai; yeye anatudai na tunasema tunaenda na mama 2025. Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mambo makubwa sana kwenye Jimbo la Nyang'hwale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla kuingia kwenye mchango wangu na ushauri naomba angalau niyaseme machache ya kumpongeza mama. Kwa nini sisi Wananyang'hwale tunampongeza? Mama ameweza kutoa fedha nyingi sana kwenye miradi ya maendeleo. Fedha hizi zimeenda kwenye miradi ya maendeleo ikiwemo kwenye Sekta za Elimu, Maji, Barabara, Afya, Umeme, Mawasiliano ya Simu, *TASAF,* Ujenzi wa *VETA*, Kilimo, Madini pia mikopo ya 10% kwa wanawake, vijana pamoja na wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja kubwa sana ambalo ni kama miujiza ametufanyia sisi Wananyang'hwale. Ameweza kutenga fedha kwa ajili ya kutujengea daraja ambalo lilibomoka zaidi ya miaka 40 iliyopita. Mama Samia ameweza

kututengea fedha kiasi cha shilingi milioni 573. Daraja hili linaenda kukamilika mwezi wa 12. Baada ya miaka 40 mama ameweza kutoa fedha; Mama hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, ameweza kutujengea kilometa moja ya lami kwenye Makao Makuu ya Wilaya yetu ya Nyang'hwale kwenye Mji wa Kharumwa. Baada ya kuyasema haya nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Mheshimiwa *Professor* Kitila Mkumbo, kwa hotuba yake nzuri ya mipango ya maendeleo ya 2025/2050. Ni mipango mizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba kwa mwongozo wake na kwa maelezo mazuri aliyotupa kwa hatua ambayo tumeifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, sasa nijielekeze kwenye mchango wangu kwa kifupi. Mchango wangu huu unaelezea mpango huu. Kuna baadhi ya mambo ambayo mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo nla Nyang'hwale na Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna maeneo ambayo nataka nishauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mpango ni mzuri lakini kuna maeneo ambayo nikiyaangalia ukusanyaji wa mapato bado haujawa mzuri kwenye baadhi ya maeneo. Mfano, kuna watu ambao wamepewa majukumu haya kwa ajili ya kuisaidia Serikali kukusanya fedha ikiwa ni watumishi wa *TRA* na wafanyabiashara. Kumekuwa na ujanja unaofanyika wa kulipotezea Taifa hili mapato makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kweli inabidi tutangulize uzalendo mbele. Tuseme haki japokuwa tutalaumiwa, lakini ukweli lazima tuseme. Kwa nini nasema kwamba kuna uvujaji wa makusanyo ya fedha za Serikali? Leo hii utaona vijana wetu ambao wameaminiwa na Taifa hili hasa wa *TRA* wamekuwa wakishirikiana na wafanyabiashara ambao siyo waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wa *TRA* siyo wote wabaya, lakini wamo ambao ni vijana wameingia mle kwenda kupiga na kujinufaisha wao na siyo kulinufaisha Taifa. Nitatolea mfano kidogo. Utakuta kuna baadhi ya wafanyabiashara wanapofanya biashara zao hawatoi risiti. Vijana wa *TRA* unawaona wanapita kwenye maeneo hayo na hayo yanafanyika na hawachukui hatua. Kwa hiyo, katika ushauri wangu huu naomba, nitakapofika mwisho wayachukue wayafanyie kazi, kwa sababu nimekuwa nikichangia mara kwa mara na kutoa ushauri huu, lakini sioni kama unafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii unaweza ukaenda dukani ukanunua mali yenye thamani hata ya shilingi laki tano, tajiri mwenye duka au muuzaji anakuuliza, unataka risiti nikupe bei ya risiti au bei ambayo siyo ya risiti? Utakaposema nataka bei ya risiti, wakati wa kutoa risiti, hatoi risiti inayolingana na fedha ambayo umeilipa; umelipa shilingi laki tano, unakatiwa risiti ya shilingi laki mbili. Haya yanafanyika. Je, ndani ya *TRA* hakuna kitengo cha kufuatilia mambo haya? Kwa hiyo, ili tuweze kuendelea kukusanya pato la Taifa, nashangaa Mheshimiwa juzi hapa anasema tunakusanya fedha nyingi, lakini nikiangalia kuna fedha nyingi bado tunaziacha kule nje. Leo hii *TRA* inakusanya zaidi ya shilingi trilioni mbili, lakini kuna shilingi trilioni mbili au zaidi tunaziacha kule nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, naomba sana wauchukue. Watengeneze utaratibu ulio mzuri wa kuongeza hii faini ya shilingi milioni mbili/milioni tatu, naona si chochote si lolote, kwa sababu unayemtengenezea sheria ya kumpiga faini shilingi milioni mbili wakati amekuibia shilingi bilioni moja, tofauti yake ni kubwa sana. Naomba sana hili jambo wajaribu kulifuatilia kwa vijana wetu wa *TRA*, pia, wafanyabiashara wetu wanakuwa siyo waminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nishauri, kwa nini kumekuwa na tofauti kwenye hizi biashara zetu? Tuchunguze ni kwa nini? Leo hii unakuta mimi ni mfanyabiashara, tunatoa mzigo China makontena yetu ni mawili, tumepakia mali inayofanana. Makontena ya *40 feet* yote mali iliyomo mle inafanana na tumenunua kiwanda kimoja na tumesafirisha meli

moja, tunakuja kufikisha bandarini mzigo huo *agent* wetu wanaotoa mzigo inakuwa huyu anachukua *agent* wake na nachukua *agent* wangu. Unakuta huyu analipa shilingi milioni 40, huyu analipa shilingi milioni 20 kwa mali ileile. Hivi hamlielewi hilo? Hebu jaribuni kufuatilia. Haya yapo yanafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hili linaumiza. Nimeshachangia na kutoa ushauri huu tangu wakati ule wa enzi ya Waziri wa Fedha, Waziri Mpango, nilishalizungumzia hilo lakini sioni kama hatua zinachukuliwa. Madukani huu utaratibu unaendelea. Leo hii nenda kwenye baadhi ya vituo vya mafuta, unafika pale unajaza mafuta anakwambia bwana mashine ni mbovu. Tangu asubuhi anauza ila anasema mashine ni mbovu. Hamlielewi hili kwamba huu ni upotevu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, wafuatilie kuna maeneo mbalimbali nendeni kwenye vituo vya mabasi na nendeni kwenye magari yanayosafirisha mizigo. Magari yanapakia mizigo hawatoi risiti na wakitoa risiti wanatoa risiti za mkono, kwa nini? Nendeni kwenye mabasi, unaenda kusafirisha mzigo gari linajaa chini mzigo zaidi ya shilingi milioni tano ama sita lakini hawatoi risiti na wakitoa risiti wanatoa za mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, kwa nini Serikali isichukue maamuzi kuagiza mashine za *EFD*? Mashine hizo ziletwe kwa gharama nafuu, wafanyabiashara wote wakopeshwe walipe kidogokidogo ili wawe na *EFD machine*. Tuondoshe lile suala la kwamba inatakiwa huyu mwenye shilingi milioni 100 ndiyo awe na mashine na huyu ana shilingi milioni 50 asiwe na mashine. Hii inaleta upotevu wa fedha za Serikali. Walete mashine, wahakikishe mtu yeyote anayekuwa na leseni ya biashara awe na mashine ya *EFD* ili tuweze kukusanya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato haya yanapotea. Ukiangalia mfano katika maeneo mbalimbali nchini, nenda maeneo mbalimbali kwenye maduka hawatoi risiti. Hizo pesa zinakwenda kupotea bure. Naiomba Serikali yangu sikivu ichukue ushauri huo wa kuweza kuagiza hizo mashine kutoka kiwandani kwa gharama nafuu na kuwakopesha wafanyabiashara kwa gharama nafuu ili waweze kulipa kidogo kidogo. Pia, wote

ambao wana leseni za biashara wasajiliwe kwenye mfumo huo wa ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho naishauri Serikali, kwa nini isipunguze ongezeko la *VAT* 18% angalau basi turudi kwenye 14% ili watu wengi wawe na hamu ya kuingia kwenye mfumo huu wa *VAT?* Mwisho, nimewahi kuishi Malaysia, ndugu Waheshimiwa nchi ile hata ukienda kula mishkaki...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba hitimisha muda umeisha.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukienda kula mishkaki ya shilingi 1,000, itaandikwa 1,000 na shilingi 100 chini pale kodi ya Serikali. Hebu tutenge fedha kwa ajili kutoa elimu, kuwaelimisha wananchi wetu kwa ajili ya kujua nini maana ya kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Nassor Amar kwa mchango wako.

Mheshimiwa Athuman Almas Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Samwel Xaday Hhyuma na Mheshimiwa Tumaini Magessa ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu nichangie hoja hii ya Mpango wa Taifa. Mpango huu una vipaumbele vyake na vipaumbele hivi wamechagua vichache ambavyo ni muhimu; kuchochea uchumi, kuimarisha uwezo wa viwanda, kukuza uwekezaji wa biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza ujuzi (elimu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha mpango huo ni lazima tuwe na programu ya Kitaifa. Napendekeza programu hiyo ianze na chakula. Chakula ni kitu muhimu sana. Kwa hiyo, kuwa

na chakula cha kutosha cha kuwatosheleza Watanzania wote kwa kutumia kilimo chetu wenyewe halafu kinachobaki tuuze nje kupata fedha za kigeni ni jambo la muhimu sana katika mpango wetu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo cha umwagiliaji, tuna bahati sana kumpata Waziri Bashe. Kwanza, yeye mwenyewe anafanya kilimo cha umwagiliaji, ameanzisha mpango mzuri. Pia, ameng'ang'ania kuanzisha mabwawa ya umwagiliaji; haya yataleta uchumi mkubwa sana. Wakulima wakiweza kulima zaidi ya mara tatu au mara mbili kwa mwaka italeta tija ya ukuzaji wa chakula katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo la ardhi. Sasa hivi ni tabu sana. Ukisema upate uwekezaji wa ekari 1,000 au 2,000 za kulima shamba, hakuna. Serikali itenge ardhi ya kilimo na ijulikane kwamba ardhi ya kilimo iko hapa na anayetaka kuwekeza awekeze hapa na ijulikane na itunzwe kama tunavyotunza hifadhi za wanyama; iwepo ardhi ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la nishati, amesema Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa kwamba umeme mkubwa utakaotoka Bwawa la Mwalimu Nyerere. Sasa naambiwa mashine mbili au tatu zimewashwa. Zile mashine tisa zikiwashwa zote kutakuwa na umeme mwingi sana. Tusiutumie kuwasha taa na kuuza wenyewe kama rejereja au chukuchuku. Umeme ule kuanzishwe viwanda vikubwa vya uchakataji wa kibiashara ili tuweze kuzalisha mali ambayo tutauza nje tupate fedha za kigeni. Suala la kupoteza dola moja moja hapa nchini na kwa mkasa mkubwa litaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika mpango huu kuna kitu kinaitwa ufuatiliaji, uthamini au tathmini na vihatarishi, lakini. sikuona mahali palipoandikwa *research and development (R and D);* lazima kuwe na utafiti na uendelezaji. Mataifa yote yaliyo juu kabisa kiteknolojia na yamepita vikwazo vingi vya uchumi yanafanya *research and development.* Bila kufanya hilo katika mpango huu tutajikanyaga. Lazima kuwe na mpango ambao unaonekana kwamba tunafanya utafiti na uendelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu, nina furaha sana elimu tulipofikia siyo pabaya, lakini tunaifanya juu juu mno. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuletea hela nyingi tumejenga madarasa na mabweni, lakini limetokea tatizo la makazi ya walimu na walimu hakuna. Vijijini anapelekwa Mwalimu, lori la halmashauri linampeleka darasani; umefika saa 12 jioni teremka; hapa ndipo umeletwa, hakuna nyumba ya Mwalimu na hakuna chochote. Asubuhi yake Mwalimu anapaki mizigo anaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule tunazo ila hazina walimu. Nashauri bajeti ya elimu iongezwe ili kuwepo na miundombinu na huduma za walimu ziwepo shuleni. Tunasema elimu ni ufunguo wa maisha na ufunguo uko shuleni. Kama huko shuleni ni jalala, hauwezi kuwa ufunguo mzuri. Ni lazima iwe shule inayotambuliwa kwamba ni shule ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, liko tatizo moja, nami naumia sana, Bunge linakaa kujadili choo, matundu ya vyoo mpaka tunaomba msaada wa matundu ya vyoo. Hebu mpango huu uondoe suala la matundu ya vyoo katika msamiati wa Hazina na bajeti yetu. Vyoo vya watoto wa shule ni jambo baya sana, tuongelee madawati kwa sababu watoto wameongezeka, tumejenga shule, madawati sawa, tatizo la matundu ya vyoo linaweza kuondoka kabisa kama tuko *serious*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji ni jambo kubwa sana kuleta maendeleo kwa wananchi, wananchi wanazurura kutafuta maji maana hayana mbadala. Itakuwa jambo zuri sana kama mpango huu utakazana kuleta maji kama ambavyo ipo na kukuza kiasi cha maji yanayopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nafurahia sana miradi iliyokamilika kama *SGR*, Bwawa la Mwalimu Nyerere, madaraja, meli zilizojengwa, Daraja la Magufuli. Ninampongeza sana Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, amejikita katika kuendeleza kufanya mambo yaonekane, hili litatusaidia sana, lakini nina jambo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *TRC* liwe *corporate* shirika pale juu, liwe na kampuni mbili, ya *SGR* na *MTR*, itaenda vizuri kuliko sasa, shirika limekuwa moja linaendesha reli mbili. Itakuwa jambo la maana sana kama kutakuwa na mashirika mawili ya kuendesha shirika letu la reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mashirika, taasisi au sekta zinazotoa huduma, ni sekta muhimu, lakini Serikali haioni umuhimu wake. Sekta ya ulinzi binafsi nchini ina miaka 44 leo tangu ianzishwe haina kanuni wala sheria, wana uwezo si mnawaona?

Mheshimiwa Mwenyekiti, polisi ni wachache askari zaidi ya 560,000 nchi nzima na kampuni zaidi ya 3,000 yapo, yanakusanya hela kiasi gani? Hakuna mfumo wowote, polisi wanatoa vibali mwisho leo polisi wenyewe wamejianzishia kampuni ya ulinzi, tazama sasa, si *conflict of interest*? Italeta mgongano wa maslahi maana polisi wanatoa vibali vya kampuni za ulinzi, leo na wenyewe wamejipa kibali. Lazima sheria ya sekta ya ulinzi nchini itungwe, ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote duniani kuna sheria ya sekta ya ulinzi katika nchi husika. Sasa hivi inashindikana, kampuni zote za *security* Tanzania hazina viwango kwa sababu hakuna mamlaka ya ku-*certify* kwamba kampuni hii ni *group* gani na hii ni daraja gani. Matokeo yake kazi zote za kimataifa kampuni za Tanzania marufuku, hazina viwango na vipimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nami ninafurahi sana na hii Sekta ya Afya inavyojengwa na Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuanzia hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati pia. Ninaomba, ninasali, vitendea kazi vyote katika hospitali hizi na zahanati viwepo kama ambavyo tumekusudia. Itafanya watu wawe na afya nzuri, watibiwe vizuri na wataipenda Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa muda huu na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Athuman Almas Maige. Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma, atafuatiwa na

Mheshimiwa Tumaini Magesa ambaye ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia kwenye Mpango wetu wa Maendeleo ya Taifa letu 2025/2026. Ninaanza mchango wangu kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameturuzuku uhai na hatimaye tunaweza kuchangia yale ambayo tumeyaandaa kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimepitia wasilisho ambalo ameliwasilisha Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Profesa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, mawasilisho yote yanaonyesha dalili nzuri ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pato letu la Taifa limeongezeka kutoka shilingi bilioni 141 mwaka 2022 na kwenda kwenye shilingi bilioni 148, mwaka 2023 ambayo ni sawa na ongezeko la 5.1%. Hata hivyo, tuna matamanio ya kwamba uchumi wetu utaendelea kukua kwa 5.4%, mwaka 2024; 5.8%, mwaka 2025; na asilimia 6.1, mwaka 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni matamanio na mwelekeo mzuri wa uchumi wa nchi yetu na tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa usimamizi mzuri. Pia, watu wote ambao wanamsaidia akiwepo Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika kutafuta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaanza kuongelea masuala ya uwekezaji kwenye Bandari ya Dar es Salaam kelele zilikuwa ni nyingi kweli, kwamba tunaenda kupoteza, lakini ripoti ambayo tumeletewa, uwekezaji ambao umefanyika kwenye Bandari ya Dar es Salaam umetupatia mapato na mwelekeo mzuri. Pia, tumepata taarifa kwamba ndani ya miezi mitano tu tumepokea shilingi bilioni 325.3 na haya ni mapato ambayo yanatokana na kodi ya pango na tozo mbalimbali na *wharfage*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inawezesha Mamlaka ya Bandari ya Dar es Salaam iendelee kuwekeza kwenye maeneo mengine ili tuweze kuboresha mapato yanayotokana na bandari yetu. Kipindi kile wakati tunaongea kila mtu alikuwa anaona kwamba Bandari ya Dar es Salaam imeuzwa, bandari tumepoteza, lakini sasa tunapata fedha ambazo tunaenda kuwekeza kwenye maeneo mengine. Tutawekeza kwenye elimu, afya, maji kwa mapato ambayo yanatokana na Bandari ya Dar es Salaam. Ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ujasiri wake wa kwamba ule uwekezaji upokelewe na hatimaye matunda sasa tunayaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yanayotokana na Bandari yetu ya Dar es Salaam yameongezeka ndani ya mwezi mmoja kutoka shilingi bilioni 850 na sasa yanaenda shilingi trilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni ujasiri mkubwa na kazi kubwa na maamuzi mazuri ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya. Tunasema ahsante kwa ujasiri wake, nchi yetu inaenda mbele kwa ujasiri ambao yeye ameufanya na sisi tunamuunga mkono na hatuna cha kumlipa zaidi bali tunasema mitano tena kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya niliyoyasema, niseme tu kwamba Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Rais wa Tanzania, Rais anayewapenda Watanzania na anawajali Watanzania. Ninayasema haya kwa ujasiri mkubwa kwa sababu ni sauti iliyotoka Hanang.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tarehe 3 Disemba, 2023, tulipata changamoto kidogo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliacha kila kitu chini. Leo hii ninavyoongea hapa Bungeni wale ambao nyumba zao zilienda na maporomoko, wamejengewa nyumba zao, nyumba 109 zimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiache kuwashukuru wenzetu wa *Red Cross*, tunaye Rais wa *Red Cross* hapa ndugu yetu Naibu

Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Kihenzile, alisimamia kwa karibu sana, kati ya nyumba 109 zilizojengwa, 35 zimejengwa na *Red Cross*. Tunasema ahsanteni sana na hili limewezekana kwa sababu Mheshimiwa Rais ana upendo na anawajali watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanahanang tunasema tunatambua mchango wa Mheshimiwa Rais kwenye maendeleo, tunamtambua Mheshimiwa Rais kwenye mambo ya kuwajali Watanzania wa kawaida na anajali maisha ya Watanzania. Sisi tunasema, tunavyosema mitano tena na sisi tutalipa fadhila, wakati wa uchaguzi mitano yake itakuwa ya mvua ile ya *El-Nino*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mheshimiwa Rais kushika nchi, kazi kubwa imefanyika. Kati ya maeneo ambayo Mwenyezi Mungu amenisaidia kutembelea ni Bwawa la Mwalimu Nyerere kati ya miradi ya kimkakati ambayo tunatekeleza ndani ya nchi yetu. Kwa sasa unasikia kila mtu anasema *comfortably*, kwamba yeyote yule ambaye tunaingia naye mikataba kwa upande wa nishati hatuna wasiwasi, tunaongea nao tukiwa tumetulia, tukiwa na amani wala hatuna haraka kwa sababu Bwawa la Mwalimu Nyerere linaendelea kutuzalishia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea, mashine zote zenye uwezo wa kuzalisha *megawatt* 2,115 zipo *site*, Kamati tumeziona. Mashine nne tayari zinafanya kazi, Bwawa la Mwalimu Nyerere matunda yake tunayaona, wale ambao walikuwa wanakebehi sasa aibu ni ya kwao sisi kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *SGR*, uwekezaji unaofanyika kwenye eneo la reli ukipanda unaona uko tofauti kweli kweli. Tanzania ya sasa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Tanzania tofauti na Tanzania ya maendeleo ya kuvutia. Ninaomba tu kwenye eneo la reli, sasa ianze kubeba mizigo, sisi tukizalisha ngano, shayiri, katani, mbaazi na dengu kutoka Hanang ifike Dar es Salaam na hatimaye iende duniani kote kwa haraka kwa kutumia reli yetu ya *SGR* ili tija iweze kuongezeka kwenye eneo hilo. Tukiendelea kusafirisha abiria tu inawezekana tija isiwe kubwa ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachangia kidogo eneo la kilimo, Kipindi hiki sisi wakulima ndiyo tunaenda shambani. Sisi wana-Hanang ardhi yetu ni nzuri inazalisha ngano, shayiri, mbaazi, dengu, ufuta, giligilani na vitunguu. Wakati huu tunavyosikia kwamba ruzuku inayopelekwa, pamoja na fedha ambazo tuliongeza kutoka shilingi bilioni 294 mpaka shilingi trilioni 1.24 ruzuku tuliyopata ni ya mahindi peke yake na haya mazao mengi ambayo tunazalisha nafikiri haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nami Hanang, Mheshimiwa Bashe, ananitazama, iangalie kwenye eneo la shayiri, ngano, mbaazi na dengu. Tukipeleka nguvu sasa wakati wakulima wanaandaa mashamba yao, tukaweka mkono tukawasaidia, wakati wa masoko tukaanza kuandaa kuanzia sasa. Tunawaambia Stakabadhi Ghalani, twende tukapeleke sasa elimu ya Stakabadhi Ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Stakabadhi Ghalani ni mfumo mzuri ili wakulima wapate tija zaidi, lakini mfumo ule unahitaji elimu na mifumo iliyo imara ya watu kapata fedha. Lengo la Stakabadhi Ghalani ni kwamba mkulima wakati ambapo kuna changamoto ya bei yeye aweze kupata fedha ili asiuze mazao yake kwa hasara. Sasa tupeleke fedha zifike kwenye vijiji na kata ili watu wapate fedha kwa urahisi. Wenzangu wananiambia kwa nini usitumie ule mfumo wa *NFRA* wa kununua mazao, kirahisi hivyo? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hitimisha muda wako umeisha tafadhali.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaamini Mheshimiwa Bashe amenielewa, nimeongea naye mara nyingi hili atalichukua. Ila, Wanahanang wanataka uende ukaongee nao uwape elimu wewe mwenyewe ili tushirikiane kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Samweli Hhayuma. Mheshimiwa Tumaini Magesa.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa fursa hii na ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa uhai na kupata nafasi ya kuchangia kwenye Mpango na Mwongozo wa 2025/2026. Vilevile, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ili nchi hii iwe na utawala bora na kwa shughuli za kiuchumi na kijamii ambazo zimeonyeshwa kama mafanikio kwenye nyaraka hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mawaziri wote wawili ambao wametuwasilishia Mpango na Mwongozo. Nimeipitia nimegundua kabisa kwamba ipo katika mazingira ambayo inatakiwa kuungwa mkono. Ninawapongeza wataalam, kwa maana ya Makatibu Wakuu, Naibu Mawaziri na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Mipango. Ninaamini kabisa ushirikiano wa pamoja ndiyo umetuletea nyaraka hizi ambazo sasa tunazijadili na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nyaraka hizi labda nianze na mafanikio kadhaa ambayo nimeyaona. Yapo mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka 2023, kwamba katika bajeti tuliyokuwa tumeipitisha mwaka 2023 ambayo matokeo yake sasa tunayaona huku na mpango tuliokuwa tumepitisha tunaona kabisa kuna habari ya *SGR*, kilometa 722 sasa inapitika na mimi nimebahatika kuwa msafiri ndani ya treni hiyo. Kwa hiyo, nina ushahidi wa kutosha kwamba sasa tunaweza kusafiri kwenye *SGR* kwa muda mfupi na shughuli zetu za kiuchumi zikafanyika kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika mpango huu wa sasa *SGR* isiendelee kuonekana kama ni sehemu ya kutusafirisha sisi kutoka sehemu moja kwenda nyingine, lakini ianze kushughulikia namna gani ya kusafirisha mizigo kwenye *SGR* ili tushughulike na suala letu la mapato na uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna umeme umeanza kuzalishwa kwenye Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere, nimepata

bahati ya kufika pale, kuna kazi kubwa imefanyika. Pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Rais, kuna kitu cha kufanya hapa. Hili Bwawa la Mwalimu Nyerere lisitupe furaha tu, furaha ni kwamba lazima watu wetu wa maendeleo ya jamii waende sasa kule vijijini kwa ajili ya kuwaelimisha watu ni namna gani watatumia kuanzisha miradi ili litumike kiuchumi zaidi badala ya kuendelea kutumika kama ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna idara yetu ya maendeleo ya jamii ukienda kwenye mikutano vijijini unauliza hapa mna vikundi mlivyounda kwa ajili ya uzalishaji? Wanakwambia hatujawahi kumwona. Kwa hiyo, ninaomba sana watu wa maendeleo ya jamii wafike huko. Umeme huu unaotegemea kuzalishwa kwa wingi uwe kwa manufaa ya kuinua uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote mtakumbuka kwamba ili tuonekane sasa tuna uzalishaji mzuri wa umeme, tunafikiria baada ya miaka mitano huenda tukahitaji *megawatt* 10,000. Hizi kidogo kama 4,000 tulizonazo mpango huu uanze kufikiria namna gani utatupeleka kwenye nafasi ya *megawatt* 10,000 ili tusiendelee kufurahia mafanikio haya baadaye tukakuta umeme hautoshi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna habari ya vijiji vyetu vingi sasa kuwa na umeme, baada ya vijiji vyote au asilimia kubwa kuwa na umeme mpango huu sasa ujikite kupeleka umeme kwenye vitongoji vyetu. Umeme huu usionekane tu umefika kwenye vijiji ikaonekana tayari ni *access,* lakini wananchi wanashindwa kuupata kwenye vitongoji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kukuta kijiji kimoja tu ndiyo kina umeme, vitongoji sita havina umeme. Sasa, mpango huu ujikite kuhakikisha kwamba umeme huu sasa unaingia kwa wananchi wetu kule kwenye vitongoji ili waweze kuutumia kwa ajili ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna habari ya maji vijijini ambayo nayo imeonekana hapa, ninataka kutaja vitu vichache tu. Mheshimiwa Waziri wa Maji atakumbuka kwamba Katoro ilikuwa haina maji lakini kwa shilingi bilioni 6.2 maji yamefika pale

na sasa wameanza kutumia maji na visima vingi vinachimbwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ni ombi langu, mpango huu tunaokuja nao sasa ukahakikishe kwamba wananchi wetu wanapata maji na kiwango kile cha upatikanaji wa maji vijijini ambacho ni 79.6 kiongezeke kiende hata 81 au 82 ili mwaka kesho tukija kuzungumza tuzungumze *figure* nyingine ya maji kwamba imepatikana kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vipaumbele vya mpango huu ambavyo tunauzungumzia leo, kwamba, tulitakiwa tuchochee uchumi shindani na shirikishi, hapa, ndiyo naona bado tuna changamoto. Anayetakiwa kushirikishwa ni nani? Anayetakiwa kushirikishwa ni mwananchi wa kawaida, sasa anashirikishwaje? Tukienda kwenye sekta zetu, ili tuweze kumshirikisha mwananchi lazima sekta za uzalishaji zifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba tukienda kwenye kilimo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anajua, niliomba *scheme* za umwagiliaji katika maeneo ya Busanda kule *Lake Victoria* ambako maji yanapatikana siyo mabwawa tena, lakini bado hatujafanya kitu chochote kule. Kwa hiyo inanionesha wazi kwamba wale wananchi wa kule Busanda hawatashirikishwa na ninataka washirikishwe ili *taxbase* ambayo tunaizungumzia hii, tuwe tumeitengeneza. Huwezi kuwa unavuna kodi mahali ambapo hujapaanzisha, tupaanzishe wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwa ndugu zangu wa Mifugo na Uvuvi, tuna Ziwa Victoria kule ninakotoka mimi, kwenye jimbo langu sasa nina vizimba saba, kwa hiyo jimbo zima la watu 700,000 lina vizimba saba. Hoja yetu kubwa hapa tunataka tuwashirikishe, uchumi uwe shindani, lakini uwe shirikishi. Ninaomba sana, kwenye Mpango huu sasa Serikali ijikite kuhakikisha kwamba vizimba vingi vinakwenda kwenye maeneo yetu ili wananchi hawa sasa wazalishe na kodi yao itapatikana, uchumi wetu huu tunaouzungumzia leo, utapanda na pato letu la Taifa litakua kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo yako maeneo mengi ambayo tunataka wananchi washirikishwe. Bahati mbaya sana ushirikishi wetu umekuwa siyo mkubwa sana. Tuna vijana wengi Taifa hili sasa hivi hawana ajira, tunawapaje ajira? Siyo lazima tuwatafutie kazi ofisini, tukipeleka fedha kwenye maeneo hayo ya sekta za uzalishaji wataajiriwa huko na hii nafasi ya kutoajiriwa watu itapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, katika vipaumbele vilivyooneshwa ni kuimarisha uwezo wa uzalishaji. Sasa hapa uwezo wa uzalishaji ndiyo napata changamoto. Wazalishaji wanaonekana hawajawezeshwa kule, tunaimarishaje uwezo wa uzalishaji. Kwa hiyo hoja yangu bado ni ileile ya shirikishi kwamba Serikali itenge na ifanye mipango ambayo itawashirikisha watu wengi ili tuimarishe uwezo wetu wa uzalishaji. Jirani yangu hapa Mheshimiwa Mwijage asubuhi alipokuwa anachangia alisema kwamba ana eneo karibu la hekta 7,000 au 8,000 huko (*square kilometres 7,000)* liko kwenye maji, lakini bado ushirikishwaji wake ili tuimarishe sekta ya uzalishaji bado siyo mkubwa sana. Kwa hiyo Mpango huu tunaouzungumzia leo, hebu utusaidie kwenye hilo

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia maeneo mahsusi yaliyolengwa na Mpango huu, la kwanza ilikuwa ni uendelezaji wa miundombinu hapa napo tuna changamoto. Mwenyekiti wa Kamati wakati anasoma Taarifa yake, alionesha miundombinu ya madarasa inahitaji takribani shilingi 267,000,000,000 ambazo halmashauri haiwezi kuzipata. Madarasa na maeneo ya vituo vya afya au zahanati ambazo zilianzishwa na akatoa ushauri kabisa kwamba Serikali iangalie uwezekano wa namna gani itawezesha hayo maboma ili yaweze kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mheshimiwa Mbunge humu ndani ukimuuliza, ana maboma ambayo hayajakamilishwa. Kwa hiyo tuombe Mpango huu ambao leo tunauchangia na kutoa ushauri wetu, ufanye hili. Tukiendelea kusubiri halmashauri maana yake maboma haya hayatafanyiwa kazi na tutaendelea kuyaona kila siku, yatakuwa na maswali lakini hayakamiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miundombinu iliyotajwa hapa ambayo inaonekana kwamba lazima tuijenge, kuna barabara. Nina mfano mmoja mdogo Mheshimiwa Waziri wetu wa Ujenzi atakumbuka kwamba tunatakiwa kujenga barabara, nilikuwa naiomba kila siku hii Barabara ya kutoka Mpomvu – Nyarugusu – Kakola lakini haijengwi. Hoja yetu kubwa tunataka barabara ile ijengwe kwa sababu wachimbaji wengi wako kwenye barabara hiyo, wanatakiwa kusomba mawe yao kupeleka kwenye *CIP* ambazo walizijenga siku nyingi ili wakazalishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaweza mkajua Sekta ya Madini inavyofanya, imefanya vizuri kwa sababu wale watu wanazalisha, bahati mbaya barabara ile haijengwi. Nitatumia neno gumu tu ashakumu si matusi, tusiendelee kuwekeza mahali ambapo tunajua panaweza pasituzalishie sana, tukawa tunatengeneza miundombinu ambayo ni kwa ajili ya kwenda kusalimiana. Tutengeneze miundombinu ambayo itakwenda kwenye uzalishaji, baadaye tutajenga hiyo mingine ambayo siyo ya kwenda kusalimiana. Tuhakikishe kwamba tunajenga miundombinu inayoenda kufanya uzalishaji, lakini tukiendelea kufanya hivi tunavyofanya na Mpango huu ukaenda tena usijenge barabara hizo, tutaendelea kupiga *marktime* muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata nafasi ya kwenda China katika semina moja, naona kuna mtu mmoja hapa tulikuwa naye kwenye semina hiyo, huwa hasemi. Tuliambiwa wao mwaka 1978 walianza na viwanda vya chuma, wakapambana kuwa na chuma cha kwao na baadaye wakajenga reli, wakajenga vitu vingine. Leo tuna Liganga na Mchuchuma hapa, mpaka leo yuko kwenye mazungumzo, sijajua mazungumzo yatakwisha lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipokuwa na chuma yetu, kila tunachokijenga tutaagiza chuma kutoka nje. Mfano mzuri ni huu, leo tumejenga daraja kama lile la Kigongo – Busisi, chuma tumetoa wapi na tunapokwenda kushughulika na reli yetu ya *SGR*, chuma tunatoa wapi? Kwa nini tusianze kidogokidogo tukawa na chuma cha kwetu ambayo itatufanya tufanye miradi mingi kwa sababu tunaendelea kujenga *SGR*. Kwa hiyo kuna kitu

cha kufanya hapa, tufanye maamuzi ili twende kwenye mafanikio makubwa kama inavyotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambacho nataka kuzungumzia tena hapa ni ile *gap* ya kutokuwa tegemezi…

*(Hapa kengele ililia kuashira kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magessa, muda wako ulishaisha. Unaweza ukahitimisha tafadhali.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sekunde tano hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja, nilitaka tushughulike na lile *gap* ambalo sisi tumekuwa tegemezi. Mpango wa mwaka jana ulikuwa na 29.3% ambao tunaomba mikopo na vitu vingine na Mpango wa mwaka huu una *value* ileile kwamba tuna 70.7 ambayo tunaweza kuitafuta ndani, lakini nyingine tunaitafuta nje. Tuangalie namna gani tunaweza kuiondoa hiyo 29.3%, kwenye Mpango huu tuje na wazo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tumaini Magessa.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:** Bunge linarudia.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao sikuweza kuwatangaza kabla. Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Sophia

Hebron Mwakagenda, ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninatumia fursa hii kuwashukuru sana wote ambao walipata nafasi ya kuchangia leo. Nitumie pia fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Manaibu Mawaziri wote wa Wizara hizi mbili ambazo zina ajenda Mezani, kwa ushiriki wao wa kikamilifu kabisa kupokea maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. Tumehitimisha shughuli zetu za leo.

Naomba sasa kuhitimisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.28 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 5 Novemba, 2024, Saa Tatu Asubuhi)*